

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION.**

**(C.K.R.C).**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU WEST  
CONSTITUENCY, HELD AT**

**LAMU FORT, LAMU DISTRICT.**

**ON**

**MONDAY, APRIL 29<sup>TH</sup>, 2002.**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, LAMU WEST CONSTITUENCY, HELD AT LAMU FORTON  
MONDAY, 29<sup>TH</sup> APRIL 2002.**

**Present:**

1. Com. Dr. K. Mosonik Korir.
2. Com. Mr. Ahmed I. Hassan.

**Secretariat staff in Attendance:**

- |                     |                              |
|---------------------|------------------------------|
| 1. Treza Apondi     | -Program Officer.            |
| 2. Carolly Okeyo    | - Assistant Program Officer. |
| 3. Mohamed Abubakar | -District Coordinator.       |
| 4. Asha Boru        | - Verbatim Recorder.         |
| 5. David Muturi     | -Sign Language Interpreter.  |

**The meeting was called to order at 11.00 a.m.**

**Mohamed Abubakar** (District co-coordinator): Ya kwanza ningependa kuwashukuru kwa kufika kwenu, hapa na kuweka time, lakini kasoro ni kuja kwetu kwa kuchelewa kufika hapa sisi, ama Commissioners wetu, kwa sababu ambazo wakati wa introduction nafikiri watawaelezea. Kwa hivyo kwa ufupi, kuna mmoja hapa wengi wenu mwanifahamu, mimi kama district coordinator, Mohamed Abubakar hapa, na lengo kuu ni kuwa ni kuja kusikiza maoni yenu, baada ya kutembelewa mara mbili nyuma na ma-Commissioners, kwa sababu tofauti tofauti. Kwa hivyo leo ndio hii siku ya ule mpunga ukipikwa kila siku, leo ni kupakuliwa na kuliwa. Lengo la hizo

(Inaudible) zote, ni kufikia leo hii, at the

collection of views. Kwa hivyo, bila kupoteza wakati, ningelianza hapa na ku wa-introduce wageni wangu, kisha tupate Sheikh

mmoja atutolee dua, tuendeleo na mkutano wa leo kawaida. Kwa hivyo, -sijui kama wataka ni wataje mimi ama watajitaja wenyewe? Lakini nafikiri nitaanza na program officer wangu hapa,

(inaudible) for collection of views for panel six.

**Treza:** Ahsanteni. Mimi kwa majina naitwa Treza Apondi, nafanya na C.K.R.C. kama program officer. Ahsante.

**Com. Hassan:** Salaam Aleykum. Kwa majina mimi naitwa Ahmed Issak Hassan, mimi ni Commissioner wa Tume ya Kurekebisha Katiba. Lakini kazi yangu mimi kwa kawaida ni wakili, lakini kwa sasa niko na Tume ya Katiba. Huyu mwenzangu anaitwa Dr. Mosonik arap Korir.

**Com. Dr. Mosonik:** Hamjambo? Mimi naitwa Dr. Mosonik arap Korir, kwetu ni pande za Bomet. Hii ni mara yangu ya kwanza hapa, na nimeshangaa ni mbali sana. Kawaida mimi hufanya kazi kule Egerton Njoro, kama mwalimu wa historia. Ahsanteni.

**Carolly Okeyo:** Salaam aleykum! Kwa majina mimi naitwa Carolly Okeyo, mimi ni assistant program officer C.K.R.C. Ahsanteni.

**Asha:** Salam Aleykum! Naitwa Asha Boru, mimi ni Verbatim recorder.

**David Muturi:** Habari ya asubuhi! Mimi naitwa David Muturi, mimi kazi yangu ni sign language interpreter, wa wale hawasikii. Ahsanteni.

**Mohamed:** Ahsante. Basi moja kwa moja, nafikiri nitampatia Maalim Hussein atutilie dua.

**Maalim Hussein:** Salaam aleykum. Kulingana na program, tunanyenyekeza roho zetu kwa Mwenyezi Mungu, kumuomba kazi tulojija iweze kuendelea vizuri, na malengo kutimia. Kwa vile tunataka pia, -na wageni wetu waliokuja hapa-, tutaomba kwanza kwa lugha ya dini yetu ya Kiislamu, halafu tutaeleza pia maelezo hayo kwa Kiingereza.

*(He prays in Arabic).*

**Translation in English.** In the name of God most gracious, most merciful, master of the day of judgment, thee do we worship and thine aid we seek. Show us the straight way, the ways of those ones whom thou has bestowed and blessed. Those whose worship is not wrong and who go not astray, Amin.

**Mohamed Abubakar:** Shukrani. Nafikiri bila kupoteza wakati, moja kwa moja tutaenda kwa mpangilio ambao tumeingia, na tutawaomba wale ambao wamekuja na maoni yao, ambao wamekuja kutoa maoni, waje hapa wakiji-introduce kwa majina

yao. Watupe majina yao kamili, na ukisha present, kuna register hapa utakuja kuandika jina lako, na ikiwa una memorandum yako, utatuwachia hapa. mengineyo mtaelezewa na Commissioner Hassan.

**Com. Hassan:** Ahsante Mohamed. Kwanza tunataka kuomba radhi tumechelewa. Tulikuwa tunatakikana tuanze saa mbili, hapa Lamu leo. Lakini mimi na Dr. Mosonik, tulikuwa tumetoka Mombasa asubuhi na ndege ya Air Kenya, na tumefika hapa karibu saa tano. Kwa hivyo tunaomba radhi tumechelewa, lakini tujaribu kukaa mpaka ule wakati ambao kila mtu ambaye amejiandikisha, atakuwa amesikizwa. Kwa hivyo poleni sana kwa hiyo.

Ya pili, naona kuna watu wengi wamejiandikisha, kuna wale wameandiksha written. Yaani wameandika maandishi maoni yao. Na kuna wale wameandikisha oral. Yaani watakuwa wakiongea verbatim. Tunawaomba wale wameandiksha written, wasijaribu kusoma neno kwa neno yale maandishi ambayo wameandika. Lakini wajaribu tu ku-highlight yale maneno muhimu, kwa sababu sisi ndio tutaichukua tusome. Kwa hivyo, wale ambao wameandika written submissions, don't read word for word. Just highlight the main points. Na kwa wale ambao watakuja kuongea, tutawapatia dakika tano tujaribu kuongea kwa haraka, ndio wale wenzetu wengine pia wapate nafasi.

Na pia tunawaomba wale wengine ambao wanasikiza, mtu akianza kuongea, apewe nafasi, kwa heshima, asikizwe. Hata kama huwezi kukubaliana na maoni yake, lakini ana haki ya kusikizwa, na kutoa maoni yake. Kwa hivyo hatutaki mtu awe ana kerwa, - there should be no heckling. Kwa hivyo mnampatia mtu nafasi asikizwe, yeye pia akusikize. Bila kupoteza wakati, tutamwita Bwana Abubakar Madhubuti. Tunaanza na number one kwa hii list yetu. Ahsante.

**Interjection.**

**(Inaudible).**

**Com. Hassan:** Kuna kitu kimoja ambacho pia nimesahau kuwaeleza. Tafadhali wale wako na simu ya mkono, tunawaomba waweke off. Kwa sababu tunafanya recording live kwa hii tape recorder yetu. Na itasumbua hiyo recording. Unasikia ni nyingi zinaanza kupiga already. Nawaomba tafadhali muiweke off.

**Abubakar Madhubuti:** Sasa niwaelekee watu au niwaelekee nyinyi?

**District coordinator:**

**(Inaudible)** simama hapa tu.

**Abubakar Madhubuti:** Salaam aleykum! Commissioners na wageni wetu waliokuja, tunawakaribisha katika district yetu ya Lamu. Mimi jina langu naitwa Abubakar Madhubuti, ex-member of Parliament, na maoni ninayotoa ni yangu binafsi. Na nimeshaandika memorandum yangu, nafikiri mukifika Nairobi mtaikuta katika sanduku lenu la posta, kwa hivyo nita-highlight four points only, kufupisha mambo yetu hapa.

Point yangu ya kwanza, Serikali ambayo kwamba maoni yangu niko nayo, sisi tunataka Serikali ya Majimbo. Serikali ambayo mfano wake ni Nigeria. Ambayo kwamba tunayo Federal Government, halafu tuna regions. Mfano wa pili, jambo hili si jipya. mwaka jana England, United Kingdom, wameanzisha Majimbo. Leo utaona Scotland wana assembly yao, wana legislative assembly yao, vile vile Wales wanayo regional assembly yao, na sheria zao zinatungwa huko; vile vile Ireland ya kasikazini, wako na assembly yao. Kwa hivyo nikisema Majimbo, watu wasione kwa kuwa tunarudi kinyume katika 1963. Lakini ni mambo ambayo kwamba, sasa yaendelea huko Europe. Kila nchi inanza kuondoa ule uwezo wa Serikali moja kuu, kuwapa wale wadogo wadogo. Na India, ambayo kwamba ni nchi kubwa sana, kuna Federal Government headed by the Prime Minister, na vile vile kuna regions. Hiyo ndio ya kwanza.

Ya pili, katika Katiba, mtu yeyote ambaye kwamba ni citizen wa Kenya, mbele ya Katiba anatumainiwa kuwa ni sawa na mtu yeyote. Lakini kuna sheria ambazo kwamba zinaletwa, ambazo ni sheria za ubaguzi, hivyo nataka ma-Commissioner waisikize, na waondoe sheria hizi na wazitie katika Katiba, kuonesha kutakuwa kuna uchaguzi. Kwa mfano, ukija wewe kutaka Identity card, unaambiwa Lamu iko katika border. Border maanake sisi na Wasomali. Kwa hivyo tunawekewa kikundi cha watu, - mapolisi, ma D.O. ma-special branch, wazee, ma-Chief-, ukifika kule unajieleza. Unajivua nguo zako zote. Wewe ni nani? Watoka wapi? Umezaliwa na nani? Mpaka mwisho wakisha kuhakikisha, wanakupa Identity card. Hiyo wewe ushahakikishiwa kuwa wewe watoka katika district ya Lamu, na wewe hakika ni mwananchi. Sasa umefika wewe kuenda kuomba passport, ukifika kule, ukitoa karatasi yako ya maombi, wakiangalia jina ni Mohamed, ni Ali, ni Salim, pale pale utaambiwa nenda kaleta karatasi ya shakue, maanake babu yako. Wewe, birth certificate yako, na ya nyawe au na showe, na ya babu yako. Watu watatu. Wewe unayo identity card yako ambayo kwamba umehakikishiwa huku, lakini kwa kuwa jina lako ni Salim, Ali, Ahmed, waambiwa nenda kaleta karatasi ya babu yako. Mtu yule yule ana ndugu yake. Jina lake aitwa Kimani, aitwa Njoroge, aitwa Mungai, pengine wewe na yeye ni mama mmoja, baba mmoja. Wewe umesilimu, yeye hakusilimu. Mukifika, Kimani akitoa karatasi tu, - kuzaliwa, pale pale atapewa passport. Wewe uliyesilimu, utaambiwa lete karatasi hizo ndizo zitajwe za babu zako. Kwa hivyo, ma-Commissioner, sheria namna hii ni mbovu. Kwa sababu ni ubaguzi wa kidini. Na aliyeanzisha Taifa hili Mzee Jomo Kenyatta, alikataa communal punishment. Yaani kudhulumiwa, - kuadhibiwa watu wa kijiji, au kidini au kikabila. Kwa hivyo mambo hayo yanatendeka sasa, kwa hivyo naomba katika Katiba itoke kuwa, akitendewa Mbajuni, atendewe vile vile Odhiambo alivyo Kisumu. Tumeelewana nafahamu.

Akitendewa Mbajuni hapa, atendewe yule yule Mkikuyu alivyo Kiambu. Leo wamwambia mtu lete birth certificate ya babu yako, ni kweli? Raila akienda akiomba passport ataambiwa alete ile ya babake Odinga? Ni kweli jamani? Kwa hivyo hizo ndio dhuluma ambazo kwamba tuzionazo zinapita. Kwa hivyo sheria kama hiyo ni mbovu. Sheria inatakikana iwe uniform kwa watu wote. Kusiwe na sheria ya kibaguzi.

Tatu, Kenya leo iko zaidi ya miaka thelathini tangu kujitawala. Katika kitabu hiki jana nimesoma usiku, kinaeleza je? unafikiria nini juu ya kuwa na dual citizenship? Maanake kuwa wewe ni raia wa hapa, na vile vile ukawa ni raia wa Uingereza au wa Tanzania, - wewe mtu mmoja ukawa na passport mbili? Mimi nasema, jambo hilo linamanufaa sana sana kwa wakati wetu.

Mkenyaleo namna alivyofika, anasafiri, -tumerundikiwa na watu wengi kuwa na elimu-, ni lazima tuwe na citizenship mbili. Nitawapa mfano. Bwana Korir unawafahamu wanariadha wetu ma-athlete, wale wawili au watatu, ambao wanakwenda Ulaya kukimbia. Wakirudi hapa, letu kubwa ni kuwatuza.- kupewa nishani ya dhahabu, nishani ya fedha, basi. Lakini ndani ya mifuko yao...horrible. Watu masikini. Lakini oh, wakifika 'nchi imekuwa kubwa kwa sababu mmekimbia vizuri,' sasa hawa watu wetu wanariadha, wanapokimbia wale Wazungu wakiwaona, waona kuwa – aah! fulani – Madhubuti hodari kukimbia-, Kipkorir hodari kukimbia. Waambiwa kimbieni kwa jina la nchi yetu. Lakini huwezi kufanya hivyo mpaka ubadilishe uraia. Kwa hivyo hawa ndugu zetu wakabadilisha uraia wakawa wao sasa ni Wazungu. Habari ilipokuja Kenya tukawalaani. Lakini, leo watu wale ni matajiri ajabu, kwa sababu wanakimbia kwa jina la Wazungu, na senti wanazopata hawaweki Uzunguni. Wamenunua mashamba makubwa katika former white highlands. Wengine wamenunua manyumba mengi Mombasa, Nairobi, -na mmoja namjua mimi, amenunua na hoteli haswa, ya ki-tourist. Hiyo ni moja. Kwa hivyo ni faida kwetu sana.

Pili, wale ambao kwamba ni wagonjwa, siku hizi wakienda India, kuna hospitali moja kubwa sana. Wakenya waipenda, inaitwa Hinduja hospital. Hinduja ni ndugu wawili ambao kwamba wana biashara kubwa katika dunia. Sasa biashara zao, wameingia mpaka wamefika Ulaya, Uingereza. Katika nchi zilizokuwa zikitawaliwa na communists, nchi zile, zimekuwa zikiuza vitu vyao kwa urahisi. Ma- industry makubwa makubwa yanauzwa kwa urahisi, mandege,

**Com. Hassan:** Mheshimiwa please try and summarize.

**Abubakar Madhubuti:** Kwa hivyo hawa Mahunduja wamekuja Uingereza na wameomba citizenship, ili wapate mikoko kuenda kununulia vitu kule Ulaya. Si kwa kuwa wao hawana, la. British Government inaruhusu mwananchi wa Kiingereza kuweza kupata mikoko kuenda kununua vitu. Kwa hivyo India imetoa ruhusa mtu kuwa na citizenship mbili. Na hapa naomba tufanye hivyo.

La mwisho, naturalization of citizens. Kenya, tuna watu wengi wameomba citizenship. Wao wa kutoka Ulaya, wakitoka wapi, wapi, wakija wanaomba naturalization. Kitu ninacho omba na ninasisitiza, ni kuwa yule anayekuwa citizen by naturalization, awe na haki kama mtu mwingine; - biashara, nini, isipokuwa asiruhusiwe kuingia katika Parliament. Asiruhusiwe kuwa Rais wa nchi hii. Ni hii ni (Inaudible) ambayo kwamba ni mpya. Hii ni Katiba iliyoko America, ambayo inasema mwananchi yeyote ni sawa mbele ya Katiba, isipokuwa hawezi kuwa Senate, au member wa House of Representatives, au kuwa yeye ni Rais. Kwa mfano, Dr. Henry Kissinger. baada ya Nixon ilikuwa watu wengi sana wakifikiria Kissinger atakuwa Rais wa ile nchi. Lakini kitu kilichomzuia, - the only thing that barred him was the Constitution of America, that you had to be born in America, rather than just to come as a naturalized citizen.

Kwa hayo machache ahsante.

**Clapping.**

**Com. Hassan:** Ahsante sana mheshimiwa. Ningependa wale ambao watamfuata mheshimiwa, wajaribu kutupatia recommendations. Wasijaribu ku- justify. Ukitoa maoni, jaribu kuitoa in the form of recommendations, ndio tuweze kuchukua point forms. Wa pili ni Noor Salim Omar. Noor Salim....

**Noor Salim Omar:** Salaam aleykum!

**Com. Hassan:** Aleykum Salaam. Naona muna written submissions? Jaribu ku-highlight the main points please.

**Noor Salim Omar:** Naam. Jina langu ni Noor Salim Omar, mimi ni mwenye kiti wa shirika la kina mama la Maendeleo ya Wanawake. Kwa hivyo, sisi Maendeleo ya Wanawake Organization -ni shirika la kina mama-, memorandum yetu imehusu mambo ya kina mama. Na sisi kama kina mama, tulipokaa tukatoa hii memorandum, tulikuwa tuna-negotiate, tunapigania for affirmative action. Moja. Mbili, for provision of a framework which will eliminate the objects that hinder the advancement of women. Tatu, for the removal of gender based discrimination. Nne, for an implementation mechanism to be entrenched into the specific pieces of legislation to affect the above.

Tano, women interests should be fully guaranteed in the Constitution. Na tumetoa recommendation zetu, lakini nimeambiwa nisizisome moja kwa... moja hata moja. Kwa hivyo, nitazi-highlight. Sana kwenye hii affirmative action, tumesema kwamba twataka one party representation in Parliament and local Government for -of women. Kisha pia, tumetoa specific strategies. Na pia twataka posts in employment, twataka education opportunities, especially the girl child education should be re-invented. For example, when – special bursaries for all girl child education. Kisha pia tumesema, ni lazima kuweco the creation of an institutional framework, to conduct the affirmative action. Kisha pia twataka programs za akina mama za mikoko na akiba, ziwe supported. Kuwe kuna infrastructure ambayo would support loan and credit facilities for women. So that we raise women income level.

Kisha pia, twataka enactment of legislation of affirmative action, by the relevant law making organs. Hayo yote yako kwenye memorandum yetu. Kwa hivyo tuna specific strategies, kisha tuna political parties, tumesha kusema kwamba we want representation, the electoral system and process. Pia tumetoa recommendation zetu za Electoral Commission, appointment of Commissioners. Pia tumetoa recommendation zetu, tuna basic rights, tumetoa recommendation zetu, Local Government tumetoa recommendation zetu, kuna land and property rights, tumetoa recommendation zetu. Pia katika Constitutional Commission, na Constitutional offices, tumetoa recommendation zetu. Tumesema pia kwamba twataka Commission of Gender Development, with at least 50% women representation to be entrenched in the Constitution, with an aim to maintain gender parity in development planning.

Pia, katika the legislature, tumetoa recommendation zetu, na la zaidi tumeongeza kusema Parliamentary gender parity should be

Constitutionally provide for. Kisha participatory Government, tumetoa recommendations zetu. The Constitution should provide for greater participation of women in Government. Hiyo ndio kwenye memorandum yetu –A. Memorandum yetu – B, ilikuwa ni yale ambayo yalijitokeza tulipokuwa tunatoa elimu ya uraia kwa kina mama na vijana. Kwa hivyo, some of the Constitutional issues said by women during our civic education discussion, moja ilijitokeza - Mwanamke wa Kiislamu akifiliwa na mumewe, huwa yuko kwenye eda. Eda, ni state of seclusion ya miezi minne na siku kumi. Hiyo haiko provided kwenye Constitution, kwa mwanamke yule apewe leave. Kwa hivyo mara nyingi, baada ya kuwa ni mjane, ana dhiki ya kufiliwa, na hua huna hamu kuwa nikimaliza eda, nitakosa kazi. Kwa hivi recommendation ni kuwa, women get a special leave whether paid or unpaid when in this state. Hata kama ni unpaid, lakini tuhakikishe kuwa ukimaliza eda, warudi kazini.

Kisha kuna mambo ya passport, I.D. cards and birth certificate. Majina ya Kiislamu yakionekana, kama ilivyoelezwa, huwa ni lazima utoe document zaidi. Recommendation: there should be no discrimination on requirements to acquire identification documents; so that wote wawe treated sawa. Isiwe huyu atakuwa ni vingine na huyu vingine. Kisha tumeona habari ya miraa. Ilijitokeza sana wakati tulikuwa tuna-provide civic education, kuwa miraa ina athari sawa na bangi, sawa na unga. Kwa hivyo twataka legislation iwe enacted. Our recommendation: it should be treated by law like all the other banned narcotics. Iwe ni sawa kwa sheria kama mtu akishikwa na bangi, akishikwa na unga, akishikwa na miraa, iwe ni hivyo hivyo.

HIV/AIDS. Hii pia ilijitokeza sana, habari ya ukimwi.

**(Clapping).**

Kwa hivyo tukaona contributing factor ni kwa sababu ya ndoa, na talaka nyingi. Kwa hivyo tukasema katika recommendation zetu, mtu yeyote ambaye ataka kuoia sasa, iwe ni lazima awe atapimwa, ajulikane kama ana ukimwi ama hana. Na la pili...

**(Clapping).**

Katika recommendation zetu ni kuwa, tunaona huwa kuna watu hujijua wana ukimwi. Haitakiwi muwaseme kuonekana wana ukimwi. Na kina mama na wazee, hatusemi ni wazee pekee yao. Kisha akaachwa yule bwana, ama akafiliwa na akaolewa tena. Kwa hivyo, ikiwa mtu atamwabukiza mtu kwa kujua, sisi recommendation zetu ni huyo mtu ashtakiwe. Iwe kuna sheria ya kumfuata. Ikiwa amepimwa na anajua ana ukimwi na akaficha hali yake ya kiafya. Kitu kingine ni substance abuse. Ambayo watoto wetu sana walijitokeza, sisi tulikuwa na tournament ya Katiba cup 2002, kwa hivyo katika kutoa heshima uraia wa vijana, hii ilijitokeza sana, kuwa kijana akishikwa na unga yeye huwa ni mgonjwa. Yule naye, - yule auzaye, ule anaye unga huwa ni mgonjwa. Kwa hivyo mara nyingi hupelekwa jela, na hiyo si rehabilitative. Kwa hivyo tunataka legislation iwe enacted. Serikali ilazimishe kujenga rehabilitation center in every district hospital. Watoto wetu wakishikwa ni ugonjwa, wawe watapewa matibabu ya bure hospitali...

**(Clapping).**



Necessary treatment and counselling, katika wale drug substance abusers. Pia tukaona kuwa hakuna parole provided in our Constitution.

**Com. Hassan:** Madam Noor, jaribu kufafanua maanake unga. Ukisema unga ni nini?

**Noor:** Unga kama cocaine ama heroin. Kwenye Constitution nimesema ni substance abuse. Kwenye memorandum yangu. Kisha parole. Huo ni ule msamaha ambao hauko provided kwenye Constitution . Mpaka sasa sisi tunayo Presidential decree. Lakini sisi twataka mtu akifungwa, ikiwa kifungo ni cha miaka mingi, ataambiwa kortini kuwa wewe utafungwa miaka ishirini, lakini baada ya miaka kumi, you are eligible from parole. Kwa hivyo mpaka kule jela, uwe uta behave vizuri, na ukitoka jela u-behave vizuri. Kwa hivyo hiyo ndio sisi twaona ni rehabilitation. Hiyo ndio itamtengeneza mtu kitabia.

**(Clapping).**

**(Inaudible)**... baada ya miaka ishirini, baada ya miaka kumi na tano, Serikali itaamua kumsamehe, ikatutupia sisi yule mtoto, hajui ataanza wapi. Kisha kitu kingine ambacho tulisema, sisi, sheria yetu yaruhusu mtu kuoia wake wengi, na hiyo twakubaliana nayo, kwa sababu ni sheria yetu; hatupingani nayo. Lakini ilijitokeza kuwa watoto hawaangaliwi kisawa sawa, wale ambao huwachiwa yule bibi. Kwa hivyo, tukasema, mtu kabla hajaoa mke wa pili ambaye ametupa yule bibi wa kwanza, iwe kuna kamati, - ofisi ya Kadhi. ambayo itakwenda kuchunguza nyumba ile ameitupa, aliiacha sawa sawa kabla ile hajaidhinishwa kuoia mke mwingine.

**(Clapping).**

Kwa hivyo kamati ita-address na ita-approve. Kisha kitu kingine kilichojitokeza ni habari ya marriage certificate from Kadhi. Cheti chetu kutoka kwa Kadhi hakiheshimiwi, tukiwa twataka kuitumia kama supporting document. Sasa ikiwa wewe una bwana, na ataka kusafiri na wewe, uwe ni ile haitumiki kama supporting document, uambiwe nenda kwa D.C. ukachukue affidavit. Kwa hivyo twataka cheti chetu kidhaminiwe kama cheti cha haki zingine zozote. Tusiende tukarudi kwa D.C. tukatafute affidavit.

Kisha, kuna hii district committee. Tumesoma mfano land allocation committee, **(Inaudible)** committee, district education board, hospital management board. Hakuna women representation. Kwa hivyo twataka affirmative action. We want representation of women in all these committees. Maanake maisha yetu yahusika kwenye kamati hizo. Kwa hayo, naona nisipitilize kusema mengi, nikapoteza wakati wa wengine, nashukuru sana. Ahsanteni

**(Clapping).**

**Com. Hassan:** Ahsante sana Madam Noor kwa hayo maoni mazuri ambayo umetoa, tafadhali ujisajili kwa Commissioner.

Mheshimiwa umesha jitia hapo? Okay. Watatu ni Abdulrahman M. Bilali. Naona pia wewe una- written submissions. Jaribu pia ku- highlight kama Noor.

**Abdulrahman Bilali:** Ahsante sana kwa kupata fursa hii. Kwanza ni kushukuru Mungu zaidi, kuweza kuafikiwa kutafuta karatasi nyingine na mwongozo mwingine ambao utasaidia wale watu ambao wamedhulumiwa katika nchi hii. Ima kwa karatasi hii iliyoko, ama kwa mambo ambayo, kule kufuatiliza hii karatasi ikawa hakuna mfuatili wa kisawa sawa, -representation kutoka yale makabila ambayo yameweza kudhulumiwa. Mimi nimeandika three memoranda, na zote zinakusudia mahali pamoja, - lakini nimefungua. Ya kwanza nimesema the participation, - the voting system-, the ethnic participation. Yaani namna ya ku-vote, na uwakilishi wa makabila madogo.

Ya pili nimesema, the political representation of ethnic minorities of Kenya. Sasa, baada ya kupewa - participation ya kupiga kura, wakakuwa viongozi. wao wawakilishwa vipi?

Na ya tatu ni the Parliament of Kenya. Ningependa Bunge la Kenya liwe hivi: -sasa twaambiwa kufanya kwa ufupi, ni kwamba shida nyingi – kwanza nataka kusema, ni nani wale tuliokusudia

(Inaudible) yetu iitwe ethnic minority? Wale wachache ambao mimi nataka kuwafikiria katika (Inaudible) . Wa kwanza, ni ethnic minority communities. Zile kabila ambazo zina watu wachache katika nchi. Wa pili ni ethnic marginalized communities. Badala kuwa kuna kabila za watu wachache, kuna kabila ambazo zimetengwa, hazijulikani. Kabila ambazo katika zile kabila arobaini hawakutiwa, kabila zile ambazo hata wale ‘and others’ ati makabila arobaini Kenya, -katika Katiba iliyoko sasa, kuna makabila mengine yameandikwa ‘and others’ Sasa hao, - maanake ‘na hao nao.’ Basi kuna makabila mengine ambayo ‘na hao nao...’

**Interjection. From the audience:** sema. Au sio?

La tatu, minority inakusudia nini dini? Inakusudia dini ambazo zina watu wachache, kama za Kiislamu, za Kihindi na dini zingine. Kwa hivyo, namna gani watu hawa wamekuwa affected, - wamedhulumika katika nchi hii? Nimeeleza katika memorandum zangu, na baadhi ya mambo haya yamezungumzwa na viongozi waliopita, na ambayo yako pale ndani sikutaka kuyataja. Mambo ya haki za uraia na haki zingine. Na vile vile, wazungumzaji wengine wakazungumza mambo ya ardhi na mengine, yote haya mimi nameyataja, sikutaka kurefusha, kwa sababu nimeambiwa nisirefushe sisi

(Inaudible). Lakini mambo ambayo ni muhimu, nitataka kuyazungumza, ni kwamba kiasi ambacho watu wadhulumika katika ardhi, kiasi ambacho watu wamedhulumika katika haki zao. Jambo la kusikitisha ma-Commissioner katika nchi hii, ni kwamba there are people uncivilized, - can you imagine? There are tribes ambazo tukiwatia katika kundi la uncivilized, watu ambao hawaja staarabika. Kuna watu ambao hawawai nguo katika nchi hii. Forty years of independence, there are people hawawai nguo. Kuna watu ambao, tajiri mmoja katika nchi hii, aweza kulala kwenye mbingu. Na kuna kabila nzima, hawana nyumba, hata ule mvule wa ki-Orma hawana. They don’t have hata mvule. Where is this Government? why is the Constitution

(Inaudible) to this Government for neglecting these people? And

(Inaudible) to

the Constitution , for not protecting these people?

Sasa tutawafanya vipi hawa watu? Hao tuliowataja na sisi makabila madogo, na sisi dini ndogo? Tutafanya vipi sasa watu hawa waweze kupata haki zao? Je? ni kuweka katika Katiba protect the rights of the minority? Iko katika Katiba ya sasa, 'Protect the rights of the minority.' 'Protect the rights of all religions.' Iko bado katika Katiba iko.

How? Namna gani sisi tutawafanya hawa minority wawe protected? Ndio mimi, muhimu sana nataka ku-highlight kidogo tu, ma-Commissioner munipe nafasi, sitakwenda na mbio sana. Ya kwanza ni kwamba, ni kuwapa makabila madogo, na kuwapa dini ndogo, political power, political stability, political representation, political participation and recognition ya kutosha. Waweze kutambulikana kisiasa, waweze kushiriki kisiasa, waweze kujihusisha kisiasa, waweze kuwa wao watakuwa na bendera ya kusema kwamba sisi twataka Rais huyu, lakini sasa hatumtaki huyu, sisi twataka mbunge huyu, sisi hatumtaki huyu. Namna gani? Kama ni kuchagua, - kama inavyo chaguliwa sasa hivi, -Dar tulikuwa tukichagua President, ni mambo ambayo minority, na marginalized tribes hawana uwezo wowote.

Tumeona 1992, na 1997, a prominent Luo akisimama, 95% ya Luos *watamu-votia* yeye. A prominent Kalenjin akisimama, 95% Wakalenjin *watamu-votia* yeye. A prominent Kikuyu akisimama, 95% *wanamumu-votia* yule Mkikuyu. Hii nchi inakwenda katika misingi ya kikabila bwana ma-Commissioner. Kwa hivyo Katiba yetu itakayotungwa mara hii, iangalie katika misingi ya kikabila, kushinda kuangalia misingi ya ki-mwananchi. One man, one vote actually. Lakini kwa sababu ya kulinda haki za majority, mimi nimegawanya matokeo ya kura za President mara tatu. Mara ya kwanza, nimesema tutawapatia, - tutafanya direct one man one vote, we give them a 40% result, katika 100% ya wale watu walioko nchini. Tutatoa hizo results. Nimeandika vizuri -hata kama haitafahamika-, katika karatasi yangu utaona kwamba the 40%, tutawapatia haki ya kupiga kura moja kwa moja. Ili majority nao, ule uwezo wao wa kuwa wengi pia wapate haki. Naitetea minority pekee yake.

Number two, tutapatia proportional voting ya 40%. Hii 40% ya hii proportional voting, itakuwa ni kila kabila iliyoko katika hii nchi itapewa percentage yake. Mfano kabila, -nchi hii ina makabila arobaini, - ni zaidi, ni mfano nasema-. Kila kabila itakuwa 1%. Sasa wewe *wa-votiwa* na wakikuyu wote, 70% itakuwa Wakikuyu *waku-votie* wewe. Itakuwa proportion yako wewe katika results ni 0.7% katika hii 40% ni 0.7%, ya results za nchi nzima. Kisha kati ya nchi nzima wewe umepata kura laki...- milioni mbili, na kura ni milioni sita, wewe utakuwa umepata 14 point something percent, ya nchi nzima

(Inaudible) report. Kisha tutaingia kwenye zile kura za misingi ya kidini. 20% zilizobaki tutagawanya katika misingi ya kidini. Wale watu wawekania kuwa huyu ni Muislamu, na huyu ni Mkristo, huyu ni Mhindu, huyu ni Buddhist, huyu ni nani, huyu ni nani. Hapa mimi nimependekeza, the Christians, -kwa sababu hao they have got 80%, ile 25% haiko, ndio tukadanganya. We have more than 80% Christians.

**Com. Hassan:** Abdulrahman please try to summarize.

**Abdulrahman Bilali:** Yes. We are giving them 10% against 30%. And we are giving Muslims 5% and the other 5% we are giving to the Hindus and others. Hapa ikiwa kutaweza kupewa kura, na kuchagua Rais, committee ingetuchagulieni, kwa kweli itakuwa sisi tuliwaweza... –mimi nawaambia hapa kwamba President atateuliwa regardless of your version atakwenda mpaka kwa Watanye, mpaka kwa Wagoni kutafuta kura. Kwa sababu kwake (Inaudible) kule, kuliko kwenda kusadiki kura za Wakikuyu ama za Wajaluo, hawa kabila kubwa. Njia ya pili ambayo, -tumesha sasa kuchagua Serikali, Serikali imeingia, njia ya pili itakuwa ni kwamba, - kuna prosecution Constitutionality. Constitution tuweze kuindika, watu washapewa haki za *kuvoti*, kwa namna ambayo wanachagua watu kwa fikira zao, na watu watafaulu. Kisha kuna Constitutionalism. Hii Katiba itatengenezwa vipi? Tutaipeleka vipi? Nimependekeza, katika mambo hayo, ya kwamba ikiandikwa karatasi tu, na karatasi iende, halafu tuwache Bunge hili ambalo liko hivi sasa, ambapo Bunge hili kuna kabila moja ina Wabunge thelathini. Kuna kabila lingine lina Mbunge mmoja tu. Jamani yanapatikana wapi haki? Kisha kuna makabila mengine, hayajaingia forty years. Kuna makabila hapo hayajaingia forty years, another hundred or something years, hawaingii kwa sababu haya makabila mengine kwa sababu ya advantage na nini, na hao wamechukua mambo wainuka, makabila mengine yaanguka chini zaidi. Sasa mimi nimependekeza kuweko na nyumba mbili za Bunge.

The Parliament is a composition of three institutions. The President, ingawaje mimi sitotaka kutoa President wa nchi, katika nchi ya ki- Africa, kumpokonya mamlaka kabisa, lazima awe na mamlaka fulani. Tutapatia the President, - tutapatia the house of commons. Hiyo ndio nyumba mbili. House of commons ni Wabunge ambao wataingia katika misingi ya constituency. Then, tutaunda Bunge lingine, -mimi napendekeza tutaliita 'Ethnic houses.' Ambapo ethnic houses, ndani kila kabila zile ambazo ni marginalized, sio kabila kubwa, zitakuwa zina one representative. Minority tribes, kabila ndogo zetu zitakuwa zina one representative. Dini ndogo, zitakuwa zina one representative. Kisha wale watu ambao wamedhulumika, physically handicapped, wawe na one representative. The blind and the deaf, one representative, kila mtu. Kisha vile vile wanawake, nimependekeza mimi, watoke three, wanawake katika each province. Sasa kwa nini nimeweka mabunge mawili? Nyumba mbili? Bunge ni moja, nyumba ni ngapi? Ni mbili. Nyumba ya kuwa inataka kupitisha mambo kwa sababu majority wengi kule,

(Inaudible) hawa wa pili walitoa Katiba wakasema ala, hawafuati masilahi kweli. Na hii ikipinga, hii tutajua huwa haiwi enacted. Mpaka Wabunge wote waende wafanye nini... pande zote ziwakilishwe. Kama Uingereza kuna the House of Lords, kuna the Common house. Sisi tutakuwa na Common House, tutakuwa na Ethnic House. Hapo ndio pekee yake twaweza ku-vary kuangalia kwa matata baada ya Katiba mpya ikipangwa. Baada ya kwamba minority awe voted with the proportional votes. Sasa, wale ndio wanaangalia masilahi kwamba ile Katiba yatengenezwa vizuri, na mambo kama hayo. Kwa hivyo ndugu zangu, nimeambiwa nifupishe, nimeandika three proposals yaani memoranda, na hizo zote ziko na hawa. Na ile ambayo nimetaja labda, itakuwa ni kwa ufupi.

Dakika moja tu Bwana Commissioner. The systems of Government. Tunataka Serikali sisi, baada ya yote hayo ikishafanyika. Sasa ni Serikali ambayo imeunganisha. Serikali ya Majimbo, na system ambayo ni hi-breed system. Hi- breed system ni ile system ambayo President huku anao uwezo wake. Na Prime Minister huku anao uwezo wake. Rais awe ni kiongozi wa nchi, na Prime Minister awe ni kiongozi wa Serikali. Serikali ineleza tutampa uwezo gani Prime Minister, mpaka hapa kuendesha

Serikali. Na Rais naye, nimemuweka mahali ambapo atakuwa yeye, institutions kama atachagua yeye,

(Inaudible) Parliament, ambapo Parliament ni hizo nyumba mbili.

Ni watu ambao wataangalia masilahi ya wananchi. kwa hivyo Rais atakuwa anachunga mambo hayo.

**Com. Hassan:** You have taken more than your time. Please summarize now.

**Abdulrahman Bilali:** Okay, okay. Kwa hivyo ndugu zangu, (Inaudible) point nyingi sana na wakati ni mdogo. Ningependa kila na moja hapa, aseme wazo kama vile ambayo mimi nimetoa. Kwa hayo, Asalaam Aleykum Warakhmatulahi Wabarakatu.

**Com. Hassan:** Tumeshukuru sana Bwana Rahman. Kwa hivyo utupigie signature kwa hiyo register. Mtu wa nne ni Ali Gubo.

**Ali Gubo:** Asalaam Aleykum. Nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

**Com. Hassan:** Hebu ngoja kidogo. Tafadhali tumpatie nafasi Bwana Ali aongee.

**Ali Gubo:** Hata kama mtu hapendelei ile maoni nitatoa lakini anyamaze, tafadhalini, anyamaze asikize. Bwana Commissioners na wageni mashuhuri, na akina mama, wazazi wangu, Salam Aleykum. Mimi nashukuru kupata nafasi hii, lakini nilikuwa nimeandika memorandum yangu, na bado haijakuwa tayari, mimi naitwa Ali Gubo Ballo, ni councillor wa kule Hindi, na pia ni mwenyekiti wa Boni community self help group. Mimi maoni yangu ni kidogo tu. Hii kabila hii ndogo, ambayo alikuwa, bwana mmoja hapa alikuwa amefananisha kusema, makabila arobaini na mbili na wengineo, sisi tuko kwenye wale wengineo. Wale wengineo ambao hawakutajwa hawako kwenye hesabu. Sisi kutoka Kenya hii, kabla haijapata uhuru mpaka imepata uhuru, hatujapata faida yoyote. Hatuoni mabadiliko yoyote, ya kusema kama sisi tumepata uhuru. Hiyo area ambayo hiyo kabila inakaa, ni area ambayo hakuna mwenye haki ya chama, hakuna mwenye haki ya nyumba, hakuna mwenye haki yoyote. Hakuna mtu yeyote hata mmoja, sisi tunasikia kama anatolewa haki ya ardhi, tunasikia wana Kenya wana haki ya kupata maji safi, nasikia kama Kenya wana haki ya kupata barabara nzuri, tunasikia lakini hatuna habari hiyo kwa sababu hatujulikani. Twaomba Katiba wakati huu, itutambue, tujulikane na sisi kwamba ni Wakenya, - kwa sababu wale Wakenya wanakaa kule Kiambu, Kisumu, Thika, ni sawasawa na wale watu wanakaa Kiunga, Marani, Maangai.

**(Clapping).**

Kama mimi nikiwa mtu nikwa Mmangai, nitahukumiwa sheria ile ile inahukumiwa mtu wa Nairobi. Kwa nini sisi hatupati barabara, - barabara inatoka Thika, inatoka Nairobi inaenda Thika, na ile inatoka hapa inaenda Kiunga hebu muangalie. Kwani sisi si Wakenya? Kwa hivyo Katiba ya sasa tunataka irekebishwe iwe Wanakenya wote wawe sawasawa. Wanakenya wote

wawe sawasawa. Kama sisi hatuna kipande ya kura, Serikali haingetujua. Sasa Serikali inatujua tuna kipande ya kura. Ile kura ndio wanakuja kufuata. Lakini ndio tufanye namna hiyo, tunataka kila....

**Interjection. *Laughter.***

Kama hatuna kura hatunge-julikana kabisa. Kwa hivyo Katiba hii twaiomba, tunataka isawazi...(End of side A of tape one).

*Continuation from side A:* --haiwezi kumpeleka Mbunge aende awakilishe Bungeni. Kwa hivyo tungeomba, hata kama ni watu hawafiki kiasi kile kinatakikana ya Bunge, - Mbunge kuenda Bungeni, lakini ile Katiba iwe ni

(Inaudible) itakayo kuja wachaguliwe makabila madogo dogo, wawe na Bunge yao. Hata kama hawafiki....

**Interjection.**

**(Inaudible)**

Ile makabila madogo madogo wawe na Bunge yao, hata kama ni watu mia tano. Kwa sababu, ile haki, - haki idumike. Kwa sababu hizo kabila pia madogo madogo kuna watu walisoma. Wale Wabunge walisoma, -si hata wale Wabunge wako Bungeni walisoma, wako, lakini hawawezi, kwa idadi ya watu, watu elfu saba, elfu kumi, elfu ishirini ndio wanatakikana mtu aende Bungeni, na wao hawawezi kufika elfu tano. Kwa hivyo ile Katiba ya sasa kuwa ningeomba, ningeomba Katiba ya sasa iruhusu, kila kabila awe Bungeni apate kuwatetea, nao wajisikie kama Wakenya. Kura ikipigwa, ya ile kabila... kabila ya Kiboni, tuseme kwa mfano, au Watanye, tujue inathamani kuliko kura hamsini ya kabila ingine, kwa ile sehemu. Kura ikipigwa ya Kiboni ama ya Kitanye, ile ina thamani kuliko kura hamsini. Kura moja ya Kiboni ina thamani kuliko kura hamsini. Kura moja ya Kiboni ina thamani kuliko kura hamsini ya kabila ingine. Katiba ya sasa kama inatukumbuka sisi tuwe, -tujisikie kama Wakenya, tutafurahi sana. Majimbo pia – twaomba system ya Majimbo pia ianzishwe. Kwa sababu gani? Sisi pengine tukipata Majimbo, tutakuwa sisi makao makuu ya Serikali yetu itakuwa ni mkoa, mkoa wa hapa, - mkoani kwetu, na pengine sisi tutakumbukwa itakuwa kazi nyingi hakuna, kuliko

(Inaudible) kwa watu wetu, na hayo makabila mahali

wanaishi, haya makabila walikuwa wakizungumzia, mahali wanaishi, kuna mali asili. Kuna wanyama wa pori, kuna miti, kuna samaki, kuna kila aina ambayo sisi wenyewe, -revenue inapelekwa huko Nairobi; lakini barabara ikitengezwa, msaada ikitoka, inakwenda kutengenezea huko, huku kwetu hairudi. Kwa hivyo naomba Majimbo kwa ajili hiyo.

**(Clapping).**

Yaani mali yetu iwe inafika hapa. Kuliko sisi tunatuma Nairobi, watu wa Nairobi wanapeleka Kiambu. Haswa naomba Majimbo kwa sababu hiyo. Maanake mtu atakuuliza kwamba kwa nini wataka Majimbo? Majimbo nataka ile mali yetu iishie hapa hapa, ardhi yetu iishie hapa hapa, kwa watu wa hapa hapa wenyewe. Hiyo makabila madogo madogo, ardhi yao badala ya kupewa, -kila mmoja apewe ardhi fulani. Ardhi yao mahali ambapo wamechagua. Wapewe kwa pamoja. Wapewe, wenyewe watajua namna ya ku

(Inaudible). Kwa hayo machache jamani nashukuru sana. Ahsanteni

sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana. Bwana Ali Gubo, kwa hayo maoni. Sasa wa tano ni bwana Ali Sheikh, ambaye

(Inaudible) Commissioners.

**Twahir Sheikh:** Asalaam Aleykum Warakhmatulahi Wabarakatu. Karibuni Lamu ma-Commissioners ambao wamekuja kututembelea sisi hapa. Sisi kama wakazi wa Lamu district, na tuko makabila nyingi na leo ni siku ya kutoa maoni, - yangu binafsi, si ya chama cha Kanu-. Ni maoni yangu binafsi. Tumesikia mambo mengi ambayo wanalaumiwa ma- Commissioner, kwa kufanya kazi yao kwa wakati ule unatakiwa. Ma-Commissioner ni watu ishirini na nane pekee yake ambao wanaangalia mambo ya Katiba. Kwa ishirini na nane pia, hawakui kitu kimoja, kusema sisi tumepitisha hivi, hebu tupatane. Itakuwa vipi, maoni ya watu, milioni kumi, Kenya ni milioni thelethini. Katika milioni thelathini, one-third watapiga kura. Na one-third wote wataka kuchukuliwa maoni yao. Katika haya, ni wao, - wengine ni wenyewe mmefanya, lakini hamkufanya publicity. Wengine mpaka sasa hawajui Katiba ya kwanza ni nini? Kenyans wengi, hata Katiba ya kwanza hawajui Katiba imeandikwa kitu gani ndani? Sisi hupenda, - mambo yameendelea. Ingefanyiwa, Katiba ya kwanza ni hii, na sasa draft ya Katiba mpya ni hii, tunaweza kutazama point, point, point; tunaweza kumaliza Katiba hii kwa mapema sana.

Ile miaka miwili amepewa, tungepatiwa sisi time hiyo, kitambo ingemalizika. Kitambo ingemalizika. Lakini kila mtu anatoa maoni, unakwenda kusanya maoni ya watu wa – milioni kumi. Hakuna haja kulaumiwa nyinyi ma-Commissioner, kusema nyinyi hamkufanya kazi, na mambo hayo yamekwenda nyuma, lazima watu wafikirie, hawa ma – Commissioner ni watu ishirini na nane pekee yake. Na sisi tumekubali, - maoni yangu binafsi-, kuongezwa huo muda na hiyo Katiba imalizike. Lakini maoni yangu, mimi nataka election ifanyizwe according to Katiba ya kwanza, katika hiyo December, na Katiba iendele kurekebishwa kwa vile ambavyo imepangwa, kusema naweza kumaliza twenty three months ama twenty four months. Lakini election, - maoni yangu, tunataka election ifanyike katika December. Maanake tunaweza kufanya mambo mengi ya maendeleo. Watu wengi wa Kenya, kila mmoja anatarajia, election itafanywa lini? Lakini kama tunasema election, lazima tumalize Katiba na ifanywe, itachukua muda mrefu. Kwa hivyo maoni yangu ni Katiba iendele kurekebishwa lakini election iwe vile ambavyo imepangwa.

Mambo ya Majimbo. Nchi ya Africa, Majimbo haina faida yoyote kwetu. Hakuna faida yoyote kwetu kwa ajili hiyo mambo ya Majimbo, - mimi binafsi siungi mkono. Mimi pekee yangu siungi mkono. Kwa ajili, tulieni, na musikize kitu gani nazungumza, yeyote ambaye anapata, kama wewe councillor wewe, unazungumza huko nyuma. Unyamaze na usikie kitu gani nazungumza. Sio chuchuchu huko.

**Interjection. Laughter.**

Na ameongea wewe. Usha fahamu sio? Usikize kitu gani nazungumza.



**Com. Hassan:** Endelea kuongea Sheikh Ali.

**Twahir Sheikh:** Kwa haya mambo ya Majimbo, tunataka maendeleo kama ambayo iko. Mambo ya kitambulisho or citizenship, ambayo tunapata shida, yote yamesababishwa na wafanyi kazi wa Serikali. Yamesababishwa na wafanyi kazi wa Serikali vipi? Kila mmoja, kila mmoja ana lugha yake, kila mmoja anajulikana anatoka wapi, - North Eastern, lugha ya watu wanazungumza ni lugha ya Kisomali. Na inajulikana North Eastern, -lugha wanayozungumza wanaotoka North Eastern, iko different na lugha ambayo wanazungumza Wasomali kutoka nje. Hapa Lamu, kiswahili ambacho kina-zungumzwa na watu wa Lamu, Kiswahili kinacho-zungumzwa na watu wa bara, kiko different. Waborana wana lugha yao, Wamaasai wana lugha yao, kila mmoja ana lugha yao. Wakati watu wanakuja kutafuta vitambulisho, unajulikana wewe umetoka wapi. Hakuna haja, mtu ametoka nje? hata lugha hajui, apewa kitambulisho, halafu anakuja kuchafua jina la Waislamu na heshima ya Waislamu, kusema hawa wamepewa, wanatoka Yemen, wanatoka wapi, anatoka wapi, nini wamekuja kufanya. Kwa hivyo siku hizi katika Kenya, hii mambo lazima iangaliwe, kufanywe committee ya wazee, waangalie huyu ana right ya kupewa kitambulisho, ana right kupewa passport, mambo kama hii ni muhimu sana kurekebishwa katika Katiba.

Sisi Waislamu tuna right kama vile Wakenya wengine. Hatuwezi kusema sisi tumedhulumiwa. Ile Katiba ina-protect sisi

(Inaudible) ya kwanza, maanake kusema mtu anaweza kufanya mambo yake ya dini bila kuingiliwa na bila mambo yoyote. Lakini matatizo sasa yameletwa na watu kutoka nje? na wanatumia jina la Kiislamu, na matatizo kama yanatoka, yote ni dini ya Kiislamu. Lakini tunataka mambo kama haya, yarekebishwe. Yajulikane wakati yeye anatolewa kitambulisho, amepewa Mkenyahalisi. Mkenyahalisi. Kwa haya, ni muhimu kwa sisi Wakenya wote, hii Katiba irekebishwe, na kila mmoja apate ile haki yake, apate ile haki yake na tunaweza kuendesha nchi yetu, kushirikiana kila kitu.

Mambo ambayo mheshimiwa Madhubuti amezungumza, it is the right thing. Kusema watu kutoka nje waje?

(Inaudible) na awe member of Parliament. Na kama anakuwa member of Parliament, kesho atakuwa President wa Kenya. Example, mimi nataka kuwaonyesha nyinyi hiyo, makaratasi hizi. Early 1975, William ameomba citizen visa kuja nchi hii. 88-amepewa citizenship, 92-amekuwa member of Parliament. Member of Parliament amekuwa. Ana pesa yake, amekuja kufanya kila njia ya kuhonga, ameweza kupita. Hana kabila yake hata moja katika Lamu district. Hana shangazi, hana mjomba, hana nani, hana nani. Amekuja kunyang'anya haki ya Wabajuni. Bajuni ndio the royal family katika area hiyo. Ni nchi yao, na wamekatwa pekee yao, kusema this is (Inaudible). Not from foreigners. kwa hivyo watu wetu wanyonge, watu maskini, nimeonelea kitu kama hiyo. Kwa ajili it is a very important thing. Mambo kama hiyo, msipitishwe mara ingine.

President wa Zambia, - mmeona mambo ambayo yametokwa. Nasema huwezi kusema President wewe hukuzaliwa hapa, umezaliwa Malawi. Amekuwa 25 years, President. Kwa hivyo mambo kama hii, hatutaki kitokee kitu kama hicho. Hatutaki kitu kama hii kutokea. Tunataka wananchi halisi Wakenya wapate kiti chao, waongoze nchi yao. Sawa, amepewe citizenship, ana haki kuishi, ana haki kufanya biashara, ana haki kufanya kila kitu.



The second thing, - ni very important thing, wakati...

**Com. Hassan:** Bwana Sheikh utajaribu ku- summarize tafadhali.

**Twahir Sheikh:** Okay. Kitu kingine muhimu ni wakati anaandikwa kazi. Wananchi wa Kenya, sisi kama district ya – kila district ya Kenya, lazima tupate yale matunda ambayo Wakenya wengine wanakuwa na share ya cake ile kula. Sisi katika district ya Lamu, ni first time leo tumepata juzi, amechaguliwa ati chairman wa (Inaudible). Na tuna watu vijana, ambao wana haki kuchaguliwa na waende mbele. Pia, nafasi kama hizi, kila district lazima iangaliwe, -kila district ale ile matunda ambayo ni ya uhuru. District moja hawana kitu, na district ingine wanaongezwa, wanaongezwa, wanaongezwa. Lazima iangaliwe. Vile councillor amezungumza, Waboni na kabila dogo, kama hawa pia, Serikali wanaangalia kwa kweli, lakini mambo yaendeleo kutazamwa, tufanye mpango mzuri. Kwa hivyo, tunashukuru, na msichokeni kuendelea na kazi yenu. Maanake mambo mengi sana watu wanalaumu nyinyi, kusema nyinyi hamfanyi kazi sawa, lakini mimi binafsi naunga mkono Commissioners, ya kufanya hii Katiba ya Kenya. Maanake ni kazi kubwa sana, si kazi ndogo. Wewe kuenda kila mahali kuuliza huyu, huyu, huyu, huyu, si kitu kidogo. Halafu ulete pamoja yote ripoti hiyo, ni kitu kidogo? Si kitu kidogo. Kisha kina- rule for five years, -after five years. kwa hivyo mimi namemaliza yangu, ambayo nimezungumza haya machache, na ahsanteni kuweza kupata nafasi kuzungumza.

**Com. Hassan:** Thank you very much Bwana Sheikh Ali.

(Clapping).

**Com. Hassan:** Bwana Sheikh, tafadhali ukimaliza kutoa maoni tupigie sahihi register, ndio tupate majina yako. Kama kuna wale ambao hawasikii, - najua hao hawa hawatansikia sasa, lakini kama nyinyi mnajua kuna mmoja wenu ambaye hasikii hapo karibu yako, karibu na wewe, mwambie aje mbele hapa tafadhali, ndio waweze kumuona huyu (Inaudible) wetu. Kama ako nyuma kabisa hawezi kumuona vizuri. Kama kuna mtu ambaye hasikii na mnamjua, amekaa karibu na wewe, waambie wakuje hapa mbele tafadhali. Wa sita ni Rukia Lari Shee. Yuko?

**Rukia L. Shee:** Salaam aleykum. Jina langu naitwa Rukia Lari Shee. Maoni yangu yalikuwa ni, hasa nataka hii Commission ichukulie uzito zaidi. Kwa sababu sisi kama raia wa nchi hii ya Kenya, wananchi wa Kenya tumekuwa na shida sana. Na shida yetu imeletwa na mambo ya Wakfu Commissioner. Kwa sababu kuna hizi ardhi ambazo ni za Wakfu. Na hizi Wakfu ni za miaka mingi sana. karibu miaka alfu sasa. Na wazazi wetu, mababu na mababu, na mababu, mpaka wamekuja na mababa, mpaka wamekuja na wamama, mpaka tumekuwa na sisi, na watoto wetu, sisi tuko katika hali ya kulipia hizi Wakfu Commissioner. Na hatujui sheria hii itaondoka lini. Sasa, twataka, - kwa sababu mpango huu wa Katiba ambao waendelea, tungeomba, hizi sheria ziwe zitaondoshwa. Tuwe hizi ardhi sisi tutauziwa na watu wa Wakfu Commissioner. Wawe watatuuzia

na sisi tuweze kumiliki ardhi, tuweze kujenga majumba, model za kisasa, kwa sababu kuna watu ambao mpaka sasa, - ambao wanakaa kwenye ardhi za kukodisha tu wao. Na hawana uwezo wa kujenga nyumba. Mtu amekaa nyumba upande mmoja umevunjika kabisa. Upande mmoja ndio anaokaa, upande mmoja umevunjika, na hana ruhusa ya kujenga. Akitaka kujenga kwa blocks aambiwa wewe usijenge kwa blocks, kwa sababu ardhi si yako. Kwa hivyo twaomba, hii Tume ambayo imekuja, ituangalie sisi raia wa nchi hii ya Kenya. Kwa sababu pesa hizi ambazo sisi hulipa tungekuwa tumejenga majumba karibu mia. Pengine mtu mmoja angekuwa na haya majumba. Lakini tumekuwa hulipa madeni ambayo ni ya kulipia ardhi kama hizi.

Maoni yangu ya pili, tulipokuwa tukifundishwa mambo ya civic education, tumepata maswala mengi kutoka kwa kina mama mashambani. Kina mama wamekaa kwenye mashamba, wakilima mashamba karibu miaka kumi, miaka ishirini, wengine wazazi wao wamekufa, na mara utaona hiyo ardhi amekuja mtu ameitwaa, amesema ati ile ni yake. Na ilhali ile, - kuna mtu pengine mzazi wake amelima hilo shamba karibu miaka ishirini. Sasa imekuwa ardhi si yako tena wewe. Ulichopanda si chako, ondoka uende zako. Kina mama hawa wamekuwa wakituuliza maswali kama haya: je? ni lini? Na ni wakati gani ambapo sisi tutamiliki hizi ardhi? Kwa sababu tumekuwa hatuwezi kumiliki ardhi, hatuwezi kupata mikoko, hatuwezi kuendesha mashamba kununua mambo ya modern kutenda na mashamba yetu, hatuwezi kununua mifugo kuweka ndani ya mashamba, kwa sababu utaweka mifugo ndani ya shamba, halafu atakuja mtu akuambie ondoka kwenye hii shamba, hii ploti si yako. Na ambapo wewe ploti ile umeipatia shida miaka na miaka na miaka. Kwa hivyo twaomba hii Tume, itufanyie mashauri sisi, -na sisi kwa sababu ni wananchi wa Kenya, na ni raia wa Kenya, tuna haki ya kumiliki hizi ardhi. Tuwe tutaweza kumiliki hizi ardhi. Ahsanteni.

**(Clapping).**

**Com. Hassan:** Ahsante sana dada Rukia, kwa sasa ni Ali Abubakar. Ali Abubakar naona uko na written submission, tafadhali jaribu ku- summarize and highlight the main points. (Inaudible).

**Ali Abubakar:** Asalaam Aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Mimi kwa jina naitwa Ali Abubakar. Ninatoka kijiji kingine hapa Lamu kinaitwa Chundwa. Katika Katiba yetu, kwanza kitu ambacho napenda kusema ni kwamba, twataka Katiba iandikwe kwa lugha ambayo inafahamika na wananchi wote wa Kenya. Kwa mfano ikiandikwa Kiingereza, iandikwe Kiingereza ambacho mtu wa kawaida aweza kusoma na yeye. Na pia lugha ya Kiswahili. Na ikiwa kuna uwezo, iandikwe kwa lugha nyingine ambayo Wakenya wengi waweza kusoma.

Jambo la pili ni habari ya uraia. Uraia, ikiwa Kenya ishakubali kumkubalia mtu kuwa ni raia, ni sawa mwananchi yule, aheshimiwe na afanyiwe kila lile ambalo ni sawa kama mtu mwingine.

**(Clapping).**

Hatuwezi leo, tukampa mtu uraia, tukamwambia chukua uraia. Akitaka kufanya jingine, tukamwambia mpaka wako wewe ni

hapa. Kwa hivyo ni lazima tuheshimu yale ambayo tutaya- weka katika Katiba yetu.

Upande wa identity card na ma- passport, nafikiri yamezungumzwa kwa kirefu. Kitu ambacho mimi nataka iandikwe katika Katiba ni kwamba, si hatia ikiwa mwananchi wa Kenya anatembea barabarani, ikiwa hakubeba identity card, akamatwe na polisi awekwe ndani, apelekwe mahakamani, halafu apigwe fine. Kuto-kuchukua kitambulisho, isiwe kama ni hatia. Ikiwa ni lazima unatafikana kutoa ushahidi wewe ni nani, uitwe uende ukathibitisha kama wewe ni raia. Kwa hivyo, hilo ni jambo moja la kusumbua watu na si vizuri, Katiba muweke wazi wazi kwamba jambo hilo hatulipendi.

Jambo lingine, wakati wa kupigania uhuru, tulipigania mambo matatu. Elimu, kuondoa kutokujua kusoma na afya. Leo katika Kenya, imekuwa ni shida kubwa sana mambo haya kuweza sisi kuyakamilisha. Hali ya afya imezorota kabisa. Katika district hospital, utakwenda watu wanashindwa kuenda hospital, kuenda kupata matibabu, sasa itabidi watu wanaanza tena kurudi kutafuta miti shamba. Dawa ziko ghali, na matibabu yako juu, hatuwezi kuweza kupata matibabu kama hayo.

**(Clapping).**

Tumeambiwa habari ya elimu, -tuondoe ujinga, kutokujua kusoma. Leo hapa Lamu, kila mzazi aliye na mtoto wake, aliyeko primary, secondary, mpaka University, sote twaomba fees, twataka msaada. Kwa hivyo, ni lazima tupewe elimu kwa watu wote. Wake kwa waume. Na iwe elimu itakayo simamiwa na Serikali. Mashule yaliyoko mijini na mashambani, yaweze kujengewa kisawa sawa, wapelekwe waalimu wenye ujuzi sawa sawa, skuli ziwekwe vifaa sawa sawa. Mwanafunzi anayesoma Nairobi, na anayesoma Chundwa, wakipewa mihani, wanapewa mmoja. Kwa hivyo tunataka vifaa vile vipelekwe kule, na watu waweze kutumia vifaa hivyo kama kawaida.

**(Clapping).**

Kitu kingine, nimezungumza kwamba kuna hizi harassment ambazo tunapata kwa watu wanaotunga sheria, au wanaosimamia sheria. Isiwe ni haramu au si sawa, ikiwa watu wamekaa mahali, hawana fujo, hawana matatizo yoyote, kuja kuondoshwa na kufurushwa, na halafu kutokee matatizo waweze kupigwa au wengine washikwe. Ikiwa tumekaa, hakuna madhambi yoyote ambayo tumefanya, -kuendea Serikali kichini chini, au kutaka kuharibu-, isiwe ni hatia, polisi kupewa nafasi hiyo, kuja kuwafurusha watu. Polisi wakifurusha watu, mara nyingi ndio inatokwa ni matatizo. Kwa hivyo tulitaka uhuru, sasa tupewe uhuru tujisikie tuna uhuru, tukae chini tufanye yale ambayo tunapenda kufanya.

Kitu kingine, mambo ya recruitment. Tunataka, ikiwa kuna kazi twataka kuandikwa. Twataka 80% ya hizi kazi, tuandikiwe watu wetu hapa. Leo tuna wasichana wamesoma, wavulana wamesoma, wote wanaranda randa hawana makazi. Ikiwa ni Lamu district, nataka nikiingia ofisi, nikiongea, niongee na watu kwa lugha tunayo fahamikiana wote. Kuanzia office messenger, mpaka vyeo vya juu kabisa. Na si sawa, hata kazi ya office messenger, ati mtu atolewe Nairobi, anakuja kuwa office messenger,

fisheries department, yuatoka Nairobi. Kwa nini iwe hivi? Hawa watu tunawapeleka skuli kufanya nini? Watu sasa huku wanapiga kelele, mtoto anasoma anamaliza form four, hana pesa za kuenda training, hana pesa za kufanya lolote. Mwisho atabakia barabarani, atakula unga, atakula miraa, halafu hatujawapatia alternative. Sisi twasema miraa leo tutaipinga, lakini tuwapatie watu alternative. Sisi huku tuna natural resources nyingi sana. Tuna mikoko ndio mashamba yetu, tunaambiwa tusikate mikoko. Sasa tusipokata mikoko tufanye nini? Tuna samaki sisi ni wavuvi. Kunawekwa park, unaambiwa samaki huyu bado usiende kumshika. Uende wapi? Sasa utashika nini? Kwa hivyo hizo game reserve na nini, kuambiwa watalii watakuja kuangalia. Watalii gani watakuja Lamu kuangalia samaki? Kwa nini mvuvi akienda kuvua samaki kule awekewe restriction? Tunaweka hizo game reserves na parks, kunawekwa wanyama wa porini, wanyama hawalindwi vizuri, wanaharibu mashamba yetu. Wewe umesumbuka na familia yako unalima shamba, asubuhi ukiamka ndovu miembe yote wameing'oa. Utakwenda kushitakia wapi? Ukienda kwa game, wasema tutakuja, au hiyo si kazi yetu. Hakuna compensation, hakuna vitu kama hivyo. Sisi twataka tulindwe kisawa sawa. Mashamba yetu yalindwe, ikiwa tusiuwe wanyama, tulindwe sisi na mali yetu. Lakini mali yakianza kuharibika, hiyo itatuletea shida. Kitu kingine ni mambo ya ardhi. Mimi naona ni makosa makubwa sana kwa Serikali kuwa, mpaka leo, sisi watu wa eneo hili hatujaweza kufaulu kupata hati za kumiliki ardhi. Na pia matatizo mengi tumeletewa na viongozi, ambao kila mara wanachukua uongozi wa kisiasa. Mtu akishakupatiwa uongozi wa kisiasa, tushampa license ya kuenda kunyakua ardhi.

**(Clapping).**

Wanakwenda wanazungumza na ma-officer, ardhi zinanyakuliwa. Mimi kwetu nakaa Chundwa. Kwa shamba letu na kila kitu chetu. Mara barua inakuja mnaambiwa ardhi hii aliuziwa mtu fulani kule. Huyu mtu hata hajafika huku. Mambo kama haya yakome, na iandikwe katika hii recommendation kwamba, watu pale wanapoishi, wapewe wenyewe ardhi. Ikiwa Serikali yataka kumpa mtu ardhi, itafute ardhi ambayo hakuna mtu anaishi pale. Na kitu kingine, hii habari ya ardhi kuuza. Ningependa kutoa recommendation. Ardhi iwe ni haki ya kila mmoja wetu apatiwe ardhi. Na ikiwa mtu ana nyingi ya kuuza, iwekwe sheria ni lazima sehemu fulani ya ardhi ile isiuzwe. Ibakie kwa ile family. Leo waiona ardhi huitaji, kuna watoto kumi amewawacha. Ikiwa ni acre moja, wataifanyia nini wakati huo? Kwa hivyo iwe ni controlled. Na pia twataka ardhi yenyewe iondolewe kwa Commissioner wa land. Au President kuwachiwa mamlaka kumpa ardhi yule atakaye. Ardhi iregeshwe kwa wenyewe wananchi. Wazee wa mji ule, au wa mahali pale, wanajua ardhi hii ni yao. Hii watumia kwa ufupi, hii watumia kwa kilimo, ikiwa mmoja wao anataka ardhi kutumia, apewe aitumie ile ardhi. Akimaliza mahitaji yake kutumia, irudishwe kwa wananchi vile vile na wengine waitumie. Bila ya hivyo, itakuwa siku zote ni shida.

**(Clapping).**

Kitu kingine, kuharakisha, nafikiri ni upande wa Local Authority. Upande wa local authorities, ingekuwa ni jambo la manufaa sana, - hizi council zetu nyingi zime-fail, kwa sababu kwanza hazina pesa. Na watu wanaochaguliwa kuzi-run, ni watu ambao hawakupata elimu ya kutosha. Ingekuwa vizuri, tungeregeshewa kama vile zamani kabla ya uhuru. Wale watu wa ule mji

wachaguliwe wataalam. Twataka daktari, anakuwa ni councillor, twataka engineer, twataka nani. Wanakaa pale, wamalize mambo yanayotakikana, waweze kuhudumia wananchi wao. Kwa hayo, itaweza kupunguza gharama, yule mtu ameandikwa kazi ana mshahara wake, na atatoa huduma kama hizo mikutano ya P.C, na mikutano mEngine ambaYo mnafanya. Vile vile tungependa, ikiwa watachaguliwa ma-councillors, tungetaka chairmen, mayor, deputy mayor, iwe ni direct election. Wachaguliwe na raia wote.

**(Clapping).**

Ikiwa ni (Inaudible) kutafuta kura, achaguliwe na eneo lote lile atakalo wakilisha. Kama Mbunge akichaguliwa sehemu fulani, anachaguliwa na area ile yote. Akipata kura nyingi, awe ni chairman, au ni mayor au deputy mayor, na hayo mengine, ni lazima yaweze kufikia hapo.

Na upande wa dini. Kenya haiongozwi na dini moja. Watanguliaji wa kusema walisema, kuna dini nyingi. Lakini yasikitisha sana, -utakuta, - utafikiri dini fulani katika Kenya ndio inaongoza nchi. Wakati wa kutoa vipindi katika TV na ma-radio, utakuta sehemu nyingine wanapewa nafasi kubwa kama ile station ni yao. Nyinyi wengine, - dini nyingine pengine muna mambo yenu ya sherehe zenu, vile vile kubwa, pengine mwapewa dakika tano, au pengine hamupewi kamwe. Kwa hivyo twataka, ikiwa ile ni mali ya umma, itumikie umma wote.

**(Clapping).**

Ikiwa ni Wabaniani wataka kuonyesha sherehe zake za ng'ombe, aonyeshe. Ikiwa ni Waislamu, waonyeshe. Sio wengine wapewe nafasi kubwa kuliko wengine.

Na kitu cha mwisho, ningependa kusema kwamba haya yote ambayo nimesema, nafikiri nimeandika hapa, na kama nimesahau lingine mutasoma. Ahsante sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana bwana...

**Interjection. (Clapping).**

**Com. Hassan:** Ngoja kidogo bwana... ngoja nikuulize swali.

**Com. Mosonik:** Wasema kazi inayopatiliwa watu, kazi iwe 80% ya watu wa eneo hili? Na ukasema ardhi ni muhimu? Lakini eneo hii ni gani? Inafika Mombasa, ama ni Lamu, Malindi? Eneo hii ni wapi?

**Ali Abubakar:** Mimi eneo hili, -na tafsiri yangu ni kwamba, kama kazi ziko Lamu, kwanza waandikwe watu wa Lamu, katika eneo hili. Ikiwa ni Malindi, watu wa Malindi nao wapewe nafasi. Ikiwa ni watu wa Mombasa, wapewe nafasi wao. Kwa sababu kuna mambo ya recruitment, - tunasikia tunaandika army officers, - wale wanaokuja kusimamia watu wanakuja na watu wao tayari kutoka district nyingine, watu wanakuja hapa, unasikia Lamu imechaguliwa. Ukiangalia aliyechaguliwa si mtu wa kutoka Lamu. Kwa hivyo tunataka watu indigenous,...wa kutoka pale.

**(Clapping).**

Na pia, napenda kutia nguvu, kama walivyosema wengine, kama mheshimiwa Madhubuti, kwamba mimi pia nataka Serikali ya majimbo. Kila mmoja apewe jimbo lake, namna tutakavyo peleka katika Katiba, ikiwekwa tutapeleka.

**(Clapping).**

**Com. Hassan:** Tafadhali piga sahihi kwa register, kama huja....

**Ali Abubakar:** Nishapiga.

**Com. Hassan:** Ushapiga? ... (Inaudible) Bwana Omar Famau. Naona pia wewe uko na written submissions. Kwa hivyo jaribu tafadhali ku-summarize.

**Omar Famau:** Asalaam Aleykum?

**People:** Aleykum Asalaam. .... (End of tape one).

**Omar Famau:** Kuna haja ya Katiba hii mpya iwe itakuwa na preamble. Na preamble—

**Interjection:** (Inaudible).

**Audience:** Preamble ni nini? (Noise in the background).

**Com. Hassan:** Tafadhali tunyamaze kidogo, tumpatie Bwana Omar Famau muda wa kuongea pia.

**Omar Famau:** Kwa hivyo, tumesema kwamba kuna haja ya Katiba hii mpya iwe na preamble. Yaani, iwe na chapa na vile tu ikianza, iwe yaanza, - yazungumzia maswala gani. Kwa mfano, katika shirika letu na wale ambao tumeshirikiana kufanya shughuli hizi, tumesema kwamba ianze na kusema,: ‘Uhuru, Demokrasia na Matakwa ya watu wa Jamhuri ya Kenya, ni lazima

yaelezewe kwa uwazi na kulindwa katika Katiba'. Yaani ile, - Katiba ikianza, kwanza ianze na muongozo huo. Kama vile Katiba za nchi zingine, tungewaomba nyinyi ma- Commissioners muangalie Katiba kama ya America, ya Nigeria, ya Ujerumani na kadhalika. Halafu, pia Katiba ya mara hii Inshallah, iwe na supremacy of the Constitution. Iwe ni Katiba ambayo kwamba iko juu, na zile zingine zote zitakuwa ziko chini. Taarab, ikiwa kutakuwa na Katiba ingine ndogo au act, itaenda kinyume ya hiyo Katiba, iwe itakuwa ni null and void.

Halafu, pia tungeonelea kwamba kama kutakuwa kuna uwezekano, ile ile Katiba ya pale awali, ambayo ndio hii ya miaka ya 1963, lau nchi hii ingekuwa imefuata Katiba hii, basi haya matatizo mengi ambayo yametukumba yasingekuwako. Kwa hivyo, ninge-recommend, ningependekeza bwana Commissioners, moja kwa moja muende muipate hiyo Katiba, - maana hapo awali mulituambia mutatupatia, lakini kwa bahati ya kazi nyingi hamjawahi-, muipate hiyo Katiba, na muingalie na muchukue hasa nyingi, mambo hayo. Na pengine mambo fulani ya uwezo wa Rais mpunguze. Maana Katiba hiyo, pia uwezo wa Rais uko mwingi zaidi. Mpunguze hizo, na baadhi ya yanayofuatia ni mazuri tena sana. Katiba hii hii, inazungumzia maswala ya liwali, - hasa sisi watu wa mkoa wa Pwani. Na kuna hii argument ambayo kwamba ilifanywa na Jomo Kenyatta, na Shamte, tungeonelea na tungependa hii pia iwe adapted kwa hii Katiba mpya. Na chochote kile ambayo kwamba hakikufanywa. Kwa sababu huu mkataba ulikuwako na ulifanywa na Rais, ambaye kwamba ndiye alikuwa na mamlaka, chochote kile hakikufanyika, basi mumewajibika, Serikali, wana-Commissioners, kwamba yale yote yaliyotendeka yalitendeka kimakosa, na hayo mambo yarekebishwe kwa namna vile itakavyo wezekana. Kwa hivyo, sisi tunatilia mkazo na tunasema hii Katiba ya majimbo, ndio Katiba ya kuweza kutufaa sisi, maana ile iliyobadilishwa kwa wale wenye uwezo wakati ule, imetumaliza sana. Katiba hii pia twasema, iwe itamruhusu mwananchi yeyote aweze kukaa jimbo lolote. Ikiwa tuko jimbo la Pwani, nataka kuenda kuishi jimbo la Central, niende nikaishi jimbo la Central. Tukienda kule, kuna zile muongozo kadha, itakuwa mimi nitafuata ule muongozo wa pale. Kama hamna, -ya vile nchi ya America namna inavyoenda kwa hivi sasa.

Halafu, lingine ambayo kwamba pia tumesisitiza, ni kwamba ile Serikali kuu iwe itaangalia tu mambo ya defense, iangalie mambo ya international affairs, lakini mambo ya elimu, mambo ya hospitali, mambo ya wakulima na kadhalika, -na mambo hayo yako hapa yote-, iwe itawachiwa on regional basis. Sasa masilahi ya kazi, maswala ya ardhi, hizo zote zitakuwa zimeingia kwenye mikono ya wale watu wa sehemu zile. Kwa hivyo pia, kuna haja sana, Tume hii muutilie maanani na muipendekeze.

Halafu, pia tunasema kwamba hayo makabila madogo madogo, - kama wale wenzangu wengine waliotangulia-, yatiliwe maanani, na hata kama majority wins, lakini kuna haki ya wachache. Kwa hivyo hayo yote ni mambo, - kuna haja sana Katiba hii mpya iwe itafanya. Na baada tu ya hii Katiba mpya iwe itakuwa iko tayari, na kuwe na implementation, yaani matekelezo. Hata ile Katiba ya kwanza, lau ingekuwa yatekelezwa, - ile jamaa waliibadilisha. Walibadilisha hiyo wakaja kwa hii. Lau ingetekelezwa hata hii, pia mambo yasingekuwako mabaya hivyo. Kwa mfano, katika Katiba hii yasema, tuna haki ya kuweza kusoma mashule ya inter prefix. Yaani mimi, kwa mfano nilisoma Tarasaa hapa, sikuweza kulazimishwa kule niwe nitafanya Christianity. Lakini nililazimishwa. Hata hivi leo, kuna watoto kadha wa kadha, -hata juzi nilikuwa naye, nikamuuliza wewe wasoma somo gani na gani? Asema mimi nasoma kadha kadha, kadha, akanaiambia na C.R.E. Nikamwambia, pia

walazimishwa? Ndio. Akasema, mpaka form three. Kwa hivyo, - tayari Katiba hii imekupa haki ya kwamba wewe ukasome shule yoyote, lakini usilazimishwe kusoma Hinduism, au Islamic, au Christianity. Kwa nini mwamlazimisha? Sasa imekuwa ile board of governors ni supreme, above this Constitution . Ndio ile tumeanza na kusema kwamba

**(Clapping).**

Ndio tumeanza na kusema kwamba, hii sheria hii, iwe ndio supreme. Yaani iwe ndio mwongozo. Na haki zetu zilindwe na wasitunyime kamwe, zetu zilindwe na za wale wengine pia zilindwe.

Halafu, tunaenda kwa pahala pa ardhi. Wenzangu wengine wote wamezungumzia maswala ya ardhi, sisi nasi tumependekeza, ardhi iendelee kuwa community land. Ardhi hizi zimekuwa ni zetu, hasa sisi watu wa sehemu hii. Hasa sisi Wabajuni, hizi ardhi zimekuwa ni zetu. Mukienda katika historia vyema, mutakuja kuona kwamba hii si G.L. kamwe. Ni ule uwezo tu na nguvu na mambo kadhalika. Basi, ikiwa kumetendeka dhuluma kama hizo, wale wote walionyakua hizo ardhi, waziregeshe, zirudi kwa watu wa hii sehemu. Na ikiwa wewe una haja ya kuitumia hiyo ardhi, nenda uitumie. Lakini usichukue ardhi, na unaonea tu masikini kwa sababu wao hawana uwezo au hawana pesa. Kwa hivyo ardhi, - hasa sisi watu wa sehemu ya Lamu District-, ardhi zetu zile zote zilizochukuliwa, kuambatana na ule mkataba ambao nimewapatia, zaweza kurudi. Maana ule mkataba *uli-signiwa* na Shamte, pamoja na Jomo Kenyatta, hao wote ni watu wa kisawa sawa. Na sisi sote tunakubali.

**(Clapping).**

Halafu, sehemu nyingine ambayo pia tumesisitiza sana, ni kwamba Wabunge wetu, na ma-councillors, na ma- chairmen wetu, tunapowachagua, pia tuwe tuna uwezo wa kuwa –impeach. Yaani pindi wanapokuwa hawafanyi tena zile kazi zao, ambao kwamba ndio tumewapatia, tuwaambie sasa, hatuwataki tena na tuwa- call back, na tuchague wengine.

**Interjection. (Clapping)**

Na hiyo pia inaenda moja kwa moja kwa yule Rais ambaye tutamchagua, pamoja na makamu wake. Mwongozo wetu tumependelea Rais awe yeye atachaguliwa yeye pamoja na makamu wake. Ndio yeye akiwa ame-resign, mwenzake atashikilia ule usukani, na kuwe hakutakuwa na matatizo. Maanake kile kipindi ndilo kitapita mpaka ule wakati wa election iwe itakuja. Halafu pia tumependekeza katika mwongozo wetu, tumependekeza lile Bunge, liwe lita- dissolve wakati kadha. Ikiwa, - sisi tushaona kwamba kila December, huwa kuna kura Kenya. Basi ikifika October, November, dissolve Parliament. iwe ule Rais atakayekuja mwingine, awe, - haitakuwa ni weapon yake ile ya siri. Ile ni siri yetu sote, maanake sisi ndio tumeweka uongozi huu, na nchi hii ni yetu kama raia. Kwa hivyo tungependekeza...

**Interjection.**

*(not clear).*



Kwa sababu haya yote tumeandika na hasa ni ya ma-Commissioners. Pia tumependelea maswala ya Kadhi, Kadhi awe atachaguliwa na panel of Muslim leaders. Wale viongozi wa Kiislamu, wanakaa wanasema huyu ndiye anayefaa kuwa Kadhi, na hatimaye Kadhi yule yule awe empowered, na hasa inapokuja mambo ya social activities. Kama vile hapo awali tumeambiwa mababa wanatupa watoto wao, basi yule Kadhi awe empowered. Inapopelekwa kesi ya Omari Famau, ametupa watoto, Kadhi aniite mara moja, aniambie wewe kwa sababu ya hiyo na hiyo na hiyo, tutachukua ile shamba fulani ulioichukua pahala fulani, iende kwa watoto.

### **Interjection. (Clapping).**

**Omar Famau:** Iende kwa watoto. Yaani wawe empowered. Halafu pia, tungependelea katika mwongozo huu wa Katiba mpya, - kuna hizi professional bodies, mashirika kama 'Kenya Tourism Body,' mashirika kama ya kina mama, mashirika kama federal zile za mipira, hayo mashirika hayo yote. Yawe mwongozo wake wa kuchaguliwa ni ya grassroots. Wale wana-sports, wale wana-soccer, wawe ndio wenye kufanya ule uamuzi. Ndio wenye kuchagua. Isiachiwe provincial administration. Au isiwachiwe wale watu ambao kwamba watataka kuitumia hiyo opportunity, bila ya muongozo. Nitamaliza na kusema kwamba, mashirika kama civil society, kama vile C.B.Os, N.G.Os, mashirika ya kina mama, religious leaders, -za Kiislamu, za Christianity, Hinduisim, hizo ziweze kuwa na uwezo zaidi katika Katiba hii mpya, waweze kuwa ni watchdogs. Waangalie the Executive, waangalie politicians, waangalie kina

(Inaudible), so that kuwe na checks and balance. That is the whole idea. Yaani kuwe kutakuwa na ile mizani ya kisawa sawa. Pamoja na media, - gazeti. Pamoja na gazeti, zinaenda sambamba.

Kwa hayo machache, nimeshukuru sana Mungu kuniwezesha, kuweza kuleta presentation yangu. Ahsanteni.

**Com. Hassan:** Thank you very much Bwana Omar. Naona tunafikia wakati wa aduhuri, na najua kuna wenzetu ambao wangetaka kuenda kuomba. Wale ambao mnataka kuenda kuomba munaweza kuenda. Lakini sisi tunakaa bado, twataka kuwasikiza wale ambao wanataka kutoa maoni bado. Kwa hivyo, Zahara Shee, muungano women group.

**Zahara Shee:** Asalaam Aleykum. Mimi jina langu naitwa Zahara Shee Mohammed,

### **Interjection.**

**Com. Hassan:** Tafadhalini kama munaondoka muondoke pole pole bila kutoa kelele, tumsikize madam pale.

**Zara Shee:** Jina langu naitwa Zahara Shee Mohamed, na wakati tukifanya hizi civic education, kama C.D.O. moja ambayo nilijishirikisha, kulikuja mambo muhimu ambayo yalikuja tukasema, motherland, ambayo ni Coastal strip yetu. Na katika hii

Coastal strip yetu, kulikujia mambo ya settlement schemes. Kumekuwa, - tumeletewa watu wakawa ni settlers, ambao ni non-indigenous, wa huku kwetu.

La pili tukawa tunajiuliza, sisi wa-Coast, haswa sisi watu wa Lamu district, future plans za Serikali hii ya Kenya, kwa hizi settlement schemes ambazo tayari wamezipeana, wametufanyia nini? Ikaja recommendation ya kuwa, kuanzia sasa, kusiwe na settlement scheme yoyote itazuka. Kwa sababu hatukumbuki sisi, watu wa Coast kupelekwa mahali kuwa settlers, na hatimaye tukapewa vitambulisho kwa kuwa pale pahali ni petu.

Ya pili ikaja ni title deeds. Na title deed yenyewe tukasema hivi, wengi katika watu wetu, wamekosa kumiliki ardhi, kwa sababu ya kutojua kufuata mipango ya haki za ardhi. Pili tukasema, watu wamekosa kumiliki ardhi kwa sababu ardhi zetu zimewekwa ni G.L, ilhali twazijua ni ardhi za kiasilia, na ardhi za mababu zetu. Na wakati huo, wakati zikiwa ardhi ni namna hiyo, watu wetu wamekosa haki yao hapo, na katika kukosa haki yao, pia, yale maendeleo wangeweza kufanya katika ardhi hizo, pia wameweza kuzikosa. Hiyo, imeweza kuwafanya watu hao wawe squatters. Na ilhali hawana haki ya kuwa ni squatters. Nyingine pia, watu kama hao, wameweza kukosa haki za kumiliki ardhi, kwa sababu ya kuwa, kati ya watu hao ambao wameishi pamoja, - kwa mfano, mimi naweza kuwa nimerithi ile ardhi kwa babu yangu. Lakini sina ile title deed. Kuna mwingine, yeye ana ufahamu kamili, namna ya kupata. Akapanda juu, akaja, akanitoa mimi katika ile ardhi, huku mimi nina mmea navuna. Na nimekosa. Kwa hivyo kitendo kama hicho, yule ambaye anapigania hiyo haki, huikosa, kwa sababu yeye hana haki ile ya yule ambaye ameweza kuipata. Sasa, tukaja katika recommendation zetu. Tukasema, watu waelezwe kikamilifu, na wasomeshwe kikamilifu na Serikali, namna ya kuweza kupata haki ya ardhi. Pili, tukasema, title deeds ama letter of allotment, zisipeanwe kwa watu kama hao, mpaka, watu hao wateremke chini, -yule ambaye amemiliki pale pahali, aitwe, aulizwe je? hapa pahali wewe pamoja na community, ambayo ita-identify kwa kuwa huyu ni yake. Maanake wanakuja watu, hawajui hata ile G.L number, iko mahali gani. Sasa anaanza kuja hapa Lamu, anapata, officer wa survey, anapata officer wa settlement, anapata officer anaanza kumuonyesha G.L hii iko upande fulani na iko hali fulani. Kwa hivyo, kabla hilo halijatendeka, watu kama hawa, wahitajika waende grassroots level. Kule, tuna watu wetu a jamii ambao tunajuana. Na wanaweza ku- identify kama hapa mahali hapajaishi mtu kwa miaka kadha. Lakini ikitokwa tu kwa kuwa hapa pahali ni pangu, hata kama hizo procedure zimefanyiwa, hiyo title deed isimame. Kwa sababu itafika wakati, sisi watu wa Coast, hatutoweza kujizua. Na tunahofia, wakati ukifika wa kutoweza kujizua, kutatokwa maathuri. Kwa hivyo hayo ndiyo ambayo tumeyaona, na ni ya muhimu sana.

Kisha, yakaja mengine ambayo mwenzangu tayari alikuwa amezungumza, habari ya Wakfu –Commissioner. Kuwa watu wana ardhi za Wakfu kwa miaka. Lakini hawamiliki ile ardhi. Na Wakfu, Commissioner, tunavyoelewa, ni kama shirika la watu wote. Kwa hivyo likae, -ikiona mimi Zahara, nimemiliki hii ardhi, nikiwalipa, yaani rent, kwa miaka kadhaa, waniamulie, ninunue ile ardhi, niweze kufanya development ambayo itanistahili.

Jambo lingine ambalo tulikuja nalo, lilijitokeza mbali na land, ni mambo ya agriculture. Katika agriculture, ilikuja mambo ya

fishing, ya uvuvi. Na tukasema hivi, Serikali inatuwekwa sheria, au inatuwekwa vikwazo, tuvue na net number ndogo sio number kubwa. Kwa sababu wale

Samaki wana wa-preserve, ile consumption inayotoka, haitoshi kwa jamii yetu. Hatujakataa, vile inavyofanya, itakuwa ni usawa. Kwa sababu wamefikiria future. Lakini, wakati huo huo, pindi wanapo amua mambo kama hayo, au wanapoweka sheria kama hizo, au kikwazo kama hicho, twataka wajiulize kuwa, je? hawa watu, tumewapa elimu ya kutosha? Je? hawa watu, have we empowered them? Je? pana utajiri wa aina gani ili kuweza hili jambo kutekelezwa? Kwa hivyo, wakiwa wamekuja hapo, na pengine, - sisi tunsema hivi, watu wetu waelezwe kwa kutosha, na pia wapewe skills za kutosha, na pia kwa sababau Pwani ni yetu sisi, na huku ni kwetu sisi, tuwe na industries za fishing huku huku kwetu Pwani, ikiwa Serikali itatutafutia, au itakuja ku-settle, ili watu wetu waweze kupata kazi. Kwa sababu vile tunavyoelekwa, baada ya miaka mitatu minne, vijana wetu watakuwa ndio wakora wa mwisho. Kwa sababu hawana la kufanya. Mtoto umemsomesha, kazi hana. Pwani anayo, hawezi kugusa.

**(Clapping).**

Lingine, pia, kuna haya trailers, yanatoka China, yakija kuvua samaki, yana mdomo wao mrefu, ukienda Magogoni au kwa Bargoni, ndio unayaona kwanza. Yakitua yanazoa samaki, mkubwa, mdogo, huku sisi tunanyimwa. Kwa hivyo watu kama hao wa nje? wakatazwe kuja kutuvulia samaki wetu ovyo. Na watuwachie sisi wenyewe, wakiwa wataka samaki, they speak direct with the local people in the community. So that, wale wapate makazi, na wale waanze kufikiria zaidi. Kwa hayo ningesema ahsante.

**(Clapping).**

**Com. Hassan:** Ahsante sana mama Zahara. Imefika sasa saa saba, ni wakati wa lunch, ningetaka tu-break for lunch, turudi saa nane. Kwa hivyo mutatusamehe, tuta- break sasa wakati huu, tuende lunch sasa. Ahsante.

*After Lunch.*

**Com. Hassan:** ... za jioni, na tutaanza na Abdul Samad Basheikh. Naona uko na written submission? Kwa hivyo tafadhali jaribu kuharakisha. Summarize.

**Abdul Samad Basheikh:** Asalaam Aleykum Warakhmatulahi Wabarakatu. Mimi nime-summarize recommendation zangu to the Commissioners, kwa kufuatilia mpangilio huu. La kwanza, nina maswala kuhusi ardhi. Katika maswala ya ardhi, mimi ningependelea -recommendation yangu ni kuwa, ardhi yetu ya Lamu ibadilishwe kutoka kwa G.L- 'Government Land,' ifanywe community reserve land. Kisha, pia nasema kuwa allocation zote, za ardhi ya ukulima, iwe itakuwa ni to the citizens wa eneo hili. Isiwe kuwa mtu ameweza kutoka nje? akaja akachukua ardhi yetu. Kisha, kama ardhi imekuwa allocated kwa major project development, tuseme kama hao wanaochukua ardhi wakisema kwamba watatengeza viwanda vya chumvi, wengine

wanataka kutengeza mashamba ya miwa, wengine wanataka kutengeza mashamba ya nini, project kama hizi, ziwe ile ardhi haitokuwa transferable by sale. Sio kuwa mtu achukue ardhi acre elfu mbili mia tano, au hectares elfu mbili mia tano, kisha kesho ardhi ile watu wakisha-kusahau, aweze kumuuzia mtu mwingine na hiyo project ya chumvi, sijui project ya nini, zote ziwe hazitafanyika. Ardhi iwe ilichukuliwa kwa nia ya kutaka kuuza. Kisha, ardhi ile ambayo ni ya project development, iwe itapewa muda fulani, kama a grace period for development. Miaka mitano au miaka kumi, ikipita miaka kumi, ardhi ile ichukuliwe, iregeshwe mikononi mwa wananchi. Lingine ni kuwa, community land committees, ziwe zitachukua nafasi ya Government au district land committee. Yaani kutengezwe committee ya hapa hapa, watu wetu wa jamii, au kama ni kwingine ifanywe hivyo hivyo, committee ziwe zitakuwa ni raia. Si habari ya wafanyikazi wa Serikali ambao hawana interest na wala hawajui uchungu wa ardhi yetu. Kisha, ardhi yoyote, mahali kokote Kenya, allocation ziwe hazina siri. Ziwe zina limit. Hatuwezi kuchukua ardhi acre elfu nane, tukampatia mtu mmoja acre elfu nane, wakati mimi na wewe hatuwezi kumiliki hata acre moja. Hii italeta ufarakano mbeleni na italeta matatizo mengine.

Upande wa polisi, mimi nime-recommend kuwekwe component ya public relations. Na iwe emphasized by law, isisitizwe kuwa polisi lazima wafanye seminars na workshops, ili kuleta uhusiano bora baina ya polisi na raia. Hizi sheria za kuwa hushikwa ukenda ukatupwa ndani, huulizwi. Yaani sheria kama hizo ziondoke na watu waelewe rights zao, wakati wakiwa mikononi mwa polisi.

Sehemu nyingine nimesema citizen's rights. Watu wengi wamezungumza kuwa twataka sheria za umiliki wa birth certificate, passport, na Identity card, ziwe ni uniform kwa Wakenya wote. Without regard to race, color, or creed. Mengine ni kuwa, basic rights, haki zetu za elimu, afya na education, na mengineo. Lazima zisisitizwe kwenye sheria itakayotungwa mpya. Ikiwa sisi basic rights zetu tunaona zina tashuishi, kuundwe, Supreme Court, ambayo jamii yoyote ya Kenya, - tuseme kama watu wa Faza, matatizo yao ya maji na sisi matatizo ya barabara miaka arobaini, tuwe twaweza kupitia through the Supreme Court. Tuipeleke Serikali kortini, tueleze kwa kuwa sisi Serikali imetudharau, na ni negligence kwa upande wa Serikali, ili tupate malalamiko yetu yasikizwe.

Jambo lingine, kwa wafanyi kazi wa Serikali, na-recommend kuwa retirement letter ikija, ije na cheque ya retirement benefits. Yaani, vile ukiwa wewe sasa waambiwa wastaafu, ile barua inayokuja kukustaafisha, ije pamoja na cheque yako ya malipo ya uzeeni.

Upande wa cultural affairs, nimesema culturally sensitive issues, issues kama mambo ya miraa hapa kwetu. Kwa mwaka mzima sasa, twajaribu kuondosha miraa kwa hii jamii yetu. Sheria za namna hii za kupitia huku na huku, ziondoshwe. Iwe ni kupitia kwa referendum. Wananchi waweze kuulizwa, twataka kuondosha miraa, yes or no? mtu akisema yes, sheria inawekwa. Mtu akisema no, miraa inabaki, watu waendeleo kula miraa. Na haya ni kwa maswala tofauti tofauti, wengine wataka kupashwa tohara wanawake, wengine kuna sheria zingine. You know, hizi ni sensitive issues, ambazo ziko kwenye jamii zote za Kenya.

Lingine ni kuwa Presidential appointments, lazima iwe zaweza *ku-challengiwa* na Bunge. Sisemi zipitie Bunge, nasema zaweza *ku-challengiwa* na Bunge. Kwa ule anataka kuchaguliwa na anaonekana hafai, Bunge liweze kusema huyo hatumtaki. President chagua mwingine.

Lingine ni kuwa, katika kuchagua project directors, lazima sheria ipatie priority, wale local community. Kama ni Lamu, basi first priority ije kwa watu wa Lamu. Kama ni Kisumu, First priority iende kwa watu wa Kisumu. Namna hiyo. Kisha, ningemba kuwa Serikali I-adopt Parliamentary system, ambayo ita-create wadhifa wa Prime Minister. Lingine ni kuwa Regional Government iwe ita- replace Provincial Administration. Provincial Administration ifutwe, ili services ziende karibu na mwananchi. Pia kuchaguliwe Governor, Provincial Governor, ambaye atachaguliwa na wananchi, na yeye ndiye atawakilisha jimbo lote la Pwani.

Lingine ni kuwa Electoral Commissioners wawe na security of tenure, wasiwe kuwa Moi, leo wakiona hawa hawanisaidii mimi, aweza kuwafuta, au akiona wanifaa aweza kuwaweka. Yaani nasema President, - pole nilikuwa nimesema Moi, kwa kuwa ni President wetu-. Wawe na security of tenure.

Lingine ni kuwa Parliamentary campaigns ziwe zitakuwa na ceiling expenditure. Mbunge awe hatoruhusiwa kutumia yale mapesa anayotumia kununua, mpaka mtu wa chini. Iwe itawekwa two million kwa minajili ya logistics pekee yake, kama ni kukopesha boat, kama ni kukodisha gari, kama ni kutia petroli kwenye nini, -kununua punda kuenda Kiungani, au pengine kwote. Isiwe ni kwa sababu ya kununua kura za mwananchi. Ikiwa Mbunge – there is bribing of voters, iwe ni serious election offense.

Lingine ni kuwa, kwa kuwa Wabunge walipwa over 350, 000 thousand, commuter allowance, yaani allowance ya kuja kututembelea sisi hapa Lamu, kila mwezi analipwa karibu zaidi ya laki tatu. Lazima ihakikishwe, kuwa Mbunge atatembelea eneo lake, mara tatu kwa kila mwezi, na akiwa hafanyi hivi, iwe kuna njia sisi tunaweza kufuata, tu-report mambo kama haya na hatua ichukuliwe.

Na mwisho, ni kuwa twataka seats tano ziwekwe Bungeni, yaani viti vitano viwekwe Bungeni kwa minorities katika Kenya, wachache katika Kenya. Kama sisi Wabajuni, kama Boni, Wandorobo, kama Waarabu, -sijui kama Waarabu ni indigenous-, lakini kwa wale ambao ni indigenous. Kisha, seats hizi tano, ziwe zita rotate kwa minorities. Kama mara hii amekwenda Mbajuni Bungeni, nafasi tano haikumfikia Mboni, next session, iwe ataingia Mboni, Mbajuni atabaki nje? na hizi ziiitwe, - they should be referred to as tribal representatives. Wawe wataweza kufikisha maoni ya makabila yao Bungeni.

Na hilo ndio la mwisho. Ahsanteni.

**Com. Hassan:** Shukurani Abdul Samad, kwa hayo maoni yako. Sasa mwaona kuna... -anafuatiwa na S.M. Adhik, katika Lasegu. Lakini naona pia Abdulrahman Nzale alikuwa amesema kutoka Lasegu.

**Adhik:** Yaweza kuwa ni maoni yangu binafsi, si lazima yawe the same.

**Com. Hassan:** Basi niandike hapo 'Individual,' sio yako na yeye? Anza na jina.

**Adhik:** Jina langu ni Swaleh Mohamed Adhik. Salam Aleykum! Mambo mengi yamezungumziwa na wenzangu waliopitia, kama upande wa citizenship, sitaeleza kuliko vile Bwana Ali Abubakar alivyoeleza. Kwa upande wa Land, naunga mkono wenzangu, kwa decentralized allocations. Fadhili ya allocation ya Land kufanywa na District allocation Committee, ambayo inakuwa chaired na D.C, ambaye mara nyingi si mwanai. Twataka ifanywe na village elders, pamoja na religious leaders, pamoja na pengine Mbunge ama councillor. Lakini wazee wa mji wahusishwe zaidi, ndio watajua sehemu hii huyo hakupewa ama apate. Kwa upande wa kugawa ardhi vile vile, kuwe ceiling kama vile mwenzangu Bwana Abdul Samad alivyosema. Asiveze mtu kupewa pengine 10,000 hectares, wakati mmoja wetu hana hata acre tano. Ardhi haikuwi.

La tatu ni repossession of wrongly acquired land. Kuna watu kutoka bara, - poleni wana bara-, lakini wengi wamepata ardhi hapa Pwani. Sisi hakuna mtu ana ardhi Nakuru ama Kericho. Lakini hapa Pwani, especially beach plots zote, zimechukuliwa na watu kutoka bara. Either, Commission of lands, ama Presidential Directives. Ningependa kuisitiza hii habari ya Presidential directives, kwa sababu twaona mambo mengi yakifanywa na yeye, hayo hayauliziki. Kwa hivyo, nobody should be above the law, hakuna kitu kama hicho. Watu wote wako chini ya Katiba na sheria. Uwezo wake Rais pia upunguzwe sana, na kufuatana na majimbo, sisi ni (Inaudible) ambao sote twai-support, mini ni mmoja wao, ni kwamba, powers zile ambazo anazo yeye, nyingi zitaingia katika Governors wetu.

Kwa upande wa mabarabara, tangu independence, miaka thelathini na nane sasa, tumekuwa na Wabunge wa kila rangi. Mpaka kufikia sasa watu wapigania, “ huyu ni Mbunge wa kutoka Lamu, huyu amepata naturalization, ooh, hivi hivi,” lakini wote wamekuwa wakizungumza kitu kimoja cha barabara, Serikali haijafanya, na haina tamaa ya kufanya. Kwa hivyo, twataka kupuitia Katiba hii, iwe maeneo ya barabara, yawe yatafuatwa kufuatana na vile yalivyo. Kwa mfano, barabara ya Thika, barabara ya Nairobi, iko sawa, sasa watu waangalie Lamu, Garissa, waangalie upande mwingine ambao barabara hazijatiwa. Kwa hivyo kuwe na uniformity. Sio mwashughulika na highway ya Mombasa - Nairobi, na ile ya Kericho, Eldoret, huku kwingine Panagu, wapi, hakuna hata footpath.

Vile, vile, maji, afya, na zaidi, zaidi, zaidi, ni security. Upande wa security ndio uko chini sana. Huku sisi watu wa kutoka Lamu, saa yote twapambana na bandits, na wakati mwingine –Somalia haina Serikali kwa sasa-. Kukitoka chochote, ukicheza koi kule kwao, muko ni huku. Yaani wakicheza *kibe*, mahali pa kujificha ni huku. Kisha ndio warudi kwao. Kwa hivyo na hapo, hapo hapo Karegoni kuna Kenya Army, Kiunga border kuna Kenya Navy, kuna General Service Unit wako wengi, kuna Administration Police, wako wengi. Kuna Kenya, - ama Regular Police, wako wengi. Lakini, mpaka sasa Msomali aweza kuingia mpaka hapa, akaenda akapigia D.O 1 pale bila D.C kujua, akaenda zake. Kwa hivyo mutuangalie habari ya security,

iwe katika Katiba. Kwa sababu tukiachia mambo Wabunge, Wabunge wakati mwingine husema, katika hansard mukizifuata, watu wengi huzungumza habari ya security, habari ya barabara, lakini the Government doesn't do anything.

Na la mwisho, ni kusisitiza upande wa Majimbo. Majimbo yenyewe ni mfano wa Nigeria, si mfano mwingine kama nchi nyingine. Twataka ule ule wa Nigeria. Kwa hayo machache, ahsante.

**Com. Hassan:** Ahsante sana bwana Adhik, tafadhali piga sahihi kwa, - kwa wale ambao wameandikisha maoni yao, tunawaomba tafadhali mupige sahihi. Naona kuna wengine wameleta hizo submissions lakini, hawajapiga signature kwa document yao. Ni muhimu sana kwa mtu kupiga sahihi kwa document yake. Tafadhali, wale wameleta hapa, kama muko sasa hapa, murudi na upige sahihi. Na wale ambao mutayaleta wengine, please make sure ume-sign hiyo document. Ahsante. Now, Faisal Miji. (Pause), naona pia kuna ma-groups mengi ambayo hapa wamejiandikisha. Tungefurahi sana kama mungechagua mmoja wenu atoe maoni kwa niaba ya hilo kundi. Kwa sababu, wote mukianza mukitoa maoni, itakuwa ni shida, hatuwezi kusikiza leo yote.

**Faisal:** Asalaam aleykum. Mimi kwa jina ni Faisal, na nimekuja kuwakilisha kikundi chetu ambacho kinaitwa 'Lamu Cultural Promotion Group,' ambao ni vijana kutoka hapa hapa Lamu, na tulikaa tukazungumza, kwa hivyo haya maoni ni maoni ambayo tulichanganya fikira za vijana kadhaa. Kwa hivyo leo ndio nimekuja kuwakilisha chama changu.

**Speaker:** Jina kamili?

**Faisal:** Faisal Mohamed Miji. Mambo mengi ambayo tayari hapa tuliyazungumza, naona tayari wenzangu washasema, lakini kuna moja moja ambayo nataka kuzi... kujaza. Yale ambayo yashasemwa sitarudia kwa sababu ya kuchunga wakati. Jambo la kwanza, nataka tufikirie hii Constitution ni kitu gani. Katika sisi hapa naona, sio watu wengi ambao washaiona kama hii Constitution ya Kenya tulioko nayo sasa hivi. Watu wengi sana hawajui kamwe. Na wale ambao washaiona, wakiisoma, hawawezi kuifahamu. Kwa sababu mimi mwenyewe nishakiona hicho kitabu, na nikajaribu kukisoma, lakini, si jambo ambalo linawezafahamika kwa mtu yeyote. Wacha wale waliosoma, hata waliosoma si rahisi kufahamu, kwa hivyo, tungependekeza, Katiba iandikwe kwa Lugha ya Kiingereza, na Kiswahili ambacho kinaweza fahamika kwa kila mtu. Ndio kila Mkenyaaweze kujua mahali gani amedhulumiwa, na haki yake iko namna gani. Hilo ni wazo letu la kwanza.

La pili tukienda, pia tungependelea watoto wetu sasa wakiinukia, wajue haki zao kutoka wakiwa shule. Ndio watajua majukumu gani wao wanastahili wawe, na Serikali ina jukumu gani, na fulani ana jukumu gani. Kwa hivyo tumependekeza pia Katiba, iwe ni moja katika somo ambayo itasomeshwa katika Primary schools. Kama itaangaliwa iwe ni kutoka standard six, seven, iwe ni one of the subjects which will be taught in schools from primary level. Yaani iwe ni somo katika masomo kama vile Geography, History, kuanzia primary level, kuendelea, iwe ikifundishwa mashule.



Halafu pia tukasisitiza kwamba, kwa sasa hivi raia yuko tu, Serikali ndio ina mchungu. Tungependelea iwe pia raia ana macho na ana haki na uwezo, wa kuweza kuichunga Serikali. Kwa hivyo, tunataka Katiba ambayo itampatia raia power zaidi, kuliko ile ambayo iko sasa hivi.

Sehemu nyingine nimefupisha, tungependelea pia the administration officers, kama vile kuanzia P.C, District Commissioner, mpaka D.O, wa kila province ama kila district, awe ni mtu ambaye ametoka katika area hiyo. Kwa sababu sioni kama ni sawa, nitoke hapa niende nikawe P.C, sehemu kama Kisumu. Kwa sababu Kisumu si kwetu, sitakuwa na hamu ya kutaka kutengeneza huko. Kwa hivyo ukipata mtu ambaye ametoka kwa eneo ile ambayo amesimamia, anaweza kujitolea kutengenezea mambo yake na watu wake, kwa sababu ni kwao. Kuliko sasa hivi, mtu anafanya kazi kwa ajili ya mshahara, lakini si kwa ajili ya kutaka kutengenezea watu.

Halafu, tukaenda katika tatizo moja ambalo, sisi sana Waswahili tuko nalo. Watu wengi hapa washalalamika kuhusu – tunabaguliwa, wakitaka passport, wakitaka birth.... Lakini ukweli ni kwamba, ni lazima tuangalie ni sheria gani ilituuma sisi. Tukisema passport tufanyiwe hivi, itakuwa bado hatujatekeleza. Lakini, vile ambavyo naona mimi sheria lazima, - ile yataka kuandikwa sasa hivi, ni kwamba, watu wote waliokuwa Kenya, kabla Kenya haijapata uhuru, wakuwe ni raia kamili wa Kenya na haki zote wakiwa watu sawa. Sijui kama Tumefahamiana? Yaani all those people, watu ambao walikuwa wako katika nchi hii, katika Kenya kabla tujipatie uhuru, watambulikane kama raia wakiwa na haki sawa, bila kujali rangi, ama dini, ama alikuwa mtu wa kutoka asili gani. Lakini akiwa bahati yake, wakati Kenya ikijipatia uhuru alikuwa tayari yuko hapa, atambulikane kama yeye ni Mkenyana haki zote.

Na kitu kingine ambacho mimi nataka kukieleza kidogo hapa ni kuhusu Waswahili. Mara nyingi tumeambiwa kwamba Waswahili si watu, si kabila, Waswahili ni lugha. Sasa mimi mwenyewe sifahamu kuwa, kwa nini kupatikane lugha, bila kupatikana watu wanayo izungumza? Maana English ni lugha ambayo inazungumzwa ulimwengu mzima, America, Australia, England, India, hata hapa kwetu, lakini kuna wenyewe. Kuna English people. Kwa hivyo kama Kiswahili, inazungumzwa na watu wote Kenya, -Wakikuyu, Wajaluo, Wakamba, haimaanishi kuwa haina wenyewe. Kunao Waswahili ndio hiyo lugha ikatoka. Kwa hivyo lazima tutambulikane kama raia, na tupewe haki sawa sawa.

Halafu, tukaja kwa privileges na opportunities. Yaani ni lazima nafasi zilizoko za asilimali za umma, na nafasi za kazi, - appointment za Serikali, ama wale watu ambao walichaguliwa na President, ama Serikali kusimamia mahali fulani, ni lazima zigawanywe sawa sawa, - kama mtu ashafanya kazi, na manufaa ya kimaisha. Kwa hivyo ni lazima watoe wapewe bila kubaguliwa rangi ama vipi, ama vipi. Sijui kama tumeelewana hapo?

Halafu tuka- propose pia, tungependelea majimbo system of governance ikuwe applied, na tukasema about 75% of the revenue collected in every province should be used to develop the province respectively. Yaani kwa ufupi, tungependelea Serikali ya majimbo, na rasilimali inayopatikana katika hilo jimbo, asilimia sabini na tano iwe itatumiwa kujenga jimbo hilo, halafu asilimia



ishirini na tano, ndio tutatoa kwa Serikali kuu. Kama zimepatikana, Coast province ndio zitatumika 75% katika jimbo hili. Ikiwa ni jimbo la kule, - sio kama sasa, pesa zinapatikana hapa, zinatajirisha mahali pengine na huku watu wanaendelea kuumia.

Halafu, nyingine nitaruka kwa sababu tunachunga wakati, tukasema ni lazima watu wapewe uhuru wa kutoa maoni, kuwa na uhuru wa kusafiri, na uhuru wa kuzungumza. Ijapokuwa itakuwa ni kinyume na Serikali ambayo iko. Yaani hata kama Serikali imefanya jambo, na mtu asimame atoe maoni kupingana na Serikali, na kuweza kufanya campaign ama kutembea, ama kuzungumza, awe na haki na asiwe na uoga wala kutishwa. Kwa hivyo tukaandika in short, freedom of expression, speech and movement should be guaranteed to all, without intimidation.

Kisha nikaja kwa problem ya squatters, kwa sababu sisi tuna watu (Inaudible) ambao wamekaa miaka mingi, kama Faza, Kizingitini, kama hapa Lamu pia, kuna sehemu watu wamekaa kabla sisi hatujazaliwa, na wao wameishi hapa. unapata sasa hivi, hawana title deed, wala thibitisho kuwa hiyo mahali ni pao. Kwa hivyo tuka-recommend, watu ambao wamekaa mahali for more than sixty years, na hiyo mahali itambulikane kama ni kwake, na (Inaudible) awe na haki kamili ya kumiliki ardhi hiyo.

Halafu tukaja katika point nyingine, tukasema pre-independence land treaties and agreements involving certain communities, such as Coastal strip, should be retained. Kama ile mikataba inaandikianwa baina ya watu wa Pwani, wakati wa, - kabla ya Waingereza, wa (Inaudible) Zanzibar, na Uingereza iwe imetambulikana. Kama ile mikataba kwamba watu wa Pwani wamiliki ardhi zao wenyewe. Ni mikataba kama ya Wamasai, kama ya Mazrui, iwe ni kitu ambayo itatambulikana. Kwa hivyo Katiba ni lazima iwe ikichunga mambo kama hayo. Nafikiri hata hiyo muiweke katika kitabu chenu.

Langu la mwisho ni kwamba mayors, nilizungumza habari ya election. tunapendelea mtu kama mayor, ama Chairman awe sponsored awe *ata-votiwa* kama Mbunge na kila mtu. sio awe sponsored ....(End of side A).

... kwa hivyo nafikiri mambo ni hayo tu, na yale mengine yazungumzwe na wenzangu ... (Inaudible).

**Com. Hassan:** Okay, ahsante sana Faisal. Jiandikishe na utuwachie na hii kwa register. Sasa ni wakati wa Shee Mohamed Ali, yuko? Na Silaha Abubakar? Silaha yuko? Haya.

**Response:** Yuko, yuko.

**Silaha:** Salam Aleykum Warakhmatulahi Saalam! Na mimi sina mazungumzo mengi ya kusema, lakini yangu ni machache. Naomba Katiba, tuna Katiba, ma-Chief naomba, - nitakavyo mimi, wote wachaguliwe. Ma- Chief, na wamekuwa wengi, kama vile ambavyo ma-councillor wamepunguzwa, na ma- Chief pia naomba pia wawe watapunguzwa, wawe Chief ni mmoja pekee, kama ilivyokuwa hali yetu ya kizamani. Imekuwa twapata tabu...

**Interjection. (Clapping).**

**Audience:** Endelea bwana.

**Silaha:** Nafahamu. Kwa hivyo hayo ni maoni yangu. Salaam Aleykum warakhmatulahi.

**(Laughter and clapping).**

**Com. Hassan:** Silaha, ahsante. Please tia sahihi. Hambal Omar.

**Hambal Omar:** Asalaam Aleykum! Ikiwa mimi nimeletwa na group la Shia Etna Shariff Community group, tunayo matatizo mpaka sasa, ambayo mpaka sasa hatufahamu mambo yalikuwa vipi mpaka ikawa Katiba zirudishwe tena zipangwe. Matatizo yetu, mavungu haya kutoka huko bara yakawekwa huku. Ni kwa nini? Mbona hatufahamu? Vungu hizi zimetoka bara, kama

(Inaudible) asema kupokonywa. Kama vitambulisho watu wa bara wapata, kama haki zote ni wao ni ma-D. C, ni wao ni ma-D. O, wao ni ma-ex-officers, hawana matatizo kamwe. Kuna nini? Mbona msitueleze ukweli? Ukweli uko wapi? Mbona hamutuelezi? Twataka mutueleze ukweli, maanake watu wa bara hawana shida. Hili gutu limetoka huko. Limetoka huko likaja huku ndio

(Inaudible) ya watu. Sisi ndio hatutaki Katiba? Hayo ni maoni yangu. Ikiwa twataka Katiba, sisi tunayo Katiba yetu ni mswafu. Mswahafu, bungo hatutaki. Na mtu kama hataki hivyo, atoke hapa kamwe, aende kwao. Sisi sheria yetu twataka iwe ni mswahafu. Mungu asema kwenye Qurhan hii takatifu, (*He quotes the Qurhan*). Hukumu inatokana na kwenye mswahafu. Kwa hivyo, ikiwa twataka ahukumu ya kikweli, twataka hukumu kwenye mswahafu. Na ikiwa yeye akudhuru, mswahafu, toka uende kwenyu. Utumie Bible, utumie ng'ombe, utumie utakacho. Lakini iwe ndilo utakalo. Sisi twataka hukumu yetu itumie mswahafu, na mtu kama, - kuna mtu hupiga mswahafu? Hata kinaa?

**Interjection. People:** Hakuna, hakuna!

**Hambal:** Kwa hivyo itakuwaje hata Katiba...

(Inaudible)

**Com. Hassan:** Bwana Hambali, tafadhali toa maoni, kama una maoni ya kutoa, kama hauna, upatie watu wengine tafadhali nafasi.

**Interjection. Hambali ... (Not clear).**

**Com. Hassan:** Ni sawa. Tunataka tumsikize sasa Amina Ahmed. Amina Ahmed... hayuko. Joseph Muteru, F.C.K... okay.

**Joseph Muteru:** Ahsante sana wageni wa leo, majina yangu ni Joseph Muteru, nimetoka

(Inaudible).

Kwa maoni yangu, ya kwanza ni kwamba, - kabla sijaendelea, ningeliza kila mmoja, Katiba ni nini?

**Com. Hassan:** Joseph, tafadhali toa maoni, leo tunataka kusikiliza maoni.

**Joseph Muteru:** Okay, Katiba ni maisha ya mwanadamu, kulingana na mazingara unayoishi. Si mambo ya kuletewa na mtu binafsi, au mimi mwenyewe nilete kwako. Ni maisha unayoishi kwa njia hiyo ambayo unaoishi katika mazingara yako, na kupitia kwa Mwenyezi Mungu. Yangu ya kwanza ni kwamba, -tuingie kwenye maoni yangu sasa-. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba, ni kuhusu kilimo, au agriculture. Kilimo, - tunajua kwamba nchi hii yetu ya Kenya ni nchi ya kilimo, au wananchi wanaishi kwa njia ya kilimo, kwa sababu hakuna madini ya kuenda kufanyia kazi yoyote. Lakini tunapata dhuluma kwa ajili hiyo ya kilimo. Kwa njia gani? Kwa kuambiwa kwamba tunataka soko huru, lakini si kamili kabisa. Hiyo inamaanisha ya kwamba, soko hiyo huru, inamaanisha kwamba, kuna wale pengine wana uwezo, wanapewa nafasi ya kwanza, wapate hiyo soko ili wafanye mambo ya kujinufaisha wao wenyewe. Lakini mtu wa chini kabisa, mwananchi, hapati nafasi hata kidogo. Tunaona kwa mfano mzuri, hapa juzi, watu wamelima pengine mazao ya tomato, mimea kidogo kidogo ya kusaidia watoto waweze kusoma, lakini wanapata tatizo, unaona mkulima anashikwa, analipishwa shilingi mia tatu au mia mbili, ili aweze kuingia katika soko. Lakini ni kwamba tunatakiwa tuwe na soko huru kutoka manyumbani kwetu, hadi kwenye Serikali, au Katiba ambayo inatuongoza wakati tulioko. Au Katiba mpya hii ambayo inatikiwa kutengenezwa, inatakiwa ifikirie mtu wa chini kabisa, yaani mkulima. Kwa sababu hana njia zozote za kuweza kupata soko ya kuenda mbali.

Ya pili ni kwamba, -ni elimu. Kuna elimu ambayo imebandikwa hivi juzi, ambayo ni 8-4-4. Lakini tukiangalia watoto wetu vile wanavyosoma, kuna masomo, au masomo mengi sana ndani, au subject (Inaudible) masomo. Hizo subjects ni nyingi sana katika shule, lakini tungeomba, kupitia kwa Katiba, yarekebishwe haya mambo, kwa sababu pengine huwezi kupata mara moja, pengine masomo kumi na tatu mara moja. Ipunguzwe kulingana na ile career yako, au kama wewe ni engineer, au mtengenezaji wa gari, au wewe ni daktari, ufundishwe masomo ambayo inakuelekeza uwe daktari. Yaani mambo ya pharmacy. Si ufundishwe mambo ya chuma. Kwa hivyo, kuna jamii zingine wako chini sana, hawana uwezo wa kufikia yale mambo kikamilifu kwa ajili ya elimu yao. Tunaona kabila zile ndogo ndogo, kabila zingine ni kubwa, au nyingi. Kwa hivyo, inatakiwa wapate elimu ya kutosha. Ndiposa nasema kwamba, nikitoa maoni ya kwamba, irudi elimu ile ya zamani, ile ya standard seven, ili watoto wetu wapate elimu ya kutosha, na wapate nafasi, wazazi wao wapate pesa za kuweza kuwasomesha.

Nitaguzia habari kidogo ya ardhi. Ardhi inatakiwa itolewe kwa mwananchi wa kawaida ambaye anajulikana ni wa nchi hii, ambaye ana kitambulisho, ambaye ana kubalika katika nchi yake, au eneo lake kwa njia ya haki. Si kwamba mtu anayetoka mbali, - si kutoka mbali kuwa wewe ni mtu wa bara, no. au kutoka hapa Coast, no. Ukitoka hapa Coast uende bara, wewe ni mtu wa Kenya, kwa sababu Coast, au Central ni within Kenya. Uende pale, upate manyumba Nairobi, kama ni ekari moja au ndogo, ujenge ma orofa yako kama wale watu wa Central. Hiyo ndio haki. Kwa hivyo, usiseme kwamba tukae hapa hivi, no.

kama ni mambo ya plot, sisi tunapojenga manyumba kama haya ya biashara, una uhuru wa kuenda kila mahali. Na mimi nina uhuru wa kuja hapa, nina uhuru wa kuenda kama ni Western, niweza kuingia huko katika nchi za waluhya, niweze kukaa pamoja nao kwa sababu ni ndugu zangu. Tuko zaidi ya kabila arobaini na kitu. Kwa hivyo, ukiwa hapa, ni wewe mmoja, ukitoka jina lako, halitaitika ni kabila arobaini, itakuwa ni thirty-nine, sio? kwa hivyo ni mmoja, within that kabila.

**Com. Hassan:** Jaribu ku-summarize.

Okay. Uzaji wa ardhi, uuzaji wa ardhi unatakiwa urudi kule grassroots. Hivyo namaanisha kwamba, kwa wazee vijijini kwa sababu wao ndio wanafahamu, mimi ndio nakufahamu wewe ni jirani yangu, inahitajika yaani ile Katiba iweze kurudi katika kamati ile ya vijijini. Wakati unapouza ardhi yako, ieze kukubalika kwamba unafahamikana. Kwa sababu pengine kuna watu wengine wanatoka Nairobi, wanakuja hapa, akiwa kule, anapigia wale settlement office, wale wanapiga simu kwamba shamba yangu si ni number two, iko? Namuuliza pengine ndugu kama huyu, number yangu iko? Ananiambia ndio. Na sijafika pale. Na kumbe hiyo plot imechukuliwa na watu wengine. Ni hivyo inafanyika hapa Lamu kwetu, unakuta shamba moja ina watu kama watano, lakini yule wa kwanza anakaa Nairobi, anakula mayai, anakula starehe zake, biashara za mbali mbali, lakini yule anahitaji kulima anakuja ananyang'anywa, pengine amepanda mkwaju wake, ama mkorosho au muembe, na anakula

(Inaudible), na anawekwa kwa barabara.

**Com. Hassan:** Bwana Muteru, tafadhali toa mapendekezo yako, usijaribu kutupatia story nyingi.

**Joseph Muteru:** Okay, ya mwisho ni security. Security au usalama, hapa Lamu ni kweli, hata kama ilikuwa imetajwa, security bado ni kidogo. Tunaona hao security ni wengi lakini security ni kidogo. Kwa sababu ile kazi haitekelezwi. Lakini inapaswa kutekelezwa kwa njia gani? Kwa sababu kuna vikundi, G.S.U. Army, Navy, wako within the area. Lakini inatakiwa wao wanaohusika katika hizo sehemu za Katiba, mpeleke hili jambo, liweze kuinua kabisa. Kuna kikundi kama hiki kilichukuliwa juzi, kama ma K.P.R na wengineo, wanafanya kazi within the community. Lakini wananchi wenyewe ndio wanaweza kutoa maoni ya kutosha, kwa sababu wao ndio wamepatiwa kazi. Hiyo security ya KPR inatakiwa iongezeke, ili wale watu wanasaidiana na ile usalama ndani ya vijiji, na ili wapate sehemu ili (Inaudible) kabisa na wapate sehemu yao ya kumi, au msaada wa kulipwa. Barikiweni sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana. Ahsante, tafadhali tunawaomba mjaribu kutoa mapendekezo, because hapa tumekuja kuchukua maoni kuhusu Katiba mpya. Kwa hivyo usiseme tu shida, ukisema shida unatoa mapendekezo yake pia. Ali Debby, hayuko. Ali Mohamed Fami,

**Interjection. Audience:** Hayuko.

**Com. Hassan:** Muna hakika? Zein Mzee, Kenya National Union of Teachers, mwalimu, hapa naona umeandika KNUT, huku

pia umeandika Union, hapa inasema jina yako kwanza ...

(Inaudible). Tupatie jina lako tafadhali.

**Omari:** Omari Bakari. Asalaam Aleykum. Kwa niaba ya waalimu, ningependa kutoa mapendekezo haya: Kwanza tumeanza na preamble, yaani utangulizi. Katika utangulizi wetu, tumeweka kuwa Katiba hii ni ya watu wa Kenya, na itahakikisha usalama amani na maendeleo, na pia Katiba hii itahakikisha kuwa mali ya asili yanagawanywa sawa sawa kwa watu wote. Na kuwa Katiba hii iwe juu ya sheria nyingine yoyote, ama mtu yeyote.

Kwa upande wa uraia, sisi tunapendekeza kuwa sheria ile ya kusema kuwa 'Naturalized citizen,' tunasema kuwa yule 'Naturalized,' apate haki zote kama yule wa kawaida na mambo yote, kama raia wa kawaida. Pili, ikiwa ni Mkenya, ameo ama ameolewa na mgeni, watoto watakao zaliwa wawe ni wenyeji, raia wa Kenya, na yule bibi ama bwana pia awe ni automatic citizen. Tatu, twasema kuwa intimidation na segregation isiweko katika raia wa Kenya. kwa mfano sasa hivi, ukiangalia birth certificate imeandikwa kuwa, birth certificate hii si hakikisho la uraia, hiyo ni form of intimidation. Kwa hivyo iondoke, ifuatane na sheria. Na identification za Wakenya kama I.Ds, na passport, zitolewe freely. Sio you are subjected to a Commission, mbele ya watu.

Kwa upande wa structure na system za Serikali, twasema kuwa hii Presidential system ya sasa iendelee, Judiciary system iendelee, lakini kuwe na autonomy kwa upande wa kusimamia mali ya asili, kama vile samaki na vitu vingine. Na D.D.C. zifanywe kuwa ni chombo cha kisheria. Sasa hivi D.D.C. ni chombo cha Serikali. Kwa hivyo tungesema D.D.C iwe na sitini na tano kwa mia ya wanachama, wawe ni wananchi, chairman wa D.D.C awe ni mwananchi, wale ma-officer wa Serikali watakao kuweko, wawe ni technical persons.

Kwa upande wa Legislature twasema hivi, kuwa mapendekezo yote ya Rais ya kuchagua, kupendekeza watu, yapitie kwa Bunge yahakikishwe. Yaani they should be vetted. Rais ni mwanadamu, anaweza kufanya makosa anaweza kufanya favors. Pia Bunge liwe na uwezo, lakini uwezo wake pia uwe na limitation, kuwe na checks and balances. Pia tuseme kuwa wakati Bunge likiwa liko kwa extension kama wakati huu, Wabunge wetu ambao tumesema wanalipwa mshahara takriban nusu milioni, wawe ni fulltime employees. Kwa hivyo Tuesdays mpaka Thursdays, wakati wa Bunge likiwa in session, Wabunge wetu wawe fulltime. Sio ile mara kuwa Bunge limehairishwa, kwa sababu kuwa ndani ya Bunge kuna Wabunge sita pekee yake. Haya kwa upande pia wa Wabunge, twasema hivi kuwa, nomination ya wale Wabunge maalum kupitia kwa vyama vya kisiasa, vihakikishe kuwa vinazingatia zaidi zile marginalized groups. Kwa mfano wanawake, watu wasiojiweza, na pia interest groups. Kwa mfano, vyama vya wafanyi kazi, walimu, wanajeshi, na pia wale wenye kuweka uchumi, -industrialists-, wapatiwe kiti katika Bunge, angalau. Kwa upande wa Rais, twasema kuwa ile mpangilio wa sasa wa Rais kuwa na vipindi viwili uendelee, na lakini, kazi za Rais ziwe redefined, na uwezo fulani uondolewe. Kwa mfano, Rais aondolewe uwezo wa kuliita na kilivunja Bunge, aepuke uwezo wa kuitisha uchaguzi, kwa sababu mara nyingi anasema hiyo ni secret weapon, hiyo secret weapon iwe na Bunge yenyewe. Halafu pia apokonywe uwezo wa kutoa ardhi, ama pesa ya aina fulani kwa sababu za kisiasa.

Na mwisho nitasema kuwa, walimu wanasema kuwa Provincial Administration yaweza ikaweko, lakini ule wajibu wake uwe redefined. Kwa upande wa Judiciary, walimu wasema kuwa Kadhi's court ipatiwe powers za pia kusimamia mambo ya watoto. Yaani ile children's Act kwa upande wa Waislamu, irudishwe kwa Kadhi, awe implementing agent.

Pia, Kadhi na Chief Kadhi, wawe na kiwango cha elimu cha degree, kama ma-officer wengine wa court, na kwa kuwa wao ni Waislamu, wawe na angalau diploma katika somo la wanasheria wa Kiislamu. That is, from a recognized university, a diploma in Islamic law. Pia Kadhi's court, iwe na kiwango cha mtu kukata rufaa. Isiwe ukihukumiwa kwa court ya Lamu, huwezi kuenda mbele. Pia twasema kuwa, Kadhi awe na court assessors. Ikiwa ni kesi ya talaka, ambayo ni kesi ngumu, ama kesi ya urithi, Kadhi aruhusiwe kuita court assessors, wana vyuoni kama wanne wasikilize kesi pamoja, na wakate uamuzi pamoja.

Nne, nyingine, twasema kuwa Serikali impe huduma za kisheria, that is to say, legal aid. Mtu yeyote Kenya, akifanya kosa lolote, akiwa ameuwa, amefanya nini, yeye hana uwezo wa kuajiri wakili, kwa hivyo Serikali ihakikishe imempa legal aid, ndio itasaidia kuonyesha haki. Kwa sababu ikiwa yeye amedhulumiwa na tajiri, na yeye hana uwezo wa kuweka wakili, tajiri atahonga, tajiri ataandika wakili hodari, na yule atashindwa.

Kisha twende kwa local Government, twasema pia sisi walimu kuwa mayor, na chairman wa County Council, na municipal council, na city council, wachaguliwe moja kwa moja na raia, na awe na kipindi cha miaka mitano, na pia local authority ipatiwe autonomy zaidi. Sasa hivi, bwana Waziri wa mambo ya Serikali za mitaa, ama local Government anaweza kumfuta mayor ama councillor ambayo si sawa. Pia twasema kuwa ni lazima kuweko na...- there should be moral and ethical qualifications kwa councillors na Wabunge. Na pia kwa upande wa ma-councillors twasema kuwa tu-retain hii system ya nominated councillors, lakini pia tuzingatie wanawake, wasiojiweza, na zile other interest groups. Kama tuliwaambia Waboni wako kando na maendeleo, kwa hivyo Lamu County Council itenge kiti kimoja kwa Waboni masadan. Kwa upande wa electoral systems, twapendekeza kuwa mtu yeyote ambaye ame-fail kupata kiti kupitia kwa chama, asiruhusiwe to cross to another party. Yaani... *(End of tape two)*.

*(Beginning of tape three)*. Ikiwa wewe ume-see nomination kwa Kanu, na umeshindwa katika mlolongo au njia yoyote, usiruhusiwe kuruka sakafu kuenda D.P, au chama kingine. Kwa sababu hiyo inaonekana you are not patriotic, you are just after the Parliamentary seat. Kwa hivyo Katiba itakayokuja ihakikishe, mtu aamue, mimi nitasimama kwa Kanu, kupata, kukosa ni Kanu. Kitu kingine, ni kuwa tuwe na mpangilio huu wa kisasa wa viti. Tatu, tuendeleo kuwa na kura za Rais na Wabunge kwa siku moja kama ilivyo kawaida.

Kwa upande wa haki za msingi, that is basic rights, twasema kuwa elimu, elimu ya msingi, ile E.C.D. yaani Early Childhood Education, and Primary school education, sheria ihakikishe kuwa inakuwa ni ya bure na ya lazima kwa kila mtu. Na iwe ya bure kweli. Sio kuwa ni ya bure, halafu Rais ama Waziri aseme "local communities sit down and consider a figure," la. Ikiwa ni bure, iwe ni bure. Haya, halafu twasema pia kwa upande wa elimu kuwa ya bure na kuwa mzuri, director wa education,

**Com. Hassan:** Summary please.

**Omari:** Okay, Director wa education, na Chief inspector of schools, hizo ziwe considered as Constitutional offices, with security of tenure, ili waweze kufanya kazi independently. Pia tungetaka huduma za afya, za msingi. Kwa mfano katika dispensaries up to district level ziwe bure. Sio saa hizi unakwenda hospitali, halafu unaambiwa toa shilingi themanini za dawa, ilhali wewe huna shilingi ishirini za chakula. Kwa hivyo huduma ziwe za bure, maji yawe ni ya bure na yapatikane. Pia wafanyi kazi wote waruhusiwe kuwakilishwa na vyama vya wafanyikazi, na makubaliano yoyote baina ya Serikali, au mwajiri na mwajiriwa, ni lazima yatekelezwe.

Kwa upande wa ardhi tunasema kuwa, ardhi imilikiwe na wenyeji, mpaka katika sub-location level. Kwa mfano ikiwa kuna land control board, land allocation board, hizi zianze kutoka sub-location. Halafu pia katika management ya ardhi, kuna seventeen different acts of Parliament, ambazo hizo zinasaidia grading of land. Kwa hivyo tunataka hizi seventeen Acts zichanganywe pamoja, iwe one single Act, au two Acts. So that, mwananchi wa kawaida aweza kuzisoma na akazielewa. Kitu kingine, lazima kuwekwe kiwango cha kumiliki ardhi. Pia kitu kingine tumesema kuwa Katiba ihakikishe kila mwananchi anakuwa na ardhi. Kwa upande wa culture ethnic and regional diversity, walimu wanasema kuwa Waswahili watambuliwe kama kabila, kwa sababu wana mila yao, wana lugha yao, na wana identity yao. Sasa hivi tunazungumza lugha yao, sijui wenyewe wako wapi? Kitu kikingine twasema kuwa, Katiba pia itoe uhakikisho, against discriminatory aspects of culture and origin. Na hiyo ni kusema kuwa katika acquisition of employment na mambo mengine.

Kwa kitu kingine ni management and use of natural resources, ni kusema kuwa ile uwezo wa Serikali kusimamia mali ya asili, uletwe chini mpaka kwenye District. Na...

**Interjection. Com Hassan:** You have taken more time than I have given you. Please try and sum up.

**Omari Bakari:** Lakini Bwana Commissioner, this is the only opportunity walimu wa Lamu watewaza kuzungumza. Kwa hivyo tafadhali just another three minutes.

**Com. Hassan:** But you know you people have written submissions. Hata ukisoma saa hii bado itakuja kwa Commission.

**Omari Bakari:** Sawa, nataka watu wengine wasikie na kama press iko hapa isikie. Ahsante. Haya, kitu kingine ni katika environment na natural resources. Tumesema local communities zihusishwe katika hiyo, na natural resources zote ziwe protected by the Constitution. Na kitu cha mwisho, ni katika hizi Commission, twasema kuwa Serikali ianzishe ofisi ya ombudsman, ambaye atapokea malalamiko ya wananchi wote, ikiwa wamekosewa, na itachukua malalamiko from, - against the three arms of Government, na pia iwe na uwakilishi katika eneo la ubunge.



Mwisho ni kusema katika succession and transfer of power, ili kuhakikisha proper and successful transfer of power, Rais, wakati wa kuchaguliwa Rais, kuwe na running mate ambaye atakuwa ni vice President ili kuepuka mambo yaliyoko leo Kenya. leo Kenya tuko na succession battles. Lakini kama tungekuwa na Makamu wa Rais aliyechaguliwa, hayangekuwako. Pia ikiwa wakati Rais aliyekuwa ambaye yuko, pengine akifariki ama akiwa ataondoka kwa njia yoyote, twapendekeza kwamba Makamu wa Rais achukue, ikiwa Makamu wa Rais hawezi, Speaker wa Bunge achukue, na ikiwa speaker wa Bunge hawezi, Chief Justice achukue hapo mahali kwa muda wa miezi tatu, kisha aweke uchaguzi.

Halafu mwisho, ambayo si mwisho kabisa, ni kusema kuwa, Rais mstaafu apewe attractive retirement package, ambayo itakuwa na usalama, nyumba na welfare yake. Lakini walimu wanasema, ikiwa Rais ambaye yuko mamlakani atajiingiza kwenye active domestic politics, kwa hivyo sheria ama Katiba imnyang'anye yule Rais zile haki zote za former President. Kama vile ilivyokuwa Zambia. Hii ni kuepusha duplication of power. Kwa sababu katika Katiba yetu mpaka sasa, hakuna limit ya chama kiko wapi, na Serikali yaanzia wapi. Kwa hivyo ikiwako hii sheria, ndio itaweza kusaidia. Kwa hivyo nimeshukuru, na hayo ndio maoni ya walimu. Ahsante.

**Com. Dr. Mosonik:** Swali moja, umesema kuwe na kiwango cha juu cha ukubwa wa ardhi, lakini hukutueleza kiwango, kipi?

**Omari:** Kwa kuwa hili swali tumelipita na umeniuliza sasa, nitaeleza pengine kwa maoni yangu ambayo nafikiri walimu wale walioko hapa wataniunga mkono. Sisi twasema acre hamsini. Na zile ambazo zitakuwa ni zaidi Serikali izichukue na pengine tuambiwe sisi wengine tuzinunue. Kwa hivyo 50 acres, anywhere in Kenya.

**Com. Hassan:** Thank you very much mwalimu. We come to Mohamed Somo, from Faza.

**Mohamed Somo:** Salaam Aleykum. Yale nitakayo yasema mimi, yote yamekwisha kusemwa, kwa hivyo nitachukua muda mfupi sana, kwa vile wanalia time. Kwanza mimi niko kwenye msimamo wa Serikali za majimbo, na haki zake. Hii namaanisha kwamba, tukipata majimbo, zile haki na matunda yake, yaje kwa watu wa jimbo hilo, kama walivyosema wenzangu. Na iwe 50% ina-benefit hilo jimbo kwa kuimarisha na kustawisha hilo jimbo, zisitoke tu hapa, zikaenda huko juu. Na sisi hapa jimbo la Pwani twajua tunao, jimbo letu ni nzuri, lina mazao mazuri, lakini yale mazao ndio hatuyaoni. Kwa hivyo, kile tunataka, itupatie hiyo.

Pili, mimi natoka Faza. Faza kule na Kizingitini na sehemu zote sisi uchumi wetu ni samaki, na ukulima. Lakini sasa leo Serikali hii, ambayo tuliyonayo, imefanya maisha ya samaki, na maisha ya wanyama, ni bora kuliko binadamu. Imetuwekwa park sehemu ambazo tunaweza kutoa samaki kwa uzuri, na tukaenda tukauza. Inatuwekwa Park. Tunataka Katiba hii itoe uhuru wa bahari, vile wavuvi wanavyopata faida. Na wakitaka kufanya park wasifanye (Inaudible) tu huko Nairobi, sehemu fulani in fact waje wapige tu. Waende waelewane na wavuvi ni sehemu gani kama sisi tungetaka kuhifadhi



mazingara ya samaki.

Kadhalika, mashamba. Ile sehemu za madodori ambazo sisi tulipokuwa watoto tukizilima, zilikuwa ndio sehemu zinatoa mazao mazuri, Zinafanywa Park. Ili kutawanyisha maisha ya wanyama ni bora kushinda maisha ya binadamu. Tunataka Katiba hii ifikirie binadamu kushinda wanyama.

Jambo lingine, number four hiyo. Wananchi katika passport huwa tunaandikiwa tatu, ukoo, kuzaliwa na kujiandikisha. Kwa hiyo, tunataka Katiba hii isimame kwenye msimamo huo huo. Kama mtu amekubaliwa kuwa mwananchi, awe na haki ya wananchi. Hivi sasa kuna wanaume ambao wamenunua uwananchi, wamezaa na watu wetu, wamezaa na dada zetu, mkiwanyima haki hiyo, ndio kuwanyima watoto wetu haki zao. Tuna kina mama wetu wameolewa na wababa zetu, wameowa wengine, na wamezaliwa. Ukiwanyima haki yao ya uwananchi, kama makaratasi yaliyotolewa hapa, ni kuwanyima watoto haki yao. Hiyo ndio nasema. Land taken by outsiders, ardhi inachukuliwa na watu wa nje? pia sasa kuna mtu ambaye si wa district hii wala hajulikani, alikuja juzi na jana tu hapa, ana ardhi, -nimesahau karatasi ningewaonyesha ambayo mwananchi wa hali ya chini yeyote hajaipata wala haipati. Hiyo pia Katiba hii iangalie maisha ya wananchi hali ya chini kidogo, ili nao wapate umilikaji. Kwa hayo machache, yote ningeyasema nafikiri wenzangu wameyasema, lakini tunataka Katiba hii, katika hayo niliyoyasema, ifuate. Na makaratasi yaliyotolewa hapa, si makaratasi ya wageni wote walio (Inaudible) msikitini kutoka Kenya nzima. Hii (Inaudible) ni mia moja, na wana-save personal hatred. Kwa hayo, ahsanteni.

**Com. Hassan:** Thank you very much Mr. Mohammed. Tafadhali utupigie sahihi register yetu. Abdala Abbas, hayuko. Twalib Mzee, Omar Twalib Mzee, huyu Twalib Mzee ni Chief? Kennedy Mwaingi, sorry, huyu ni observer. Twende kwa Hassan Said, hayuko. Elijah Shibira, Methodist Church? Okay.

**Elijah Shibira:** In fact it is N.C.C.K.

**Com. Hassan:** N.C.C.K? Jaribu kufupisha maoni.

**Elijah Shibira:** Okay. Ma-Commissioners, mabibi na mabwana hamjambo?

**Com. Hassan: ... (Inaudible).**

**Elijah Shibira:** Ninataka kuenda mambo mafupi sana. Jina ninaitwa Elija Shibira. Ningetaka kusema mambo mafupi sana, ambayo pia yamezungumzwa na kina mama. Habari ya urithi ndio ningetaka tu kuongezea kidogo. Sisi tunapendekeza ya kwamba, mimi nikifa, katika sheria yetu ya Kenya, iweke wazi wazi ya kwamba bibi yangu, ama yeye akifa, mumewe ambaye ni mimi, atakuwa ndiye mrithi pamoja na watoto. Na tukasema ya kwamba, ikiwa bibi huyu ataamua kuolewa na bwana mwingine, basi sheria iweke kipengele cha kwamba, mali ile ilio wachwa na yule aliyekufa, kama ni bibi au ni bwana,

tunapendekeza ya kwamba kuwe na kipengele cha kufanya mali ile igawanywe kwa watoto wale, mdogo awe na sehemu kubwa ya mali ile, na yule mtoto ambaye ni mkubwa, bila shaka kwa ajili ya umri wake amekula vingi, atakuwa na kitu kilicho chini kidogo ya yule mdogo. Na bibi naye awe na kitu kidogo chake, ili akiolewa watoto wale wawe wana urithi kamili wa baba ama mama. Na tumependekeza hivyo kwa sababu bwana akiwachiwa watoto, ni rahisi kuuza mali ile, watoto wakose, ili apate pesa za kuoza bibi mwingine.

Na tunapendekeza pia ya kwamba katika Katiba mpya, ikiwa mmoja wa bibi ama bwana ni mwananchi wa Kenya na mwingine ni mgeni, basi mgeni yule, kuwe na uhuru wa yeye kuchagua. Kama anataka uwananchi, basi afanye application, na tunapendekeza ya kwamba akisha apply yeye, haingewezekana kwa vyovyote apewe kazi katika Serikali kwa sababu ya security reasons. Hiyo ni shida ambayo tunajaribu kuingalia, - tumejaribu pia kuangalia jambo la kumiliki ardhi. Ardhi Kenya ni ndogo, na haiwezi kuongezeka maana haizai, ni ile ile. Kwa hivyo, tumependekeza ya kwamba kuwe na sheria. Ardhi tuliyonayo, ikisha gawanywa, mtu akipatiwa kipande chake, iwe ni mali yake yeye, pamoja na Serikali. Kwa sababu huyu mmoja ikiwa .....

**Com. Hassan:** ... (Not clear). Endelea.

**Elija Shibira:** Ahsante bwana. Lazima tumuheshimu Mola. Tunapendekeza habari ya wananchi, mambo kama haya yafuatayo. Kwamba yeye awe mwananchi wa nchi moja, asiwe mwananchi wa nchi mbili, ama sivyo tutajikuta tuko kwenye matatizo. Na tunapendekeza ya kwamba, huyu mwananchi, ama mtu mgeni ambaye atajiandikisha kuwa mwananchi wa hapa kwetu Kenya; asikubaliwe, - sasa nazungumzia yule amekuwa mwananchi kwa kuomba, asikubaliwe hata kidogo kununua ardhi, isipokuwa Serikali ichanganye kitu kimoja kuwe na kipengele cha kumfanya mtu yule atakayenunua, asinunue zaidi ya acre hamsini. Na ikiwa ameshanunua, aangaliwe ya kuwa, je? katika yeye mwenyewe kama mwananchi, ana mali gani? Ana pesa kiasi gani ambazo ziko bank? Na kuwe na kipengele cha kumfanya kwamba haya mali yake asiweze kuyahamisha kwa siku moja, Kwa ajili ya usalama wa nchi yetu. Tungependekeza kuwe na Serikali ambayo kutakuwa na mtawala, President, kisha kutakuwa na yule mwingine anaitwa Prime Minister.

Ningetaka kugusia mambo ya lami, na niyamalizie hapo, kwa sababu kuna council tuko nayo, nayo ni hii: Nchi haiongezeki, bahari hii tuliyonayo haiongezeki. Tulipendekeza ya kwamba, mimi ikiwa nimezaliwa pahali kama hapa Lamu, uhaki wangu uko hapa Lamu. Kwa sababu wewe mwananchi wa Lamu, samaki aliye hapa ni mali ya wewe mtu wa Lamu. Kuja kweli kupokonywa, - jambo hili tuliliangalia tukasema si jambo linalofaa-. Kwa hivyo tukasema, msitu kuwa pahali pale utunzwe, na utunzwe na nani? Utunzwe na Serikali, pamoja na mwananchi wa pale. Kwa sababu tukiweka Serikali, ni Serikali pekee yake, Department ya Forest tuko nayo, lakini anaenda anahongwa shilingi mia mbili na wanaikata misitu yote, sasa tabu inatuingilia Kenya nzima hakuna mvua, hakuna maji, matatizo yanatuingilia. Tukasema ya kuwa kama kuna mnyama pale, mnyama yule asitunzwe na Serikali pekee yake. Ile Serikali ya watu wa wildlife. Mwananchi naye wa pahali pale naye atunze. Tena tukapendekeza ya kwamba, waheshimiwa, ya kwamba, ikiwa basi kuna kitu kama hivyo, ikiwa ni vitu vya kuuzwa, kama kuna

utalii katika area ile, kuna mhogo, watalii watakuja waangalie, basi mimi mwananchi ama mwenyeji wa area ile, ile outcome ya kutokana na ule utalii, na sisi wenyeji wa sehemu ile, tupatiwe. Sio kuchukuliwa inaenda kufanya kazi za Nairobi, na sisi huku tunakuwa hatuna hohe wala hahe. Tukapendekeza basi ya kwamba, misitu, maji wanyama, iwe inalindwa na -vipengele viweko, iwe inalindwa na Serikali pamoja na wenyeji. Ningetaka kumalizia hapo, na naamini ya kuwa katika karatasi hii tumeweka mambo haya wazi wazi, na Mungu awabariki.

**Com. Hassan:** Ahsante sana mzee, piga sahihi hapo. Sauda Kassim, yuko? Naona wewe ni mtu wa kutoka kwa maisha ya Annaswiha. Kwa hivyo nitakupatia wewe uongee kwa niaba ya Annaswiha.

**Sauda Hassan:** Mimi ni mwenyekiti wa Annaswiha Women Group, Lamu, na katika kikundi chetu kinahusisha akina mama pamoja na wasichana, yaani youth and women. Sisi, baada ya kushauriana na kubadilishana fikira na mawazo, juu ya maswali kadha, tulikuwa na mapendekezo machache yanayo fuata. Pendekezo la kwanza ni kuwa, kuhusu maadili yanayopaswa kuwekwa kwenye Katiba, sisi twaona kuwa ni muhimu sana kwetu sisi Wakenya kuwa waangalifu mno, katika kuchukua maadili ya kimagharibi, kwa sababu mengi ya mambo ambayo kwa vipimo vyao ni mzuri, na muhimu, kwetu sisi mambo hayo, hayo ni mabaya, na yasiyofaa hata katika maswali ya mambo ya kijamii. Kwa hivyo tulisisitiza Katiba ifafanue wazi juu ya misimamo yetu, juu ya maswali aina hiyo. Kwa mfano, kwa nchi nyingi za kimagharibi, tendo la ngono baina ya mwanamke na mwanamke, au mume na mume ni jambo la sawa, na hawalioni na makosa yoyote, ambapo tendo hilo, na mfano wake, kwa mila yetu, na desturi na dini, ni mambo ambayo ni ya kinyume kabisa, na mwacha mila ni mtumwa, mila ikiwa ina madhara ya kiafya au kiuchumi, madhara yaliyodhahiri, huwa si sawa, bali yapaswa kutupiliwa mbali, lakini tusiache mila yetu mizuri kwa ajili ya kuiga Wazungu.

Katiba, iwe imeandikwa katika lugha ambayo imefahamika na kila mtu. Ili maana mtu anapoambiwa kurekebisha Katiba, iwe kwake ni rahisi katika kujua ni makosa gani yako, na kurekebisha vipi.

**Com. Hassan:** Sauda, naona uko na written submission. Usijaribu kusoma word for word. Jaribu tu ku-highlight zile main points.

**Sauda:** Katiba, Bunge liwe na mipaka katika uwezo wa kubadilisha Katiba. Maswali yote ya kijamii isiwe Bunge pekee yake litaamua, bali ni lazima umma ushirikishwe na kupewa nafasi ya kutoa maoni yao.

Uraia. Uraia, mtu yeyote ambaye yeye hakuna mahali duniani anapoona kuwa ni kwao, isipokuwa Kenya, basi mtu huyo awe ni raia wa Kenya bila swali lolote. Kwa mfano, hapa Kenya wako watu wengi ambao akili zao wanakusudia mababu zao wametoka Arabuni au Uajemi, watu hao hawana jamaa huko wanakoambiwa ni kwao. Wala hawana mali yoyote, bali hata hawajui kwa hakika ni mji gani ambao mababu zao walitoka. Watu hao ni lazima wawe ni sawa kabisa na Wakenya wengine wowote, kwani wengi wao katika watu hao, mababu wao walifika Kenya, hata kabla ya mababu ya wengine katika wale

wananonekana kuwa ni Wakenya halisi. Vile vile twaona kuwa Katiba isiruhusu raia wa nchi ya zaidi moja.

Serikali. Tunapendekeza mfumo wa majimbo ule uliokuwa Kenya wakati wa uhuru, na kuna uwezekano wa kufanya marekebisho ya mipaka. Uwezo wa Rais upunguzwe, na asiwe na madaraka zaidi ya moja. Pia awe chini ya sheria kama Mkenyamwingine yeyote. Vile vile neno lake lisiwe ni sheria, lichukuliwe ni pendekezo ambalo litajadiliwa na Bunge. Bunge liwe na uwezo wa kufuatia mambo yote ya kiserikali, na waamue juu ya maswali yote ya nchi za kigeni. Kwa mfano, kupeleka majeshi nje ya Kenya kuhudumia shughuli za umoja wa mataifa na kadhalika. Wabunge wasiwe na uwezo wa kuamua juu ya mambo ambayo yanawahusu moja kwa moja, masilahi yao, kama mfano wa kujadili mambo ya mishahara na kadhalika. Wabunge walioteuliwa wasiwe na madaraka yoyote mbali na ubunge. Mtu yeyote aliyewahi kushtakiwa kwa kosa la uhalifu, basi asikubaliwe kupigania kiti cha ubunge.

Mahakama ya Kadhi. Mahakama zetu zifanye marekebisho, haswa upande wa kesi. Iko dharura ya kesi ndogo ndogo ziwekwe taratibu ya kuziharakisha kusiwe na mambo ya nenda rudi. Kesi ndogo ndogo zifanywe haraka ili zimalizike. Mahakama ya Kadhi iwe na uwezo wa kushughulikia maswali mengine, mbali na mambo ya ndoa na talaka na miradi. Iwapo wanaohusika na shtaka, watakubaliana wote wawili kuhukumiwa na mahakama ya Kadhi. Kama vile mahakama ya kienyeji zinavyofanya, katika mahakama ya Kadhi, kuwe na (Inaudible) la ushauri na nasaha, la kuwa ushauri mume na mke kabla hawajaanza kushtakiana.

Makadhi ni lazima wawe na shahada ya chuo kikuu kinachokubaliwa katika somo la sheria la Kiislam, kwa kiwango cha chini kabisa, mtu awe na L.L.D. Manaibu wa Kadhi wateuliwe na watu wenyewe katika kila kijiji. Mahakama ya Kadhi iwe na uwezo wa kulazimisha mababa kutimiza mahitaji ya watoto wao sawa, wakiwa na mama zao au wakiwa wametengana. Mahakama ya Kadhi iwe na uwezo wa kusimamisha ndoa ya mume ambaye ana mke, mpaka mahakama hiyo itosheke kuwa mume huyo ana uwezo wa kutimiza mahitaji ya yule mke mwingine, na bila ya kumnyima mke mwingine haki yoyote katika haki zake. Inginge ni mayor na wenyeviti wa mabaraza za wilaya wachaguliwe moja kwa moja na Wananchi. Pia wananchi wawe na uwezo wa kumwondoa diwani wakati wowote, akiwa hakufanya kazi yake baada ya mwaka mmoja au mbili.

Jambo lingine ni katika shule, au taasisi zozote za kielimu zilizoanzishwa na makundi ya kidini. Mtu asiyekuwa wa kundi hilo asilazimishwe kusoma masomo ya dini hiyo, wala kushiriki katika shughuli zozote za kidini, ambazo ni kinyume na itikadi yake.

Na mwisho kabisa, wanawake walioajiriwa na Serikali, au mashirika, au na mtu binafsi, wawe na haki ya kupata leave ya eda iwapo watafiliwa na waume zao. Ahsanteni.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Sauda kwa hayo maoni yako. Tafadhali kuja utupigie sahihi kwa register. Anafuatiwa na Mohamed Bwanamkuu. Mohamed Bwanamkuu, Hayuko. Omar, Abubakar M.A.L. Hamoud, hayuko?

**Audience:** Yuko.

**Abubakar:** Jina langu kama mlivyoambiwa ni Abubakar Ahmed Ali L. Hamoud. Commissioner nafikiri pointi nyingi zetu kuhusiana na mambo ya Katiba, kuna mzee ambaye, kwa maandishi atakuja hapa, kutueleza. Mimi pengine nitazungumza kwa ufupi,

**Com. Hassan:** Mzee mgani? Anaitwa nani?

**Abubakar:** Hussein Soud. Kwa ufupi nitazungumza mambo machache ambayo pengine hatukuwa na wasaa kuyazungumza. Kwanza ni kuhusu hizi tirabu zetu za kiasili, za kitamaduni. Utakuta katika Kenya ni sehemu chache sana huona museum. Kwa hivyo tunataka katika Katiba mpya kuwe na policy ambayo kila District kuwe na museum ili kuchunga mila, desturi, na hizi historic artifacts na monuments, ambazo ziko katika Kenya. Kadhalika, kuwe na sheria kali sana ambayo *ita-stopisha* wale watu ambao wanachukua archives na kuzihamisha. Vile vitu vya kizamani vya kiasili vya hapa, wanavichukua na kupeleka nje? kuwe na sheria kali ya kuwazuilia watu kama hawa. Na vitu kama hivi, kuwe na legislation, kuna vitu vingi ambavyo viko nje ya nchi ya Kenya. Ukienda nchi nyingi za nje? utapata mambo yetu ya hapa Kenya, yako huko, kuliko kuwa yako hapa. Kwa hivyo tunataka vitu hivyo vyote viregeshwe nchini Kenya na virudi katika museums.

Kadhalika, kuna wale wavuvi wa kigeni, ambao wanavua hapa Kenya. Kwa hivyo hao wanamaliza samaki wote, hata wale wadogo. Hata majumba ya samaki wanamaliza. Kwa hivyo wale wavuvi wetu wa hapa hawapati samaki, hawapati kuvua samaki, hawapati samaki kwa sababu ya kuingiliwa na wavuvi wa kigeni. Kwa hivyo mambo kama haya yazuliwe. Na kadhalika wavuvi wapewe misaada ili waweze kutoa samaki wa kutosha.

Kadhalika, kuna mambo ya michezo. Michezo katika Kenya utakuta imefifia sana, kwa sababu serikali yenyewe haitii mkazo katika michezo. Na ndio ukaona vijana wameingilia mambo ya madawa ya kulevyaa, na mambo mengine. Kwa hivyo tunataka katika hii Katiba mpya, katika kila district kuwe na ground, sports ground ya kisawasawa, na facility zote ziwekwe, ili vijana wapate kuendelea katika mambo ya kimichezo. Kadhalika, ikiwezekana hata katika tarafa, kuweko na sports ground ili mambo kama haya yapate kuendelea. Michezo, na madhara mabaya kama drug abuse yapate kuondoka na vilabu vitapata kuendelea kimichezo.

Kadhalika, kuna hizi natural resources ambazo zinapatikana katika Kenya. Kila sehemu ina vitu ambavyo vinazaa mali ya asili, Lakini haya mali ya asili yana-generate income, yanatoa pato. Na hili pato twataka litumiwe katika mambo ya infrastructure kama mabarabara, kama ma-hospitali, utasikia hakuna madawa, pesa kama hizi zingekuwa zikihudumia mambo kama haya. Kadhalika kuna utalii mwingi. Kwa mfano, kama hapa Kenya, haswa Pwani, utakuta mabarabara hakuna. Kwa mfano kama Lamu, sasa imekuwa imechaguliwa katika world heritage site. Sasa tunataraji watalii wengi watakuja hapa. Sasa ikiwa hakuna barabara nzuri, kweli watalii watakuja? Haiwezekani kuwa tunaweza kupata kitu kama hicho.

Natilia mkazo ya Waswahili. Waswahili wako, wana lugha yao, wana mila yao, wana utamaduni wao, wana utu wao. Kwa hivyo tunataka kabila la Kiswahili liweko, - mimi nashangaa, ukienda katika kituo cha kujiandikisha, Wabajuni. Wabajuni ni nani? Si Waswahili? kuna kabila Wajomvu, kuna kabila Wasiuru, kuna kabila Wapate, kuna kabila Waamu. Kwa hivyo Bajuni ni moja katika kabila la Kiswahili. Kwa hivyo Kiswahili twataka iingie kwamba ni moja katika kabila za Kenya. Kisha atajulikana yule, ni wa wapi? Ni Muwamu, ni Mjomvu, ni Mvita na kadhalika. Kwa hayo, ahsanteni sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana, ahsante sana Bwana Abubakar. Ali Aboud yuko?

**Ali Aboud:** Asalaam Aleykum warakhmatulahi wabarakatu!

**Com. Hassan:** Naona kama uko na written submissions? Kwa hivyo usichelewe sana, just summarize.

**Ali Aboud:** Mimi nitaanza na Lancaster House. Nitaanza na Lancaster House. Hapa Lancaster House, ndiko kulikuwa na vurugu la kila aina. Mimi naona hayo yote tunazungumza, lau tutakuja kukubaliana kuwa tuanzie hapa Lancaster House, nafikiri mambo yatakuwa mazuri, au yatakuwa mafupi. Maanake, kuenda huku, kuanzia huku, kurudi huku, kuja huku - maanake Katiba iliandikwa mpaka sasa nafikiri bwana Omar Shaban alikuja akatuonyesha hapa, ya kuwa Katiba ni nini, ambayo iliandikwa Lancaster House, na Katiba ile ndio iliyofanya hiyo faratu kukuja hapa kwa teke, mpaka haliitwi hivyo sasa.

**Com. Hassan:** Bwana Ali, tafadhali anza kutoa mapendekezo sasa.

**Ali Aboud:** Kwa ufupi tu, hapo hapo Lancaster house, nina neno moja nataka kulisisitiza. Wajua watu walichaguana wakisema tumchague mfalme. Basi wakasema haya, tumchague mfalme. Basi twataka kuchaguliwe mfalme, atachaguliwa na namna? Namna gani atatutawala? Lakini kama angechaguliwa na dagaa, ingekuwa (Inaudible). Kwa hivyo, sasa twataka utawala wa majimbo. Katika utawala wa majimbo, mimi ningependekeza hivi, ya kuwa -tuanzie katika utawala wa jimbo, yaani kutakuwa na Rais, kutakuwa na wajumbe na mambo mengine tena. Lakini kuna kitu kimoja, katika utawala huno wa majimbo, mimi nakusudia utawala wa majimbo wa district pekee yake. Na mazungumzo yangu sana nina-base katika Lamu district. Kwa sababu katika district yetu ya Lamu, kuna mambo mengi, ambayo sisi, lau tukizingatia kweli, kweli au tuki

(Inaudible) mengi ni mambo ambayo tume... -mimi naona tumeonewa-. Kwa mfano, kuna madude hapa Pwani hapa ya timber, na hujui wewe unafanya nini, wafanyi kitu gani wakati gani, wakati gani unafanya kazi, wala hakuna hata mtoto wetu mmoja ambaye ameandikwa kazi pale. Basi ikiwa hiyo Katiba ambayo sisi tutaiunda hivi sasa, itaweza kulinda mambo kama hayo, sijui lakini mimi naona Katiba ni karatasi tu, kama karatasi ya aina yoyote. Kwa hivyo ikiwa kwa ile karatasi ya zamani ya Katiba ya zamani haikuweza kulinda haya mambo, hii mtakayo tengeneza sasa ndio itaweza kulinda? Lakini fanyeni hivyo hivyo.

La mwisho naja katika habari ya Taasisi. Taasisi zote zilizoko katika Lamu, -tuseme Kenya, mimi ningependelea Taasisi hizi zichaguliwe na watu binafsi. Zisiwe zitachaguliwa na kama tuseme kwa mfano Rais, au nani. Kwa sababu zile zikichaguliwa na watu kama Rais, zitashindwa kufanya kazi. Kwa sababu kutakuwa kuna watu wengine ambao, ama Taasisi zile zitakuwa zikimheshimu yule, haziwezi kufanya kazi kisawasawa. Lakini lau zitachaguliwa na watu, zitaweza kufanya kazi sawasawa. Na hapo tuseme kwa mfano, kama Mkuu wa Sheria, au uchukulie kama Muislamu mkuu, au yule maanake Mwakilishi wa Tume ya marekebisha ya Katiba, na mambo mengine mengi. Lau kama team hizi zingechaguliwa na watu binafsi, au na wananchi, zingekuwa leo zaweza kufanya mambo yake kisawasawa. Lakini mimi nina hakika bila (Inaudible), team hizi zote ambazo, au Taasisi zote hizo ambazo zimechaguliwa, kuna mahali pengine ikifika lazima wapige breki, hayawezi kuenda popote. Kwa sababu bwana fulani hataki vile. Kwa hivyo mimi ningepomba, kutoka sasa, maanake hizi team – hizi Taasisi zote zichaguliwe na watu binafsi. Sio zichaguliwe na bwana fulani, awe ni Rais, awe ni nani. Mimi naona hiyo itakuwa haitusaidii chochote. Kwa hayo machache mimi naona ahsante sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana bwana... Mzee. tafadhali utupigie signature hapo. Sasa tunamtaka Ahmed Swaleh, ambaye atafuatiwa na Ahmed Omar, halafu Omar Mkenzi na Hussein Soud.

**Ahmed Swaleh:** Salaam Aleykum! Bismilahi Rwahmani Rwahim. Ningependelea la kwanza Kadhi kama wenzangu walivyosema, Kadhi wetu wa Kenya achaguliwe na Waislamu wenye elimu ya kutosha. Na wawe na uwezo wa kuhukumu kama jaji yeyote hapa Kenya. Na wawe na sauti, na wawe watatoa hukumu kutoka mara ama kurhani. Hususa ambaye ana uradhi na mengineyo.

La pili, ningependelea mambo ya Serikali, department zote za Serikali, especially, heads, kama chairmen wa Kanu, Wabunge, D.C, mkubwa wa polisi wa district, wawe ni born from the district, within the district. Mkubwa wa elimu, mambo kama hayo pia, department zote za Serikali katika district. Na kila district yake iwe na hivyo. Ufanyaji kazi wa kawaida katika D.C, kwa D.C ama ofisi ya elimu, ama ofisi nyingine kuwe ni mchanganyiko lakini kusiweko na application, nafasi za kazi, first privilege wawe ni wenye kutoka Lamu. Asitoke mtu, kama walivyosema wenzangu wengine, wachikue wengine nafasi ziko hapa, na wafanyaji kazi wako.

La tatu, ninaunga mkono majimbo.

Na la nne, ningependelea kumaliza... Ahsante sana mzee shukuran. Kama nina maelezo zaidi, nitawaandikia barua.

**Com. Hassan:** Ahsante Bwana Ahmed. Mzee tafadhali, Ahmed M. Omar.

**Ahmed Omar:** Salaam Aleykum warakhmatulahi wabarakatuu. Mengi yamezungumzwa na yamo kwenye makaratasi, lakini yale ambayo yametokwa kwa juu au kwa vipi, nitawaelezea. Kitu cha kwanza, tunaomba hii Katiba ya sasa, iturudishie mila zetu na



desturi zetu. Ma-tourist wanaokuja, akija na dola mia moja analeta maafa elfu moja. Mabangi, *ma-drugs*, mambo mabaya mabaya yote. Kuzunguka uchi katika ma-beach na (Inaudible), kwa hivyo Katiba itulindie zile haki zetu. Kwa sababu, visa na lawama nyingi zinatoka wanaambiwa viongozi wa dini wamenyamaza, na makosa si yetu. Asili tunaitaka lakini naye nyuki hatuna haja naye kutudunga mwiba.

Kitu kingine, kuna super power. Sisi hatuandiki, Katiba ipangike sawa sawa, iwe kama ni kitabu cha Mungu na

(Inaudible) lakini pia kuna super power. Super power walikuja hapa manwari ikaja tanda mji ikapita ma-helicopter ma nini, kisha kutuletea (Inaudible) sijui katika mji Somalia, na akitoka akisukumiwa bomu na atusukumie sisi. Yeye (Inaudible) kwake. Na hayo ni mambo aliyaamua mtu mmoja tu, na bila ya kufikiria wengine kwamba nao waulizwe, wakajibu. Kwa hivyo kusiwe kuna super power, kisha ikaja ikaguza hii mipango yote tunayoifanya.

Kisha nimewasikia wengi wakisema kwamba Rais apunguziwe mamlaka. Lakini mimi naona si kitu cha maana. Kitu cha maana ni Rais hakutudhuru sisi, wala hajajitokeza kwamba yeye ni adui yetu sisi. Lakini hawa walioko karibu na sisi, ambao hawakuwa mwongoni mwako, ma-D.C, ma-Chief, ma-D.O, ndio mambo mpaka na saa nne za usiku wanakwenda kuwapigisha watu faini za...

*End of side A.*

... nafikiria, lakini wala (Inaudible) kwa hivyo Katiba ya sasa iwafikirie watu wote sawa sawa. Lazima watu wote wawakilishwe. Na kitu kingine, mtu pengine anasingiziwa jambo, anashikwa bila kuwa na makosa. Akifika kule ndani ya court, akitaka kujitetea mwenyewe hawezi kujitetea. Ati mpaka kuwe na wakili ndio aweze kujitetea. Kosa nimelifanya mimi mwenyewe, nalijua mimi mwenyewe nikitaka kusema ukweli, niwache niseme ukweli ndio sheria ichunguze. Sio kwamba mimi mpaka niwe na wakili, ikiwa sina wakili siwezi kujitetea. Au mtu amechukuliwa na polisi aende aandikishwe statement za urongo, kortini apewe vikwazo vya adhabu, haya mambo, Serikali ifikirie, mapolisi wasije wakawadhulumu watu na court isije ikawadhulumu watu.

Kitu kingine ni ile mambo ya Lancaster House, na ya Chief Kadhi na vile vile mipangilio ya elimu. Tumeona hii system ya 8-4-4 hiyo haitufurahishi, imetufikisha mahala pabaya. Kwa hivyo tunaomba Katiba ijaribu kuzungumzia elimu ile ile iliyokuwako hapo nyuma. Vile vile sarafu ya nchi, sio mara ikabadilishwa ikaenda huyu ikaenda huyu. Aliyekuwa mwanzilishi wa nchi hii, yeye Mzee Kenyatta, irudi sarafu iwe kama ile ile, isibadilike huyu, ikibadilika huyu, isibadilike sarafu. Pia tunapendekeza katika mkoa wa Pwani, kuwekwe university, university zote ziko bara, na nafasi hatuzipati sisi. Kwa hivyo iwekwe Pwani, tuwachiwe nafasi sisi wenyewe watu wa Pwani.

Kitu kingine, madarasa za Kiislamu, Serikali twataka izingatie vile vile mahala pa kufundisha watoto tabia nzuri, na masomo mengineyo ambayo yanajenga katika (Inaudible). Lakini utakuta hata kama akipata shahada ya kutoka



university ya Kiislamu hawezi kupatiwa madaraka yoyote. Kama Serikali ya Zanzibar, mwalimu wa madrasa analipwa kama mwalimu wa shule ingine. Kwa hivyo na ili nao Serikali iwafikirie pia wao ni raia. Tofauti ya dini isitubague sisi.

Kitu kingine, utakuta kama barabara ile-- Leo kulitoka maafa hapa, kuna K.P.A. K.P.A ina kazi gani? Ukiingia meli ukijua, naenda kaisaka, itashika laki tano, laki sita, lakini leo kuzunguka ufuo wa bahari, hakuna K.P.A. iliyosimama, wala polisi waliosimama kwenye ukingo wa bahari, maiti ipate kesho, kesho kutwa.

### **(Clapping).**

Na kitu kingine, Rais wa nchi hii aliwahi kutangaza kuwa Kenya ni nchi ya Kikristo. Wanaoishi Kenya si Wakristo pekee yake. Wako dini mbali mbali, na percentage ya kila dini inajulikana. Waislamu hawako zaidi ya 35%, kufanywa kwamba wao ni wachache kwamba hawafanyi chochote, wala – mbona wakati wa kura wasiwatajije za wale? Kwa hivyo najua wanapoomba kura ni wale ambao wao walitupwa nyuma. Kwa hivyo, hili neno si zuri. Iwe Serikali ya Kenya hakuna kuangalia angalia dini wala nini. Kwa kuwa hii inafaa watu maana wakisema kwamba hii inatizama upande fulani, upande fulani haitizami. Hayo natumai yametosha. Asalaam Aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Shukrani.

**Com. Hassan:** Omar Makenzi.

**Omar Makenzi:** Salaam Aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Mimi ni chairman wa Coast Youth Group na ni Organizing Secretary wa D.P Lamu East. Ma-councillor tafadhali pendekezo letu twasema ma-councillor wasiwe na elimu ya zaidi ya standard seven or standard eight, kwa sababu wananchi katika nchi yetu ya Kenya, wachagua mtu atakayefaa, sio mwenye elimu. Vikwazo vya elimu, kuwekewa ma-councillors, haimaanishi kwamba itakuwa ni muhimu kwa raia. Bali raia wataka mtu ambaye ataweza kuwatumikia, na hatojali kuwatetea haki zao. Hilo jambo tafadhali mliweke mbele, na tuisikie kwamba ma-councillor wamewekewa ma-degree mpaka form six, form four. Hamutapata. Kuna sehemu nyingine ma-councillor hawakusoma, basi inaonekana kwamba hatutakuwa na ma-councillor.

Pendekezo lingine letu, chama chochote kinachotawala nchini, kisiwe na uwezo wa kufanya watakalo kinyume na sheria, ati kwa sababu wao ni watawali, na ni matajiri wa pesa, na hawalindi haki za binadamu, kwa sababu wao chama chao ndio watawali wa nchi hii, watatuonyesha unyonge. Kwa hivyo, utawala wa nchi usituonyeshe unyonge kwa sababu wao ndio watawali, twataka haki. Ikiwa uchaguzi utakuwa 2002, basi mabadiliko yanayohusika na uchaguzi yafanywe kwa haraka, ikiwa uchaguzi utakuwa ni 2002. Uchaguzi, mabadiliko ya uchaguzi, yawe yatafanywa kwa haraka. Mabadiliko ya uchaguzi sio haya tuliyonayo sisi kwa sasa. Haya ni ya unyonge na kuoneshana kwamba sisi ndio watawali, kwa hivyo sio mnavyotaka nyinyi watu wa upinzani. Twataka sisi watu wa KANU iwe na hivyo na inakuwa hivyo. Kwa hivyo pendekezo hilo lazima liwe, tupewe haki zetu, sio tuonyeshwe unyonge kwa sababu sisi si watawali, basi kwa hapa sisi tutafanya tutakalo. Tumeyaona mengi wakati wa 97, na mimi sasa nawaambia. Ikiwa ni Muislamu na ni raia wa nchi hii, kwa nini anapotaka identity card awe atasumbuliwa aambiwe lete documents hizi na hizi, kana kwamba yeye si Mkenya. Hiyo si haki, na lazima tuzungumze. Chama chetu

kimenituma haswa niwaambie. Kuna wengi wataka I.D, na wamewekewa vikwazo, kwa birth za nyanya na nyanya, na ambapo hawajui watazitoa wapi. Basi inaonekana kwamba wao wanajiona kwamba wao si binadamu, na hawana haki katika nchi hii, kwa vikwazo wanawekewa, lakini wengine hawaambiwi maneno hayo, wanaambiwa watu Waislamu pekee yao. Birth zinazotolewa kwa siku hizi, kwa nini ziwe zinaandikwa birth certificate is not proof of Kenyan citizenship, why? Watoto wetu wawekewe vikwazo namna hiyo? Inaonekana kwamba baadaye watakuja kupata shida.

Kwa upande wa polisi, mimi naomba polisi wawe watapewa mishahara mizuri, na allowance nzuri, ili ipungue kuhangaishwa kwa raia wasiokuwa na hatia. Wao wanahangaisha watu kwa sababu ya mishahara, na umasikini, na ambao wanajiona kana kwamba wao wanafanya kazi bila ya kupata msaada wowote ambao waweza kujitosheleza katika maisha yao. Kwa hivyo wanaona afadhali wafanye lolote, ambapo wakifanya na hufaulu. Lete shilingi mia mbili, mtu anapiga, lete shilingi mia tatu, lakini ikiwa watapewa mishahara mzuri, wakajilinda kisawa sawa kama wafanyikazi wengine, inaoneka uhalifu wa kuhangaishwa zaidi zitaondoka.

Mtu yeyote asiwe na uwezo wa kufanya atakalo nyuma ya haki za binadamu, ati kwa sababu Serikali iko nyuma yake ya kumtetea kwa lolote, na hiyo ni kinyume na haki za binadamu. Kwa sababu kuna viongozi wengine, wenye

(Inaudible) kwamba wao Serikali iko nyuma yao, nchi ni yao, kwa hivyo waweza kufanya jambo lolote mbele za umma, na wasijali kwamba hapa mimi nadhulumu, hapa mimi naharibu, kwa sababu yeye amejua kuwa Serikali iko nyuma yake. Kwa hivyo sisi twataka haki, na mtu asivunje sheria.

Chama chochote kinachotawala, hakina haki ya kufanya chochote walitakalo kinyume na sheria, wakati wa uchaguzi wowote unaokuja. Kwa sababu chama kinachotawala huwa kikifanya mambo ambayo ni kinyume na sheria. Mimi nilipigania kura 1997, mimi nilikuwa councillor wa Ford People, lakini mambo niliyoona mimi katika kituo ilikuwa ni kinyume na sheria. Nao walikuwa wakifanya ni watu hao hao watawala wa nchi hii, kwa kutoa pesa mbele ya kituo, wakituonyesha kwamba nyinyi hamuna nguvu, sisi ndio wenye nguvu. Wakiingiza watu kwa kutumia mabavu, na tukizungumza askari wako hapo hapo, tukicheza sisi watu wa upinzani twaonekana kama hatuna haki. Wenye haki ndio hao. Na ikiwa mambo yataendeza namna hiyo, hata uchaguzi afadhali tuondoshe sasa usiweko, ikiwa moja kwa moja wao wanaheshimiwa kwamba ndio Wanaume kushinda sisi.

Hukumu za kortini ziwe na sheria mpya. Kwa sababu makosa madogo madogo isiwalettee na faini kubwa kubwa zisiwalettee, wale ambao wamefanya makosa madogo madogo. Ni lazima Serikali ifikirie kitu kama hicho.

Ardhi zenye thamani, utakuta mara nyingi ardhi zetu hapa Lamu huvamiwa na watu wenye mapesa. Hata katika kugawanywa, utaona masikini, hapa tuna ma-Hamadi, hapa tuna wachunga punda, hapa tuna masikini wengi ambao nao walia. Waomba nao wapate mashamba, na wapate ardhi. Hawapewi kwa sababu ya unyonge wao, na umasikini wao. Lakini mgeni yeyote akitoka nje, akija hapa na pesa zake na kifua chake, ardhi yoyote aweza kuichukua, na mtu yeyote akanyamaza kimya, na wakubwa wote wanao husika, ma-D.C, ma-D.O, wote quiet, watanyamaza kimya kwa sababu wanaongozwa na mtu mmoja.

Jambo lingine ambalo mimi napendelea, ni kwa upande, - hata kama ni mimi ni councillor nimepitishwa, hata kama ni Wabunge, tafadhali twaomba ikiwa kiongozi yeyote amechaguliwa na umma na ameonekana huyu sasa hafai tena, tafadhali mwaka mmoja uwe ni mwingi. Atupiliwe mbali, na aangaliwe mwingine kwa haraka. Aangaliwe mtu mwingine kwa haraka, asiendelee kutuhangaisha, na kutumaliza, na kutumiminya na kutumaliza nafsi zetu. Akionekana hafai, moja kwa moja aondolewe.

Jambo la mwisho, naomba Katiba kama hii iwe italinda ardhi zetu, italinda haki zetu, isiwe ni kama mfano wa mambo mengine yaliyopita. Kama mimi hapa, ingawa nimekuja, lakini watu wa D.P waniambia wewe wapoteza time yako tu. Wewe hata haujui wazungumza nini? Katiba ya zamani na hatujui, wewe utakuwa ukitaja nini? Nawaambia wacheni twende na tutaandika maombi yetu na tutaangalia. Kwa hivyo mtusaidie kitu, ambacho chatuumiza sisi hapa Lamu, ni matajiri wanaojigamba kwamba wao wana uwezo kwa Serikali, kwa hivyo wafanya vile wanavyotaka wao. Hata katika uchaguzi, sisi tukisema twamtaka huyu, lakini Serikali ikisema yataka huyu, kwa hivyo ni huyu, sio yule ambao wanamtaka raia. Asalaam Aleykum.

**Com. Hassan:** Ali, ...

(Inaudible). Mohamed Abdulkadir, Ufungamano, hayuko? Haya, Ali Mohamed

Salim.

**Ali Mohamed Salim:** Waheshimiwa wageni wa Constitutional reform, mabibi na mabwana. Mimi nimesimama hapa lakini siwezi kusema najitambua kwamba ni mtu nimezaliwa Kenya, na nina haki kamili kama mwanakenya. Sijui kulingana na tarehe yangu nilipozaliwa katika 1940s, nilijikuta mimi sijui nimetawaliwa na nani. Kwa sababu nilikuwa nikikuta bendera moja nyekundu lapepea la Sultani, moja ya Union Jack ya Mwingereza. Nikawa namwambia baba yangu, “hizi maana yake ni nini? Kwa nini hatuchukui tukatia kwenye jahazi yetu?” kwa sababu nilikuwa sijui alinitawala ni Sultani kutoka Zanzibar, au ni mwakilishi wa King George, - the late King George. Nikakaa nikaona kuwa 1950, kukajengwa skuli ya kwanza kwetu, ilikuwa hakuna skuli. Babangu akanipeleka skuli ya Lamu, ndio ilikuwa skuli pekee yake ikiitwa Lamu Prime Arab Primary school. Akaulizwa personal (Inaudible) politics yake, ili iweze kuwekwa hapo, kwa sababu alipoenda Zanzibar, akaona skuli ni zina haramu kumbe (Inaudible) Islamu. Aliponieleza akaambiwa toa

(Inaudible) asipotoa akaambiwa “wewe umeandika African Bajuni, kwa hivyo hufai.” Nikarudi wakaenda wakafanya mipango na mzee mmoja wakaanzisha skuli, tukaomba kwa D.C, tulikuwa na pesa za kuchezea ngoma, tukatoa kujengea skuli watu walisema nini. Hiyo ilikuwa ni bahati mbaya, mimi kusoma ilikuwa ni bahati mbaya. Kwa sababu, Wazungu wasema “ to know what is the problem,” - pengine ndio imenifanya mimi nikawa mzee haraka. Kwa sababu nilianza kujua haki zangu. Mimi niliposimama hapa, kuna nyumba inaweza kufika miaka mia -saba-, mpaka sasa nyumba hiyo mimi ni squatter. Sijui kama kuna mtu huku Lamu ni original and indigenous person in this Republic of Kenya today. Nikisomeshwa skuli twaambiwa twataka Protectorate, nikitoka nje kuenda kuangalia land registry naambiwa “you are under the Colony.” You are under the Protectorate, huku naambiwa wewe una (Inaudible) na Sultan. Ndio ana ku-protect. Ajabu, na ajabu na ajabu, mimi mamangu ni ardhi, mimi aliyenizaa ni ardhi.

**Com. Hassan:** Bwana Ali Mohamed, tunakuomba tafadhali utoe mapendekezo yako.

**Ali Mohamed:** Mapendekezo yangu ni kwamba, mpaka sasa mimi sina haki ya ardhi ambayo nakaa, nalala, napata usingizi, na ardhi hii ndio mamangu, na ndio itatupatia chakula, na ndio tamaa ya maisha yangu, kwa vizazi vyangu nilivyovizaa. Leo twasikia vita vyapiganwa duniani (Inaudible) kwa sababu ya ardhi. Je ardhi yangu kama leo itachukuliwa juu ya shauriwa ati 'a good cake for a good boy,' where am I going to keep my children when I am dead? Kwa hivyo hii ni time bomb. "Be planned in future." Where? Sijui watoto wangu watatupwa wapi mimi? Sijui mimi nitatupwa wapi? Am I going to be buried on somebody' land? -Who is not known even to me. While nina haki ya kupiga kura katika Katiba, when I don't have even a piece of land after all these years. Kwa hivyo Katiba ya Kenya imenisaidia mimi nini? Watu walipokwenda katika Constitutional Conference Lancaster House, tuliambiwa " mutapewa ardhi zenu." The issue of the independence for Kenya started from Land. Nikakuta nchi yangu, mimi nimeandikwa Bajuni land is tribal land. Hivi leo, baada ya kupata uhuru, *ika-reverse*. Tumepata ni state land. Ili watu wapate kuja kunyakua ardhi katika nchi yangu niliyojaliwa. Sasa mtu kutoka nchi nyingine aweza kuja akawa na land in Kenya, mimi sina. Kwa hivyo, tunajiwaza vizazi fulani Katiba haikutulinda, - iliyopita kuhusu ardhi yetu. Sasa ni kuanza upya kwa sababu, huwa ni state land, Muingereza aliwacha Bajuni Land as a tribal land. Kwa hivyo, tuseme stage hii tutaichukua sisi, na sisi wenyewe tupewe. Constitution mpya ya Kenya, wewe when you are buying land order, ingechukua papers za state land, so that it will be open to everybody. Sasa lazima tupange...

**Com. Hassan:** You have made your point. So go to the next point now.

**Ali Mohamed:** Kwa hivyo ningepomba Katiba hii itakavyokuwa, iwe ni active and alive Katiba. Inipe mimi haki, so that I become proud of my country. Isiwe ni kitoto ya sanamu unaambiwa yuko yule, lakini likipigwa, yeye hawezi kushika panga kujisaidia. Thank you very much.

**Com. Hassan:** Thank you very much. Ali, mzee ukimaliza kuongea tafadhali unatupigia signature kwa register. Sasa naweza kumwita Hussein Soud. Bwana Hussein Soud...

**Hussein Soud:** Jambo la kwanza, nataka kufanya maombi kidogo, mapendekezo ambayo nitayatoa hapa, ni mapendekezo ambayo yameshirikisha kuchukua maoni kwa watu wengi katika Lamu. Lakini mbinu tulioichagua, ni mbinu ambayo tulitengeneza kamati, mapema tuliposikia kuna mpango wa kutengeneza Katiba, kutoka 98. Kutoka katika dakika hiyo mpaka leo hatujakaa kitako, tulikuwa tunakusanya maoni. Kwa hivyo maoni haya kijumla ni ya wengi. Siwezi kusema ni ya wote, lakini ni ya wengi. Katiba tulipopanga sisi, tulitumia mbinu, tukaitazama ile Katiba ya sasa iliyoko katika Kenya, na tukachagua, yaani tunaweza kuwaita scholars, intellectuals, katika area mbali ya vifungu vya Katiba. Wengine walikuwa wana experience, ya kufanya kazi katika mambo mbali mbali, tukaona hawa, bila shaka waweza kuchangia sana. Sasa kwa hivyo kwa ufupi, katika atakayekuja kuzungumza hapa, ni watu wawili. Ni mimi mmoja ninazungumza, ambaye nitazungumza juu ya Kadhi's court, law of succession, Wakfu Commission, land issue, education, and the Coastal strip agreement. Na mwingine yuataka kubaki,

mmoja alikuja hapa akanieleza mwenye walinisaidia pia akachukua moja akanieleza habari ya mambo ya kuhusiana na Antics katika habari za (Inaudible). Nimekwisha kuzungumza na mwingine, atakuwa ni mmoja wetu, baada yake natumai ikuwa vizuri...

**Com. Hassan:** Mzee kama ungeenda kwa mapendekezo tafadhali.

**Hussein Soud:** Ndio, ni muhimu kwa sababu katika pale kutaja waliochangia, ni kuisema pasi na kutaja majina, twaswema nilikwenda pale, nilifanya haya na nayatoa yote ni yangu. Ni lazima niwape heshima waliochangia. Kwa hivyo, hiyo voluntary Constitution review ilikuwa ni member, tukiwa na Ahmed Abdhurahiman Chairman, mimi mwenyewe Hussein Soud vice Chairman, kisha tuna Said Abdalla Khamisi ni Secretary, kisha ambaye pia ni member Omar Asman Maya, Ahmed Said Baguba, Abubakar Mohamad Lamudi, -Aboud of Agriculture, Mohamad Amana, Mohamad Abdulahi -the present Kadhi of Lamu, Shariff Jawadh- ex-Kadhi, Sheikh Mohamad Sheikh – ex-Kadhi, mwalimu Mohamad Ali Badi, Omar Mohamed Famau, Mohamed Mubarak Shaban, Famau Fumo, Sheikh L. AbdurKadhi Mohamad, Omar Mohamad Wela, Nassir Bwanamkuu, Sheikh Kale, na Kibwana Sheikh. These twenty people formed that particular committee.

Now I have also made a summary because the memorandum consists of about thirty five pages which I will hand to you, but quickly, if you will allow me, in spite of the fact that, I would have to speak in Kiswahili, so that everybody will understand. But because I am covering a big area, I will actually need the summary. It is not all that is there, and mind you, if each one of these people would come and speak on their paper, if every one of these were given five minutes, that will be twenty times five, how many minutes? One hour and twenty minutes. So if I take half an hour, there should be no reason for you to tell me stop.

**Com. Hassan:** No, you have ten minutes. Please try and summarize up all your points in ten minutes.

**Hussein Soud:** Right. Now, I go straight on in English, without translating. Because that will be a double job.

**Com. Hassan:** No, you don't have to do it in Kiswahili and English, because these hearings are meant for us but not the public.

**Hussein Soud:** Very good. Now, we begin with Kadhi's court. And why? I have not told you I am highlighting certain things, I am going over every point. Because about the Kadhi court, many people have already spoken. I want this one so that there will be a difference. Now, according to section 66, of chapter four of Kenya Constitution, the current one, it says like this; There should be a Chief Kadhi, there should be not less than three of other Kadhis, they all must be Muslims, Number four, knowledgeable of the Muslim law to any sect of Muslim, in the opinion of the Judicial service Commission, to hold a Kadhi's court. Their Jurisdiction within the former is protected.

Number six, will deal with Muslim Law, pertaining to personal status. Marriage divorce and inheritance. This is all that there is

currently in the present Kenya Constitution . Not more than quarter of a page, concerning the jurisdiction of Kadhi's court. Now, basing on that section, we had gone through, and we had found that there is a necessity of making the following suggestions. The following additions should be enacted, in addition to the old and the existing one.

1. The Kadhi to hear civic cases, and even some criminal laws pertaining to marriage and divorces that concern the Muslims.
2. Status of the Kadhi court be raised to a second-class magistrate.
3. Kadhi to have the power of calling witnesses, even non- Muslim witnesses to give evidence for a citizen in allegations between Muslims.
4. Kadhi to have power, to attach the property or salary of the Muslim litigant if the said property or salary is in the hand of a Non- Muslim.
5. Kadhi's qualification, He should be a Muslim scholar, pass in Islamic religion, at least be B.A or L.L.B in Islamic law, or its equivalent.
6. There should be an assistant Chief Kadhi.
7. There should be a senior Kadhi.
8. And then, the section 66 2A, and 66 2B Constitution of Kenya, and in ( Inaudible) combined by section of Kadhi's Act, to keep justice; we recommend the following to be included: The opinion of the Committee of highly learned Muslim scholars, when discussing about matters that concern the Muslims.
9. The retirement age be raised from 55 years to 65 years.
10. All current Kadhi grade two, should be interviewed by the above proposed Committee of Muslim scholars, that is ' Ulama.' If one fails twice he should be terminated.
11. English should not be a barrier to appointment to Kadhi's status, provided he has a thorough knowledge of Muslim Law.
12. Kadhi's court should be extended to exercise jurisdiction in the proceeding following chapters of the law of Kenya, as they are directly related to the jurisdiction of the same.
13. Chapter 55, which is the men and Mohammed and marriage divorce, legislation Act,
14. Chapter 156, Mohamed and marriage divorce and succession Act. (c) Chapter 109 Wakfu Commission, and number (d) Chapter on public trustees.

And finally, the chapters that discuss about children and young persons Act. All the Muslim children, that fall under a problem because of the divorce, or any conflicts that there have been between a husband and a wife, and the children maybe they might have been abandoned, before instead of it being taken to the child office, it should come under the jurisdiction of the Kadhi, to decide all that matter pertaining to Muslim children, infants and those ones who have been abandoned by their parents. So that therefore, the details of which is in the memorandum. So that is as far as the Kadhi's Court is Concerned.

Now, the next one is the law of Kenya, concerning the Wakfu Commission Act, chapter 109. This Act was enacted in 1951, set up a board of work Commissioners, with the following responsibilities: looking after Mosques, graveyards and family welfare.

The board consists of the following persons. P.C, of course Ex-Officio, Chief Kadhi Ex- Officio, one Muslim appointed by the ministers to be nominated by the P.C of Coast, five members appointed by the ministers from a panel of names submitted by the P.C courts after taking the opinion of the Muslims.

Now, shortfalls, of the board:

1. None of the descendants of Muslim donors is represented.
2. No balance sheets are written for the Muslims or those concerned with the work to know.
3. The activities of the board are not known by other Muslims.

Now, suggestions and recommendation.

- a) Wakfu Commission Act to be reviewed to protect the property entrusted to it.
- b) To establish district advisory Committee, to include representatives of the original donors of the Wakfu.

The function, -these proposed advisory Committees, the functions of the District advisory Committee:

- 1) To advise the Commission on issues relating to their district.
- 2) Prizing of Wakfu property. Why have I said here? Prizing of Wakfu property. We know, some of the property belonging to the Wakfu. For example, if I had a house that I would fight to rent it at ten thousand shillings a month, there are similar types of houses that the Wakfu Commissioners are renting at SH.100. Would somebody actually, - if that was his own house do that? So, because of this we have said the purpose of this District Advisory Committee, is to look to such things.
- 3) The Chief Kadhi to appoint eight Muslim Scholars 'Ulama,' knowledgeable of the Islamic law to be members of the board. But you know, first, before I mentioned this, I mention what was already current to compare the two. I think you get that particular purpose.

Now I come to another issue, which is land issue in Lamu.

**Com. Hassan:** Your ten minutes is up please try and summarize your points now.

**Hussein Soud:** I am taking the place of twenty people. Land issue in Lamu. Land in Lamu in most places, particularly on the Lamu island, is G.L –Government Land. This has led to many ills, such as grabbing of the land by politicians, councillors,



Government officers, influential people, and some ordinary people who manage to get it but fail to develop it because of poverty, and also get – and Government settling, non indigenous people. The example of which Mpeketoni speaks for itself. My recommendation is,

- 1) The all ready title deeds issued to the indigenous, obtained legally be recognized and sanctified owners.
- 2) If the above is to be taken away, the owner should be compensated. If the owner is an individual, or the land belongs to a group of the Community.
- 3) Law should be enacted that only allows the indigenous to acquire land in their home districts.
- 4) Land in Lamu district, should be trust land, or Communal land, so that each place, and the right of Lamu will be paramount and fully protected. The method how we should go about it, is written in the memorandum.
- 5) When land is adjudicated, an issue of ownership document elders from locational, zonal district, should be incorporated, so that justice is done in the land allocation. On education, it is proposed by this selected Committee, that B.O.G. in secondary schools be scrapped. In place P.T.A be given mandate to manage the school. The details are given in the memorandum you can look, but I am just highlighting. P.T.A. are incited by parents. B.O.G. does not respect it and they are not the beneficiaries to the education given these schools.
- 6) P.T.A are partners in the schools in providing the financial support.
- 7) P.T.A. are in better position to promote standard and quality education compared to B.O.G.

Finally, to make complete what we have written, and whatever I might have left because here I had summarized, our memorandum's contents Kadhi's court issue, law of succession, where on the law of succession I had summarized by saying that as far as law of succession is concerned, you will remember in the 1970s, there was a national protest when the Government wanted to change the law of succession. The reason is, the law of succession is theocratic. And Muslims can never touch it. And nobody can touch it because amending it or changing a dot to fit is Tantamount to committing a grievous sin against the Creator Himself, and the Muslims will never allow that one. We know as Muslims, inspite of the

(Inaudible) time people talk about equality, that if a boy gets ten shillings inheritance, the girl should also get ten shillings inheritance. There are reasons, which I have given in that memorandum, which cannot allow that to happen. Because the responsibilities of a husband far much outweigh the responsibilities of a wife. Because whatever the wife has is her property. But, the property of the husband is not only his. He has to feed the wife, he has to look after children, and all members of the family, but whatever the...

**Interjection. Com Hassan:** That is fine. Just summarize your points please now. You have taken too much.

**Hussein Soud:** It is not too much.

**Com. Hassan:** I have given you respect because of your age. ... (Inaudible).

**Hussein Soud:** I am finishing. Just one more minute, and not more than that. I am just finishing that one. So, in this one,



what we have in the memorandum, because I had forgotten to talk about the Law of succession, that is why I had to count them. But in this memorandum there is Kadhi's court giving details, Law of succession, Wakfu Commission, Protection of fundamental rights, and freedom of individuals, which will be given by Maalim Badi, and then Land issue, and matter on museums has already been discussed, P.T.A., board of governors, Kenyan Coastal strip agreement, which I have also included in here. And this- what is in that Coastal strip Agreement between the first President and the Prime Minister 'Shamte' should be adopted. If you look into it very closely, many things would have been Okay now, but because that was ignored, we are today suffering.

Finally, there is also a recommendation brought and included in this handout, which I am giving out from the Chairman of Islam, Islamia Mr. Mohamed Amana who has not been able to come today. Thank you very much.

**Com. Hassan:** Thank you very much. Thank you mzee just sign for us register. Did you sign the document? Mahamad Silaha, ... (Inaudible) Mzee Aboud... Sheikh M. Salim Baaga, hayuko. Awadh Nassir hayuko.

Councillor Abdul Issa Twalib. ... (Inaudible).

**Abdul Issa Twalib:** Asalaam Aleykum Warakhmatulahi wabarakatu. Mimi sina mengi, kwa sababu mengi yamezungumzwa na (Inaudible) maoni yangu. Bwana ... (Pause) haya, bwana Chairman, maoni yangu ni haya yafuatayo: moja ni kuhusu mambo ya gender, gender equality. Sisi tuna wasi wasi sana ikiwa kuhusu mambo ya gender, utasikia kuwa kila mahali kwenye vipindi, kwenye Daruban huku, kwa sababu haki ya mwanamume na haki ya mwanamke iwe sawa sawa. Kwetu sisi nafikiri itakuwa si kitu cha busara. Kwa sababu itakuwa imeingilia mpaka kwenye Kuran ikatufikia aya zetu za Kuran. Sisi hatu (Inaudible) wanawake wawe na adhifa nzuri, vyeo vikubwa vya Serikali, au katika kujenga nchi na kadhalika. Lakini isiwe na power fulani aina moja, kama tuseme kama inheritance yule apate sawa na yule apate sawa, au katika mambo mengine yataingilia mpaka yataharibu mambo ya miola na dini itakuwa ni kitu ambacho, - Uislamu utakuwa hauko considered. Kwa sababu itaenda mambo mengi sana, italeta vurugu huko mbeleni. Na hilo moja ndio langu kubwa ambalo, hawa outsiders, foreigners hutilia nguvu sana hii mambo ya gender equality, ichukulike. Maoni yangu ni kuwa sisi ile ....

**Com. Hassan:** Councillor Abdul, are you talking for yourself personally or as (Inaudible)?

**Cllr Abdul:** Jahara. Ichukuliwe kuwa kila dini iwe na interest yake. Ichukuliwe na interest kulingana na –considering their faithfulness-, ichunguliwe

Ya pili, ni kuhusu mambo ya Kadhi. Kadhi ilizungumzwa lakini kwa ufupi tu ni kuwa, ni kitu kidogo tu kurekebisha. Kwa sababu twataka Chief Kadhi awe na same powers like of the Chief Magistrate. Power zao ziwe sawa sawa. Isiwe kuwa Kadhi ameamua kesi kisha ipelekwe tena kwa magistrate. ... ni yeye kuwa apewe nguvu moja, akimaliza iwe final. Isiende

tena huku, Kadhi ameamua kesi kama ma- judges. The same case ambayo judges wameamua

(Inaudible) Kiislamu haiishi dini ya Kiislamu, haiishi mambo yetu na mioyo yetu ya utamaduni za Kiislamu,

(Inaudible), sana sana huwa hupata failure nyingi. Huwa haturidhiki na uamuzi ambao wameamuliwa kule. Kwa sababu sasa itakuwa ameniangalia Qurani, ameanalia na hadithi, ameanalia na mambo mengi mbeleni, conscience na nini kuwa aliamua ile kesi. ile (Inaudible) iamuliwe na mtu ambaye hata haimuhusu, unapata hapo udongo, sasa nataka wapewe same powers, Chief magistrate na Chief Kadhi.

Lingine, hili kidogo nataka tulisikize kwa makini sana. Kwa sababu ni kitu ambacho hututia dhiki sana. Kwa sababu katika Kenya, -kama vile tulifahamishwa, kuna makabila madogo madogo, na makabila makubwa makubwa-. Lakini makabila makubwa makubwa sana huwa wa (Inaudible) wako huru in their areas. Tuseme kama district level, Provincial level, divisional level, huwa (Inaudible) wako huru. Sasa wanafanye ile, wana- move. Wanafanya migration. Wana-move kuenda kwa small tribes, ambao pengine availability za ile mambo ya ardhi ambayo yanazo zile makabila ndogo ndogo, (Inaudible) bado hazija, - nafikiri mwanifahamu hapo, bado hazija achiliwa kwa ile mambo, (Inaudible) kupata ile document ownership. Sasa, haya mambo ya kisiasa, Bunge la upinzani huwa ikilete kidogo problems. Hapa nataka kabila lolote ambalo lita-move from one place to another, au mtu yeyote akienda mahali papya, awe yeye hana haki: moja, kuchukua ardhi pale mahali, ikiwa sub-location iende kila mmoja apewe kwao. Kila mmoja apewe kwao. Kwa sababu ikiwa yeye atapewa hapa, na vizazi vitakavyo kuja ni hapo hapo, sasa utaona hapo italeta problem. Kwa sababu huku pahali sisi wenyewe hatutoshi na kule waleta kitu yao. Ukienda mahali kwao, huwezi kupata chochote. Kwa sababu huku land zote ni za wenyewe. Kwa sababu ni kwenda kila kitu, Communal kila kitu ni ukabila. Na sisi huku we don't want to be influenced. To be controlled, may be by the outsiders. Kila mmoja hataki awe controlled by the outsiders. Na kila mmoja kwao pia wengine hivyo hivyo. Na wengine wote namna hiyo. Kila mmoja ajue interest zake zisibadilike. Kwa sababu hiyo itakuwa kama vile wenzetu wamesema huko nyuma, italeta maadhura mbeleni.

Na pia mambo ya Police Guard. Police guard issues pia mambo ya interest etc yawe the same case. Kwa sababu nataka kutoa mfano mmoja. Tuseme kama Mombasa, utaona kuna watu wa Mvita, kuna watu wa huku, utaona, sasa na kabila nyingine ambazo zatoka bara, zimeingia tuseme Mombasa. Utaona mara ya kwanza, katika viti thelathini utaongeza kiti kimoja (Inaudible) kumpata mtu kutoka nje. After another five years ikuwe tena amepata outsiders. Maybe it will come to a time, pengine itakuwa ni fifty-fifty sasa. Fifty-fifty. Sasa itakuwa ile interest of the local people, the indigenous, they want to trade. Sisi twafahamu ni kwa sababu wao wataiamulia kulingana na interest zao, wataamua, -kwa sababu wao they don't represent their people there. They represent different people, - they don't have sympathy. Utaona sasa katika uamuzi wao, utoke kwenye full council, committees meetings, watakuwa wakipitisha kulingana na interests, kulingana na watu ambao wale watakuwa na (Inaudible). Sasa at the same time sisi tutakuwa tunaumia zaidi. Na kwa police guard interests pia, yataka iangaliwe kwa sababu (Inaudible) time, hapa, kama hapa mutaona kwenye makosa, sijui kama mshafahamu?

**Com. Hassan:** Tumeifahamu hiyo point.

**Clr. Abdul:** Mumeifahamu? Basi sina mengi ni hayo tu. Mmefahamu na mufahamu.

**Com. Hassan:** Ahsante. Bwana Councillor tafadhali piga signature kwa register. Sasa tunamtaka Ali Ahmed Rali.

**Audience:** Hayuko.

**Com. Hassan:** Amukami Harun... Mohamed Ali Badi...

**Mohamed Ali Badi:** Thank you mabwana Commissioners. Mimi nataka kuzungumza mawili au matatu, ambayo yanatuletea shida kama balaa. Mengi yamezungumzwa na wenzangu, na ninashukuru kwa ile (Inaudible). Bwana makamishena, tatizo liliyoko ni kwamba, Katiba haipewi ile jukumu lake, au hekima yake inayostahili. Yaani, Katiba siku zote yatungwa na watu, ambao ndio sisi wanakenya wote, wake kwa waume. Lakini ikishaandikwa ile Katiba, ile supremacy yake haipewi heshima, hilo ndilo tatizo la kwanza. Kwa hivyo naomba Commission hii ifikirie kwamba mtungaji Katiba, mtoaji ruhusa ya kuundwa Nation, mtoaji ruhusa ya kuwekwa Government, ni mwananchi. Baada ya kila miaka mitano. Kisha, mwananchi huyo huyo anawekwa chini, wale wanawachagua wanawekwa chini, irrespective of the supremacy of the Katiba. Kwa hivyo tunaomba la kwanza ipewe supremacy yake inayostahili.

La pili, matatizo yanayopelekea mpaka Kenya ikiwa haitawaliki, kutoka 1963, mpaka kufikia 91, mpaka leo kuwa haitawaliki, ni hizi amendments. Unilateral and arbitrary amendments. Yaani kubadilisha Katiba bila ya mazingatio na makubaliano ya watu wenyewe, pindi ya mwananchi mwenyewe. Hii ndio ilileta matatizo makubwa. Yaani Serikali, baada ya kuibadilisha Katiba ya kwanza ya Lancaster House 1963, ambayo niliona ni nzuri sana, -na mimi for your information bwana Commissioners, kwa niaba ya kikundi changu cha Watanye, naunga mkono federalism, mfano wa Nigeria-. Kwa hivyo wakaweza kutumia vipengele viwili, na hapa nataka msikie vizuri bwana ndugu zangu makamishena. Kipengele cha kwanza ni section 3 ya Katiba, ambayo ilibadilishwa 1966. Section 3, moja kwa moja ikaambatishwa na section 47, hizi mbili ndio walitumia kupitisha mabavu yao, na kufanya amendment kivyao, kulingana na masilahi yao, kinyume cha mahitaji ya wananchi, na makubaliano ya Katiba iliyotungwa na wananchi wote. Kwa hivyo naomba Katiba hii ya sasa, irudishie haki amendment, kwanza katika under federal system, naomba ziwekwe two chamber system, yaani iweko house of representatives, Jumba, baraza la wa (Inaudible) na baraza la wazee, ambao ni senate. Sio baraza la wale kina mwalimu Hussein, Senate. Katika ndani ya senate hizi nyumba mbili za kutunga sheria, ikiwa itafanyika mabadiliko yoyote ya kisheria iwe inapewa ruhusa ya almost, - maybe kulingana na maoni yangu, 75% to 80%, ili waweze kufanya mabadiliko-. Ikiwa imeshindika, pia together with that, ile mabadiliko makubwa makubwa, yarudishiwe kwa mpango wa referendum kwa wananchi wenyewe. Kwa hivyo hivi vifungu viwili muviangalie vizuri, section 3 na section 47.

nafikiri hapo tutakuwa tumerahisisha mambo mengi.

La mwisho ni – sitaki kupoteza wakati, kwa niaba ya kikundi changu cha Watanye, ambayo presentation yao ni hii, tulikuwa tunatoa nasaha kwa mipango hii ya Review Commission, ifikirie hii maswala ya marginalized minorities ambayo mimi nimeongezea na kifungu cha U.N., endangered human species. Kwa mfano, la Katiba hii, -hiki kikundi changu cha Watanye, sisi Watanye, ndugu zangu makamishena, ni karibu watu mia tano tu. Na tumemezwa na makabila mapya yaliyoko hapa ndani yetu 1974, tumemezwa na hawa hatuna tena ardhi. Sisi tumebakia watu mia tano na ardhi hakuna. Kwa hivyo zile interests zetu na rights zetu kama minority ziwe protected under this new Constitution haswa sisi Watanye. Hatuna ardhi, hatuna- our cultural rights have been eroded and swallowed up, our economic rights have been swallowed up. Kwa hivyo naomba hizi zote ambazo zime katika hii representation mutuangalie vizuri. Na kwa ufupi, Lamu district nzima is consisting of minority groups. Thank you.

**Com. Hassan :** Thank you very much. Sign hapo. Ahmed Shekh Hadi...

**Ahmed Sheikh Hadi:** Jina langu ni Ahmed Sheikh Hadi. Mimi ningependa kutoa maoni kwenye hii Katiba mpya. Kwa hakika ni kitu kizuri sana. Na maoni yangu ningependa total independence. Tuwe na Serikali iwe totally independent, sio leo kuwe kutakuwa sheria ya wazee, sheria ya nani, kuwe watu wote watapata sheria sawa sawa. Kwa mfano kama South Africa, kama America ama other places. Basi, ndio langu hilo.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Bwana Ahmed Sheikh Hadi, sasa tunamtaka mzee Omar T. Mzee... ni wewe?

**Omar T. Mzee:** Mimi, bwana chairman, maoni yangu nitakayo kutoa ni maoni yangu binafsi, ni machache sana, na wala sijaindika kwa maandishi. Maoni yangu ni kwamba, pengine mtu mwingine ametaja habari ya supremacy Constitution. Naona tatizo kubwa lililoko, ni kwamba kwa muda mrefu sasa katika Kenya, kumetoka laws, - kuna laws. Mbali na Constitution kuna laws na regulations, ambazo zatakikana ziwe included kwa ile Constitution . Hizi laws na regulations zatakikana zifanywe ziangalie masilahi au matakwa ya Constitution . Lakini tatizo liliyoko ni kwamba kumekuwa, kumetoka most of the Acts of Parliament, zina section nyingi za sheria katika Act of Parliament. Na kuna regulations chungu nzima zinatoka kila siku ambazo zote zina infringe, zinakanyaga ile Constitution . Sasa ndio ukaona bwana Chairman, kwamba leo baada ya sisi kuzungumza maswala ya kufanya review ya Constitution , ukweli ni kwamba tunafanya review ya sheria ya Katiba. Nyingi zinazungumza kwa mfano, maanake nitoe mfano kidogo ili kwamba, kwa mfano kama tulizungumza juu ya inheritance, matatizo ya miradi na mambo kama hayo. Mambo hayo Katiba ya Kenya yasema kwamba kila Mkenyaatakuwa na haki ya uamuzi. Sasa ikiwa sisi twataka kubadilisha sijui gani katika Katiba itabadilishwa. Lakini tatizo ni kwamba mbali na kwamba Katiba yasema kwamba, kila Mkenyaatakuwa na haki ya kuabudu, kisha kuna sheria zingine ambazo ni Acts, zile Acts of Parliament, na regulations za ambazo sasa ndio zinavuruga ile haki ya kuabudu kiasi ambayo kwa Constitution, sasa inaonekana mbaya, na hali kwamba kifungu hiko kiko cleared kwamba kila Mkenyaana haki ya

kuabudu.

Mfano mwingine ambao ningependa nitoe, ni kwa matatizo kama haya ya mambo ya passport. Kutoka asubuhi kila mtu amezungumza mambo mengi, kusema habari za passport, habari za passport, habari za passport. Katika Katiba ni kwamba passport, au kitambulisho, ni kwamba kila Mkenyaana haki ya kuwa na passport ya Kenya. Kila Mkenyaana haki ya kuwa na kitambulisho cha Kenya. Lakini, regulation ya mtu mmoja tu (Inaudible) na ni immigration officer. Atoa regulations elfu za kusema hivi, na hivi na hivi yatakikana katika certificate ya mjomba ya babu na nyanya na nani na nani, kiasi ya kwamba sasa ile Katiba imekuwa sasa imetupwa, ile Katiba imekanyagwa na ile sheria ambayo imetolewa na mtu mmoja tu ambaye ni officer wa immigration. Au...

**Com. Hassan:** Usiyarudie yale maneno ambayo tumesikia leo asubuhi. Tafadhali toa mapendekezo yako.

**Omar Mzee:** Mapendekezo yangu? Pendekezo langu la kwanza, ni kwamba ikiwa hakuna kifungo katika Constitution , cha kusema kwamba kusitokee sheria yoyote, be it a law or an Act of Parliament, or be it a regulation, ambayo ita-infringe yale matakwa ya Constitution iwe ikiwa (Inaudible) iwekwe katika Constitution mpya, na ikiwa mbeleni ilikuwa na Constitution vizuri, sasa iwe italindwa. Hilo ndilo pendekezo langu la kwanza.

Pendekezo langu la pili ni kwamba local authority. Constitution sasa hivi inavyo- provide ni kwamba mambo yote yanayo endeshwa au yaliyopitishwa na local authorities, mpaka kila kitu kipate consent ya minister. Mimi ningependekeza kwamba kile kifungo cha kwamba local authorities ikipitisha mambo yao, kusiwe na kifungo cha kwamba mpaka kupatikane consent ya minister. Ikiwa local authority imekaa chini, ma-councillor na kila mtu katika their level, wamepitisha jambo leo kusema hawataki miraa ije hapa Lamu kusiwe kwamba ni dharura mpaka (Inaudible) itie saina. If we are autonomous, wapatiwe hiyo autonomy. Kwa hayo machache nashukuru.

**Com. Hassan:** Ahsante sana. Come back. Please rudi utupigie signature. Mukimaliza kuongea tafadhali mutupigie sahihi register, ndio tupate kuwa na register hapo. Bwana Ali A. Maawiya... hayuko. Abdalla Shahazi... Hayuko. Abubakar M. Twalib... hayuko. Haya, Azra Mahmoud...

**Azra Mahmoud:** Asalaam aleykum warakhmatulahi wabarakatu. I am a student in form two, Alliance Girls High school. And these are my individual views. I would like the new Constitution to consider the implementation of freedom of worship in schools. In most national schools, Muslims do not wear hijab, the right form of hijab. They are not allowed to do so. And also, they are forced to do subjects which they are not interested in. for example C.R.E. to learn other religions.

My second, is that the percentage of students in National schools, should be proportional to the population of the districts of Kenya. For example in my school, they take, almost 90% of the students there are from Nairobi and that is making other

people around Kenya to lack the privileges that are found in that school.

I would also like that the Constitution should be taught in schools for familiarity so that the Constitution will be easy, because we cannot correct what we don't know. Okay, we don't know, most of us don't know what the former Constitution consists of, and I don't think we can correct what we don't know. Thank you.

**Com. Hassan:** Azra, please come and sign in the register. Ahmed S. Bajuba.

**Ahmed Bajuba:** Asalaam aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Mwanzo napongeza Tume kwa kuwa tayari, yaani kufika na kusikiza. Kwa niaba ya wakubwa wanao husika na Tume, twashukuru, wamefanya kazi mpaka sisi tuzungumze nao. Ahsante. Ni... kwanza naanza na drugs. Drugs ni tatizo kubwa katika Kenya, kwa hivyo twataka itolewe katika Sheria, punishment ambayo ni kali sana, ikiwa si pesa, basi iwe ni kifungu kikubwa sana. Na ikiwa ni Waziri, au ni Mbunge, au ni tajiri, mali yake iwe confiscated. Na ikiwa ni Mbunge, au ni Waziri, afutwe kazi. Au kazi yoyote ya Serikali afutwe kazi. Na mali yake moja kwa moja yataipishwe. Na corruption, kabla sijaingilia corruption, na mpango kama marungi, miraa au (Inaudible), iwe moja kwa moja, ikiwa by law itapita kulingana district concerned, inayohusika, moja kwa moja ikubalishwe kwa sababu ni raia wa sehemu ile hawataki. Moja kwa moja iwe accepted.

Nikirudia tena kusema ile mambo ya corruption, ambayo sasa imekuwa kubwa sana katika Kenya. Corruption ikiwa ni ngazi za chini mpaka ngazi za juu, za Serikali mtu yeyote atapatikana akiwa na corruption moja kwa moja awe sacked, afutwe na mali yake yoyote iwe confiscated, itaipishwe. Hiyo ni moja wapo itakuwa njia nzuri.

Kisha, kugusia maswala ya ardhi, Wazungu waliokuja Kenya, - tuna matatizo makubwa sana. Lazima iwekwe mipango maalum ya ardhi, namna ya vile ambayo kwamba wasinunue. Kwa hivi Lamu, baada ya miaka michache Lamu itakuwa kama Palestine Kwa sababu idadi kubwa ya nyumba za Lamu zimeuzwa na ardhi pamoja, kwa hivyo kuweko na kifungu maalum cha wale wanataka kununua ardhi katika Kenya. Sio kuwa wageni wanunue kiholela, itakuwa sehemu sasa wanaitenga kumbe ni ya wageni. Tutaendelea, zile ardhi zinazo chukuliwa, kwa njia ambayo si halali na ni controversial land, moja kwa moja ziwe revoked. Iwe kuna kifungu ziwe revoked moja kwa moja. Yaani itwaliwe mara moja.

Inginge maswala ya uraia. Uraia umekywa ni shida sana, kwa mfano, wa kuitwa an Arab. To be an Arab hii Kenya, hivi sasa imekuwa a crime. To be an Arab is a crime. Mimi mfano, ikiwa babangu ni Mwarabu na mimi ni Mwarabu in any way. Siwezi kuwa kabila lingine. Popote nitakapoenda mimi nitasema ni Mwarabu. Kwa hivyo. Ikiwa Serikali ina kabila ambayo, na mimi nimesema an Arab pia wasiwe ikiwa ni arobaini na tatu, au arobaini na nne pamoja na Wahindi. Kwa mfano kuna Wahindi wa Asia na Waarabu, wangukuwa tayari kabila katika Kenya. Kuwanyima na kutetea (Inaudible) ya bomb blast, ni mambo ya maonevu. Kwa hivyo, hii kitu kama hiki tusichukulie mambo ya bomb blast ikawa, to be an Arab is a crime. Kwa hivyo documents ambazo kwamba sisi twapenda kusema ukweli na twaapishwa katika koti na Quran, hatutaki kusema

uongo. Hata lile

(Inaudible) kwa hivyo ina

(Inaudible) kusema, mimi nitasema ni

Mwarabu hata kama nitauwawa, mimi nitasema ni Mwarabu. Kwa hivyo, ili ijulikane, an Arab iwe katika kifungu moja kwa moja iwe kabila katika Kenya. na Kenya tuwe tuko na kabila la watu Waarabu, kama nchi zingine zajua.

Uislamu, maswala ya dini. Kusiwe na uhuru wa

(Inaudible) kuabudu, hapana. Uhuru wa dini, uhuru wa

dini, uhuru wa kuabudu utakuwa ni mambo ya kufanya

(Inaudible) lakini uhuru wa dini ndio kifungu

kikubwa hakitaki kufanyiwa mambo ambayo kwamba yakuchezwa shere. Au ya matatizo kutoka afisi za Serikali. Kuwe kuna uhuru wa dini, ile dini wewe lazima uwe observed kwa namna yoyote ambayo kwamba umeamini. Hii ni kitu muhimu sana. Na Uislamu uitwe Uislamu. Hatukubali, -kama vile Katiba yoyote twaitwa katika Uingereza mpaka Kenya pia, wanatuita Mohamedans. We are not Mohamedans we are Muslims. Kwa hivyo iandikwe hiyo hakuna kitu kama Mohamedans, hakuna dini yaitwa Mohamedans. We are not Mohamedans we are Muslims. Iko mtu Mohamedan hapa?

Quran. Quran ndio kitabu katika Uislamu. Kwa hivyo, kukitokwa matatizo yoyote, ya mfano, nitatoa mfano ili muelewe vizuri makamishena, kama Salman Rushdin alitukana dini ya Kiislamu. Kitu kama hicho Kenya tayari kuwe kuna kifungu cha sheria za wazungu, dini, - hakuna uhuru au kifungu cha kuenda kumshitaki mwingine. Ambao kwamba, au tukutane vizuri. Kwa mfano mimi nitawaeleza nipatieni ruhusa, kama David, Solomon, Moses, Jesus wao wako katika Quran. Definitely Waislamu hawezi kuwatusi wao. Na Muislamu akiwatusi hao, Muislamu akimtusi Jesus he is not a Muslim. Kwa hivyo pia iwe Mohamed, mtu yeyote akimtusi Mohamed iwe ni hatia punishable in Kenya. Iwe ni hatia ambayo kwamba itachukuliwa kifungu maalumu, mtu asijaribu kutukana Mohamed, yaani Mtume.

Kisha, mfano, mtu mmoja ameeleza

(Inaudible) nilizungumza filsofia za Kanu ni filsofia za Nyayo. Na

filsofia za Nyayo, ni filsofia za Kikristo, na swali ni kwamba

(Inaudible) kwa hivyo wakaona vitu hivi

katika Kenya vimekuwa accepted, as a religious country. Kwa sababu President mwenyewe alisema Nyayo ni filsofia za Kikristo, kwa hivyo zaidi ya kuweka I.P.K kwa sisi, tulisema sawa, hatuoni tofauti nayo. Ikiwa ni filsofia za Kikristo. Haina maana kuwa tuwangoje Wakristo, kwa sababu huwa ile uhuru wa dini, kwa hivyo watupe kifungu Rais asiweze kutangaza kuwa Kenya is a Christian state. Hakuna ruhusa kusema Kenya ni dini fulani. Kuwe na kifungu namna hiyo. Kuwa isiwe Christian state kama Zambia vile alivyotangaza ni Christian state. Uislamu ukubalike, iwe an accepted religion, rasmi. Baada ya hiyo dini nyingine iwe ni second religion, na ambayo kwamba mtu yeyote ambaye kwamba, - kuna ni, - imekubalika rasmi kwa Serikali.

Elimu. Tukija katika elimu, elimu somo la sex education, totally we oppose, tunalipinga moja kwa moja. Kwa sababu mfano wa kusomesha condom, tayari kuna mtu mmoja alizungumza kwenye gazeti, -mwalimu labda-, alizungumza kuwa mtoto apewe chupa na condom, na aonyeshwe sasa kuvisha. Kisha ajue anaweza kufanya mapenzi na girlfriends more than five. Hayo mambo is not accepted katika uhuru wa dini. Kwa hivyo mambo ya sex education twapinga. Lingine katika elimu pia, elimu katika evolution. Somo la kusema binadamu alikuwa ni yonda is contradiction to Islam and Christianity. Kusema



(Inaudible) kwa hivyo wewe ukiambia mtoto skuli binadamu alikuwa ni yonda, mimi nitamwambia alikuwa ni Adam. Sasa wewe umpe direction, ni Adam au ni yonda, ateweza kufahamu sio? kwa hivyo to perform (Inaudible) ni nyani (Inaudible) kwa ijulikane hiyo.

..... (Inaudible) Human Rights: Haki za binadamu. Haki za binadamu ni lazima zijulikane katika polisi, labour, korokoroni iwe counselled. Kuwe mtumishi akiwa ameishi na mtu, hata kama ni mhalifu, akiwa prayer time, sio tena ku... -akiwa korokoroni polisi, prayer time wakati wa maulidi akubaliwe aweze, na Waislamu hawapaswi kwenye ibada, pasi ya kuwa na maji, wapewe maji ya kuweza ku-purify themselves, na (Inaudible) kuhairishwa, kuwe na right hiyo. Kisha na jela kuwe hakuna abuse of Human Rights, kuna mambo katika jela ya mateso, kama Ramadhani Waislamu wanapewa kazi ngumu, Ramadhani na huyo Muislamu asifikirie kivingine. Kwa sababu Ramadhani huwa ameitunza na hawezi kufanya kazi ngumu, na yeye, kwenye kifungu cha Kiislamu, uhuru wake na dini. Kwa hivyo ni lazima apewe ruhusa katika ramadhani kuwa anaweza kufanya kazi kwa masaa machache katika mwezi wa Ramadhani. Na pia kuwe kuna uchunguzi maalum katika hii Katiba, itembelee majela, kifungu maalum, watu ambao kwamba waweza kutumia nguvu au kutoheshimu mtu. Maanake kuna wengi kwa wanawake, mpaka kwa Wanaume, watu kunajisiana au kulawitiana. Kitu hiki Serikali ihakikishe hairuhisiwi katika majela.

Kitu kingine, Kenya ijue Uislamu ni mmoja. Lakini kuna sects nyingi kama ile dini zingine, kuna sects. Kwa hivyo Uislamu, Kenya schools of course, wengi majority ni Suni. Lakini twataka tupewe nafasi as shia minority, second after Suni katika Kenya, wawe na haki ya utu maalum, ambaye kwamba atapewa haki au certificate atapewa kama Kadhi, ikiwa hatakuwa employed kama Kadhi, lakini na elimu yake ikubaliwe ni sawa sawa na Kadhi. Na aweza kufanyia kesi ile ile kwa Kadhi yule yule. Na twakubali huyu hata asilipwe. Hatusemi huyu ni mhalifu hata asilipwe, lakini iwe Waislamu wa dhehebu la shia, waweza kuenda kushitakiana kwa watu ambao kwamba ni Makhadhi ambaye kwamba ni tofauti. Kwa sababu, ikiwa Kadhi atahitimu Katika School of laws ya dhulmin, ambayo kwamba, for example myself here, mimi nitakuwa sikukubali kwa hivyo rights yangu itakuwa imekiukwa. Kwa hivyo mimi sitakubali. Kwa hivyo mimi nina right ambavyo kwamba naona hivi ndivyo sawa. Na vile vile ndugu zangu. Lakini kuwe kuna special rights ya minority, ambayo kwamba ni shia, na ikiwa twasema minority, it's nearly a million now, katika Kenya. kwa hivyo wapewe rights zao, na mjumbe katika court, hakutakuwa kuna mtu mmoja, ni tatu. Mfano wa tatu.

**Com. Hassan:** Summarize.

**Ahmed Bajuba:** Okay. Kifungu kingine, hii sheria ya ... (Inaudible) kuna mtu mmoja aliingilia lakini nafikiria hakupambanua. Attorney General, hana uwezo wa kuingilia sheria ambayo kwamba tayari Waislamu ndio sheria yao imepitishwa, to modify. Mara nyingi twatoa ile memoranda and we realize it is null and void sheria ambayo imepitishwa na Chief Kadhi. Kwa hivyo hiyo tukitoa kwa statement, tumalize kuwa Attorney general hawezi kupangua. Hawezi kupangua kitu ambacho kwanza kilipitishwa na Waislamu.



Kitu kingine ni maswala ya kulawitiana. Oh, kunirathini jamani. Ushoga watu wangu. Homosexuality iwe moja kwa moja ni kifo. Hukumu ya kifo. Hanging up. Na sawa sawa na wanawake waliokwenda nao, hanging up, moja kwa moja.

Katika maswala ya election, election iwe ni... - hata kama mimi niko nje – niko Saudi Arabia, au niko Europe, naweza kuchagua niwe Mbunge au kiti nitakayo, pengine niko outside. Pengine nasoma, pengine nimekwenda kutalii, pengine nimekwenda kwa visit tu, kwa hivyo tuwe na haki. Lingine ambapo ni karibu la mwisho ni, Israeli state ikubaliwe kwa sababu Israeli is an enemy of Europe colony. Inanyanyasa Waislamu inanyanyasa Wakristo. Tena mambo ya mskiti, inaguzi makanisa, kwa hivyo Israeli should be termed as a terrorist state by Katiba ya Kenya, Constitution ya Kenya.

(Inaudible) Israel as a state

Christians.

(Inaudible) as a state terrorist in the Middle East, free for Muslims and

**Com. Hassan:** Tafadhali Mr. Jaribu kumaliza, eeh, Ahmed.

**Ahmed Bajuba:** Nishamiliza, almost. Kwa hivyo kitu kingine ambao kwamba ni muhimu sana, hii Katiba, lazima kuwe na kifungu ya kusikiza Katiba, haotoweza kutekelezeka. Tupewe (Inaudible) ikiwa Katiba ni ya – it is a Constitution, it is not implemented. Sasa itakuwa nini? Katiba hii, -ikiwa Katiba yalinda sheria, sasa Katiba italindwa na nani? Ama italindwa na nini? Sijui kama mnafahamu? Katiba ilindwe kisawa sawa. Katiba yalinda sheria, sasa Katiba yenyewe yalindwa na nini? Kwa hivyo ikiwa yale yote mazuri ambayo tunataka, kisha ikawa hayakutekelezewa, kwa hivyo kuwe kuna kifungu chasema kuwa mambo yalizungumzwa katika Katiba ni lazima yatekelezwe kwa namna ambayo kwamba inavyopaswa.

Mwisho, ni lazima siku ya kuzaliwa mtume Mohammed iwe ni holiday, kama Christmas. Si kwamba kumezaliwa prophet Mohammed iende hivyo. Na nyingine, kwa niaba ya community ya Shia, siku ya Ashura, Ashura day, the martyrdom of Imam Hussein, the grandson of the prophet iwe special for shia, kama diwali kwa Hindu. Iwe ni kitu ambayo kwamba watagusa katika Serikali. Kwa hayo machache natoa ahsante.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Ahmed kwa hayo maoni yako, mazuri tumezishukuru. Tafadhali tupigie signature hapo. Now, can we have Mr. Mahmoud Ahmed Abdulkadir.

**Mr. Mahmud Ahmed Abdikadir:** Bismilahi rwakhmani rahim. Asalaam aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Jina langu ni Mahmud Ahmed Abdikadir, wadhifa wangu katika jamii ni katibu wa ijumaa msikiti wa (Inaudible). Tukianza na mfumo wa utawala, napendekeza mfumo wa majimbo uliokuweco wakati Kenya ilipopata uhuru, ndio tunaupendelea zaidi. Na kuhusu jimbo la Pwani, napendekeza kufanywe marekebisho ya mipaka. Sehemu ya Taita Taveta isiwe tena katika Pwani, kwa sababu wenyeji asili wa sehemu hiyo wenyewe hajihesabu kama ni wa Pwani, wanajihesabu ni wa bara.

Itakuwa ni kama kuwaonea kuwalazimisha wawe katika Pwani. Kuhusu Rais, napendekeza apunguziwe madaraka na uwezo alionao, na asipunguziwe heshima na hadhi aliyonayo.

Rais awe kama Mkenya mwingine yeyote mbele ya sheria, asiwe na wadhifa zaidi ya mmoja, kama vile mkuu wa majeshi na kadhalika. Rais awe cheo chake ni Rais vivyo hivyo. Kuhusu Bunge, mtu yeyote atakaye kuwa Mbunge kwa kuchaguliwa au kwa kuteuliwa, - kuchaguliwa ni kujua kuwa na watu, kuteuliwa ni (Inaudible). Asiwe amewahi kushtakiwa kwa kosa la jinai, hata kama hakupatikana na hatia. Isipokuwa ijulikane wazi bila shaka yoyote kuwa shtaka alilofanyiwa halikuwa na haki, bali alishtakiwa kwa maonevu tu wakati huo, kushtakiwa kwake hakutakuwa na athari yoyote. Raia wawe na haki ya kumkataa Mbunge, baada ya kuchaguliwa kwa mwaka mmoja, ikiwa wananchi hawakurithika na huduma zake kwao. Na malalamiko yao yafikishwe kwa Tume ya uchaguzi, na watu wasiopungua asilimia kumi ya idadi ya kura alizopata wakati wa kuchaguliwa. Mbunge yeyote maalum, hafai kupewa cheo cha uwaziri, au naibu wa Waziri. Vyeo hivyo lazima vipewe Wabunge ambao walichaguliwa kwa kupigiwa kura na wananchi. Maswali yoyote ambayo yanahusika na masilahi ya Wabunge, wasiwe wao ndio wenye kuamua juu yake, kwa mfano swala la mishahara na marupurupu ya Wabunge, lisiamuliwe na Wabunge, bali kuwe na Tume maalum ya kuamua maswali kama hayo.

Ardhi: Ardhi ambazo zaambiwa, kuwa ni ardhi za Serikali, zinapogawanywa, nafasi ya kwanza wapewe wale watu ambao niwenyeji wa asili, wa sehemu ile ambayo ardhi hiyo ipo. Kadhalika mtu yeyote ambaye atapatiwa ardhi, basi asiwe na uwezo wa kuuza ardhi hiyo, wala kumpa riba mtu mwingine yeyote, isipokuwa akiwa mtu ambaye baina yao, pana haki ya kurithiana. Na mtu anapokosa (Inaudible) akawa na dharura kuuza ardhi hiyo kwa mtu wa kando, basi aruhusiwe kukodisha kwa kipindi cha miaka kumi ambayo yaweza kuongezwa mingine mitano, inapomalizika ile kumi ya kwanza, baada ya hapo, kila baada ya miaka mitano wanaweza kuongezea muda tena, pia wanaweza kufanya makubaliano mapya kuhusu malipo ya kuhairisha hii ardhi. Mtu yeyote asipatiwe ardhi zaidi ya ekari mia tano, hicho kiwe ni kiwango cha mwisho cha kupewa mtu ambaye ana mradi unaohitaji ardhi kubwa. Ardhi kubwa inayowekwa mradi isizidi ekari mia tano. Hata kama utashirikiana na watu zaidi ya mmoja katika mradi huo.

Uraia: Mkenyayeyote ambaye hana mahali pengine duniani, anaweza kusema mahali kwingine ni kwao na akakubaliwa, basi huyo awe na haki sawa na Mkenyayeyote katika wale Wakenya ambao wanahesabiwa kuwa ndio Wakenya halisi; zaidi bila kuangalia rangi yake, au dini lake, au kabila lake. Kwa mfano, kuna Wakenya wengi ambao wana asili za Kiarabu, lakini hawana hata mtu mmoja huko Arabuni, wala hawana mali yoyote huko, bali hata hawajui ni wapi mababu zao walipotoka. Wafika wajijua wao ni kuwa kwao ni Kenya na wao ni Wakenya. Kwa mtu wa aina hii, wanaposema ni Waarabu, ni sawa na Mkenyamwingine kusema ni Mbaluhya, au ni Mluo au na kadhalika. Unajua Waarabu wakiwa ni Waarabu, wamekuja mapema zaidi kuliko Wabaluhya, na kuliko Wakalenjin na kuliko makabila mengine. Kwa hivyo hakuna sababu kuwa ni hatia kuwa mimi ni Mwarabu.

Katiba lazima ithamini uhuru wa dini, sio tu uhuru wa kuabudu pekee yake. Kwa mfano, dini linamtaka mwanamke wa Kiislamu

kuvaa hijabu. Basi hiyo iwe ni haki yake ya kimsingi, ambapo ataweza kuitekeleza bila ya hofu wala wasiwasi, sawa akiwa ni mwanafunzi au ni mfanyaji kazi.

Watumishi wa Serikali: Mtumishi yeyote mfanyikazi wa Serikali, akiwa amefanya uharibifu katika mali ya uma, basi achukuliwe hatua za kisheria, sio kupewa uhamisho kutoka mji huu hadi mwingine, au uhamisho wa idara, jambo hili linahimiza ufisadi.

Vipengele vya Katiba: Vipengele vyote vilivyo katika Katiba na ambazo zatumiwa ... *(End of side A)*.

Hawafanyi chochote kinachobagua kati ya Wakenya, katika maswali ya kitambulisho...

**Com. Hassan:** Jaribu kumaliza...

**Mahmoud Ahmed Abdikadir:** Baadhi ya watu kabila langu umewapa muda mrefu, why not me?

**Com. Hassan:** Ngoja, kuna wale ambao wako na simu ya mkono ambayo iko on bado. Tunawaomba muweke off, kwa sababu ina-disturb hii recording system yetu.

**Mahmoud Ahmed Abdikadir:** Mimi nimechukua muda kutengeneza hii, nimesafiri leo kutoka Mombasa mpaka hapa kwa ajili ya hii.

**Com. Hassan:** Lakini nakuomba usisome neno kwa neno tafadhali, jaribu ku-highlight.

**Mahmoud Ahmed Abdikadir:** Haifikishi dakika kumi.

**Com. Hassan:** Na nakuambia usisome neno kwa neno.

**Mahmoud Ahmed Abdikadir:** Vipengele vyovyote vilivyo katika Katiba na ambavyo vyatumiwa kufanya mambo kinyume na Katiba, basi Katiba ijayo ihakikishe kuwa vipengele hivyo vimezibwa na hakuna tena kwa mfano, Katiba ya sasa haina kifungu chochote kinachobagua kati ya Wakenya katika maswali ya vitambulisho, na hali za usafiri- passport. Lakini hakika ya mambo ni kuwa ubaguzi upo, tena wa hali ya juu sana. Itizamwe ni kipengele gani ambacho kinatumiwa na wanao husika kuwanyanyasa baadhi ya Wakenya katika mambo ya passport, au katika ugawanyaji wa ardhi.

Kadhi, namaliza. Makadhi watakao andikwa kazi ya ukadhi, lazima kwa uchache wawe na shahada ya B.A. katika somo la sheria za Kiislamu, kutoka mojawapo ya vyuo vikuu, vinavyokubaliwa, au shahada inayolingana nayo. Kadhi lazima ajue lugha ya Kiarabu vizuri, au kusema, kusoma na kufahamu, kuandika na kuzungumza. Ni bora akijua na Kiingereza. Lakini si lazima,

akijua Kiswahili vyema si lazima kujua Kiingereza. Mahakama ya Kadhi iwe na uwezo wa kufanya kesi nyingine, mbali na mambo ya ndoa na talaka na miradi. Iwapo wanao husika na hiyo kesi watapendelea kesi yao isikilizwe na mahakama ya Kadhi, kama vile iliyo hali ya mahakama ya mila na desturi za kienyeji. Mahakama ya rufaa ya kusikiliza kesi za mahakama ya Kadhi, lazima iwe yategemea sheria za Kiislamu. Mahakama ya rufaa, uamuzi wake uwe ni wa mwisho. Mahakama ya Kadhi iwe na hadhi, na heshima kama mahakama nyingine za kanuni, ikiwa haitakuwa bora zaidi. Na hapa na-quote kitabu hiki.

Fungua hiyo (Inaudible) page twenty-two. Katika kitabu cha Katiba ya Kenya iliyo rahisishwa, ukurasa wa ishirini na mbili, kuna kifungu chaeleza hivi: ‘hata hivyo kuuu mtu yeyote hakutachukuliwa kuwa uvunjaji wa haki za kimsingi katika maisha, ikiwa ni katika kukomesha ghasia, maasi au mgomo. Au kuzuia mtu asitende kosa la uhalifu. Kifungu hiki chahitaji kusahihishwa, na pia chahitaji ufafanuzi, kwa mfano neno ghasia ni neno ambalo mambo mengi yaweza kuambiwa ni ghasia. Kwa mfano watu wakikusanyika mahali, na wakawa wanapiga kelele, tayari tendo hilo huwa ni ghasia. Je polisi wakiwapiga risasi, au marungu watu hao, wakawaumiza au kuwaua, haitakuwa wamewanyima haki zao za kimsingi? Na polisi watumia kifungu hiki, na mfano wa hiki katika kusumbua na kuhangaisha watu, wasio kuwa na hatia basi na kuwauwa wakati mwingine.

Mwisho kabisa, ukurasa wa thelathini, kitabu hicho hicho, ukurasa wa thelathini. Vile vile katika kitabu hicho hicho ukurasa wa thelathini fungu la nane. Karibu na mwisho, kuna ibara yasema, “mtu hawezi kulazimishwa kushiriki katika shughuli za dini, wakati akihudhuria shule iliyoanzishwa na kundi la kidini.” Yaani ikiwa wewe ni mwanafunzi umejiunga na shule ambayo asili yake ni shule ya kidini, kwa mfano Alliance, wasema hapa, si lazima kuhudhuria shughuli za kidini. Hiyo haitoshi. Lazima iwe hivi, neno shughuli za kidini halitoshi, lazima kuongezwe neno au masomo. Ili, ibara iwe hivi: mtu hawezi kulazimishwa kushiriki katika shughuli za kidini au masomo, wakati akihudhuria shule iliyoanzishwa na kundi la kidini. Nasema hivi kwa sababu watoto wetu, mara nyingi wanashindwa kusoma katika shule za kitaifa, kwa kuwa baadhi ya shule hizo huwalazimisha kusoma somo la C.R.E. Kama mfano wa Alliance Girls, ni lazima wanafunzi wachukue somo la C.R.E. akiwa ni Muislamu, akiwa ni Baniani, akiwa ni dini yoyote. Hii inasababisha wengi katika watoto wetu, waliombeleni ni wachache, waliopewa nafasi na wakakaa wachache inabidi wasiende, kwa sababu ya kulazimishwa kusoma somo la C.R.E. Kwa hivyo twapoteza nafasi zetu katika shule hizo. Kwa haya machache, nawashukuru kunisikiza, ahsante. Na hii kwa kuwa sikuandika nitaongeza kwa juu. Iko dharura ya kuwa na korti ya kikatiba. Yaani mtu akihisi amenyimwa haki yake ya Kikatiba, awe na mahali a naweza kuenda kushtaki. Maanake sasa Katiba yetu si mbaya hivyo. Kwa mfano mambo ya passport, Katiba haisemi watu wabaguliwe, lakini watu wabaguliwa, na mtu akibaguliwa tayari amenyimwa haki yake ya Kikatiba. Kwa hivyo, kuwe kuna mahali aweza mtu kuenda kushtaki kwamba mimi nimenyimwa haki yangu ya Katiba. Na hiyo tu, ndio njia pekee itakayofanya Katiba iweze kutekelezwa isibakie Katiba ni wino katika karatasi. Asalaam aleykum.

**Com. Hassan:** Aleykum asalaam.

(Inaudible) hiyo karatasi. Athman N. H. Saud...

**Audience:** Ameenda huyo.

**Com. Hassan:** Ameenda? Wale ambao wako na written submission na wanataka kuenda, tafadhali usiende bila kutuwachia hiyo submission. Ukitaka uende na hiyo. Betty Tet Baraza... hayuko pia. Melek Galole...

**Melek Galole:** Hamjambo (Inaudible). Najua kwamba sote ni watu wamoja. Watu wa sehemu hii ya Lamu, na sisi mpaka wakati tunapoonamba jambo si sawa, lije lisemeke, ili kwamba mnakamilisha kila kitu. Itakuwa ni sawa. Lakini ikiwa mmenyamaza, basi mwaonewa. Jambo moja, ni kitu kimoja ambacho tunaona utofauti, sisi katika sehemu hii yetu, na Serikali tuko pamoja nayo. Lakini sasa ni kwamba, jambo ambalo linafanyika wakati mwingine, panginepo lazima tuwe washauri, raia pamoja na Serikali, wakufahamikiana, ndio jambo jema. Lakini ikiwa moja yapo haitaki kusuluhishiana, basi hakutakuwa na mema. Kila mmoja atajua yeye la kufanya. Jambo ambalo kuwa mimi nataka kuzungumza ni kwamba, sisi tumeletewa Serikali ituchunge, na tuwe pamoja. Lakini sasa ni kwamba, wakati mwingine hatusikizwi kwamba mtu anajivunia. Wewe utakaposema unakatiwa katiwa pale maana mimi nina uwezo. Lakini sasa na mimi ni mwanadamu, mpaka unisikie. Najua ukinishika mimi utanipeleka kortini. Na kunipeleka kortini mimi kule nitatoka. Lakini sasa wewe hutaki kunisikia yale nisemayo tuelewane, sasa tunataka jambo hili liwachwe kwa ajili ya kwamba leo ni sehemu ya mwananchi. Na sehemu ya mwananchi hii, leo tunataka tuelewane. Ya kwamba sasa kuna sehemu ya Serikali, na kuwa na sehemu ya wananchi. Sasa leo imefika yangu, wewe Serikali hutaki kunisikia, leo imefika yangu na mimi sasa nataka unisikize. Ni kwamba ni lazima tuelewane. Mambo ya kwamba wewe huwezi kunisikia ya kuwa ....

**Com. Hassan:** Mr. ... Bwana Galole, tafadhali utupatie ma...

**Galole:** Mawaidha.

**Com. Hassan:** Hapana recommendation, - mapendekezo.

**Galole:** Mapendekezo ni kwamba, - yangu mimi, ni kimoja.

**Com. Hassan:** Bwana Galole, kwanza nataka unifahamu kabla hujaongea tena. Tunataka mapendekezo. Unafahamu sasa?

**Galole:** Eeeh! Haya mapendekezo yangu ni haya: sehemu ya msitu, sehemu ya msitu, sisi tunajua kuwa sisi hatuna pesa ya kujengea nyumba za mawe. Lakini sasa ile miti katika misitu ndio inatusaidia sisi. Lakini sasa leo ikiwa imepewa Serikali, sasa itakuwa ni ubishi. Maana upande wetu tutapewa hesabu ya kuenda kufanya, nenda ukakate miti fulani. Sasa ile miti mimi haitanitoshia. Inanilazimu mimi niongeze kwa ile ya sehemu yangu. Sasa ikiwa mimi, -yeye hatakubali, na ikiwa umefanya lako, wewe kule utatandikwa kabisa na ukija huku, kula langu. Maana ile mpini, ni yake yeye mwenyewe, amesema ni wake. Na atafanya lolote nawe hutafanya kitu. Sasa jambo hilo, ndilo sisi tunataka kwamba liwe na - sehemu ya msituni niwachiwe mimi mwananchi, nitaweka mtu wangu. Ili kwamba kutakuwa manufaa pale. Lakini nikikupa wewe ile sehemu yangu hutaki kuihifadhi, sasa hapo itakuwa, - hazitakubalika ni magongo tayari. Kwa hivyo sisi tunahitaji kwamba hii Serikali, hii misitu hii,

wakichukua wao, sisi hatupati chochote. Lakini sisi tunataka tuwe nayo sisi, na tutaikabidhi sisi. Hizo ndio maoni yangu. Kwa hivyo kutoka sasa, iwe kwamba maoni ya hii misitu watupe sisi. Ahsanteni.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Bwana Galole, tafadhali *utu-signie*. Amur Haji, Amur Haji... Ali Taro... Ali Taro ameenda?

**Audience:** Yuko.

**Ali Taro:** Asalaam aleykum! Nyinyi ma- Commissioner wenye kubadilisha Katiba, jambo la kwanza nataka kuwe na sheria kuhusu polisi. Polisi akiwa, - yaani kuwe na sheria ambayo itakuwa inamfaa polisi jinsi anavyokwenda kushika yule mtu. Si mtu ashikwe, akifika pale pengine ni mtoto wake anataka kumwona, akifika pale juu anaulizwa maswali mengi, 'wewe mama namna gani? Sijui kwa nini umeolewa na mwizi huyu? Akija kufanya utafiti inajulikana yeye ni mwizi, sijui nini...' maneno mengi ambayo yatukuwa yule mama yanamvunja na nini. Kuwe na sheria kama vile Tanzania ama Uganda, vile ndugu zetu ambavyo wamefundishwa, iwe ni hali ya kwamba polisi awe ana sheria maalum ya kuenda kushika mtu.

Na katika hizi Katiba ambazo zinabadilishwa hapa, kila tukisikia haki za binadamu ni Wazungu wanatoka huko, ndio wanakuja kuangalia haki za binadamu. Kwanini hatuwezi kuwa na kifungu cha kuangalia haki za binadamu hapa Kenya? Mnangoja Wazungu watoke huko ndio waje kuangalia haki za binadamu hapa, na sisi tuko hapa kila siku, sijui nini... kwa hivyo katika hizi Katiba ambazo mnaunda hapa, kuwe na kikundi cha kuangalia haki za binadamu. Tumepoteza watu wengi kwa sababu ya mtu tu, yeye ni mkubwa anaweza kufanya atakalo. Kwa hivyo kuundwe kikundi hapo, sheria ya kuangalia haki za binadamu. Jambo la tatu kama sisi Waislamu, ikiwa ni mgeni yeyote yeye si Muislamu, akiwa amefika katika kijiji cha Waislamu, ikiwa ni mwanamke awe ana nguo maalum ya kuvaa kulingana na ile sehemu. Si waende uchi, na watoto wetu sisi wanaiga na wao wanaenda, - sijui wako namna gani, na yeye anasema 'mimi ni raia, naweza kuishi mahali popote Kenya hii. Kuwe na sheria maalum.

Jambo lingine pia tuangalie katika hizi sheria, hii sheria ya uchukuzi na mawasiliano. Tunaona mtu anaendesha gari, anaangusha gari, anazungumza na girlfriend wake, anauwa watu wengi. Kwa sababu yeye ni mkubwa ama kwao kuna senti hawatachukuliwa hatia ya wale watu ambao wamekufa. Inapelekwa hapa na pale, anatoka na mlango huo mwingine anashuka chini, kesho unaona ako na gari nyingine upande ule anaenda. Kwa hivyo kuwe na sheria, mtu akiwa yeye ameangusha gari ile, iwe ni maisha hataendesha gari tena, wala yeye awe ataingia tu kwa gari nyingine wala hataona gari hiyo tena. Tumepoteza ndugu zetu, mama zetu, mabibi zetu, ndugu zetu kwa tabu kama hizo.

**Com. Hassan:** Endelea, endelea.

**Ali Taro:** Na kitu kingine pia ni kama hivi mumesikia ndugu zangu hapa wakizungumza mambo mengi. Tuna Navy wako hapa Bajuoni hapa, tuna Navy wanakaa hapa Bajuoni, wanakula hapa, wanakuwa hapa, wanajua kuzunguka hapo, wana magari

makubwa makubwa, - ndugu yetu amepotea hapa asubuhi, hata hatujamaliza masaa kumi na mbili. Na hatujaona Navy amefika hapa ndio wanakula mishahara mikubwa, wanaishi hapa tu. Na magari, ma-helicopter, kila kitu. Tumepoteza roho ambayo kama Navy wangelifika hapa wangukuwa wameweza ku... -ndio tunajua wazi kwamba Mwenyezi Mungu, siku zikifika huchukua roho ikaenda ile. Lakini katika ile hisia ya kibinadamu, tunaona kama wangelikuwa Navy, wangelifika chini ya saa moja, - na wako na manuari kubwa kubwa ziko hapa. Tumekaa sisi saa kumi na mbili na nusu, na hatujaona meli ya Navy imeingia huko. Na wakija kutembea, wanachukua meli kubwa kubwa na kuja kutembea, kuenda na magari mazito mazito yanapita huko, na hapo roho imepotea asubuhi pale Pwani, na hatujaona meli imeenda hapo, hatujaona nani amekuja hapo. Kwa hivyo kuwe na sheria, isisemekane ati lazima mkubwa ndio akiwa amekufa ndio kuonekane na nini...iwe wanadamu wote sheria itulinde tuwe sawa. Watu wote wawe ni sawa sawa. Kama kumeanguka ni mtoto, mpaka mara moja awe ni mtu, akiwa na miaka mitano awe ni mtu, akiwa ni billionaire awe ni mtu, akiwa yeye ana kila kitu, sheria iwe ni ya kisawa sawa. Hakuna kusema huyu ni mtu, huyu hana senti, huyu hana nini.

Na jambo lingine, katika hizi Katiba hizi, Bunge, kila Mbunge akae kule kwao alikochaguliwa. Mhakikishe Wabunge wote wakae kule walikochaguliwa. Maanake sisi Wabunge huwaona wakati wa kura hapa. Wakisha kuchukua magari makubwa makubwa wakipelekwa Muthaiga kule wakiishi majumba ya rangi nzuri, wakikaa huko, tunawaona sisi siku ya uchaguzi hapa. Kwa hivyo Mbunge awe ana-face the consequences za zile tabu za wale raia waliomchagua. Kama ni wa Mangai akae Mangai, kama ni wa sijui wapi akae huko, kama ni wa Lamu, ajengewe ofisi hapa. Mutakutana huko Bunge siku fulani, siku ile mtaambiwa ni siku fulani mje tukutane hapa. Wakakutane huko. Lakini sio achaguliwe hapa, kesho ameenda huko hatumuoni tena, hatujui hata yukoje? anakaa huko, mara ako Ulaya, mara yuko wapi, hiyo itakuwa si vizuri ndugu zangu. Kwa hivyo sheria hizi zetu nyinyi ndugu zangu, iwe ni haki Bunge hiyo, Mbunge akae kwao. Sio aende huko aendeshe magari makubwa, makubwa na nini huko. Hatumuoni amekaa, hata muda mwingi hatujui yuko wapi. Wacha sisi ambao tunasafiri mara Nairobi, - kuna wamama wanakaa Mangai ndani ndani chini huko, na hajaona Mbunge anakaa mahali gani hata siku hii. Ahsanteni sana.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Ali... Ali... kuja. Tupigie sahihi kwa hiyo kitabu. Kuna mama yeyote ambaye atatoa maoni? Any lady? Ushatoa? Ahsante. Kuna mtu yeyote, wale walemavu ambaye anataka kutoa maoni? Walemavu. Wewe ushatoa bwana. Nasema disabled groups ambaye hajatoa bado maoni? Hapana hujanifahamu mzee bado.

**Audience:** Asiyekiweza?

**Com. Hassan:** Asiyekiweza, kuna wale ambao bado hawajatoa maoni? Hakuna. Okay. Now we are through with this list, mzee unataka kutoa maoni?

**Mohamed Mbwana Shee:** Asalaam aleykum! Mimi maoni yangu bwana

(Inaudible).

**Interjection:** Jina?



**Mohamed Mbwana Shee:** Mohamed Mbwana Shee. Ninapendekeza kwamba Tume hii isifuate majority ya watu wanaotoa kupendekeza juu ya Katiba. Kwa sababu, ni kwamba sisi, tulipopata uhuru tulikuwa na Katiba yetu ya Majimbo. Katiba hiyo iliweza kuondoshwa wakati huo huo wa 1964. na hivi leo, utakuta kwamba Province zote za Kenya nane, hawatakubaliana na Katiba ya Majimbo, kwa sababu kila jimbo linatawala kijimbo, isipokuwa mkoa wa Pwani, ndio makabila yote wamevamia jimbo hili. Kwa hivyo tunaomba Katiba hii kwamba ukiwaeleza Katiba ya Majimbo, hawatakubaliana kabisa. Kwa sababu ile sababu iliyofanya wao kuvunja Katiba ya Lancaster house, ilikuwa ni sababu ya kutaka kuvamia jimbo la Pwani. Kwa hivyo sisi tunaomba, hii Katiba iangalie haki na usawa, na haki na usawa ni Serikali ya majimbo. Kwa hivyo isichukuliwe majority. Ikichukuliwa majority, ni watu wa Pwani pekee yake ndio wanaotaka Majimbo, lakini mikoa yote minane hawataki system ya majimbo. Kwa sababu kila jimbo linatawala na majimbo. Kwa sababu kila jimbo utakuta wamejitawala wenyewe kijimbo, isipokuwa mkoa wa Pwani ndio wamelivamia, kwa hivyo hayo ndio mapendekezo yangu.

**Com. Hassan:** Ahsante sana. Ahsante sana. Mohamed please sign for us the register. Kuna mwingine ambaye anataka kutoa maoni? Mzee....

**Ali Omar Said:** Salaam aleykum. Kwa jina ni Ali Omar Said. Mimi nina mapendekezo hapa ambayo nafikiria ni muhimu, kabla hii sheria hazijaweza kutekelezwa. Nilikuwa nikipendekeza kwamba ikiwa sheria itapitishwa, ikiwa hizi sheria zitapitishwa, kwa sababu, kama tulivyoona kwamba sisi hapa Waislamu ni wachache hapa nchini, kuna sehemu fulani za sheria ambazo zaweza kutulemea sisi Waislamu. Kwa hivyo ikiwa ni lazima sheria kama hiyo ipitishwe, basi Waislamu wawe wata...hawata lazimishwa kuifuata sheria hiyo. Kwa mfano, mwanamke anataka kuvaa hijab, na sheria ya Kenya hairuhusu mtu avae hijab; lakini Waislamu waona ni lazima wavae ile hijab, basi Waislamu wapewe ile nafasi ya kuvaa ile hijab kwa kutekelezea jambo lao la sheria ile ya Kiislamu. Ahsante.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Bwana Ali. Anybody else? Kule nyuma? Anza na jina.

**Alex Munyoki:** Majina yangu ni Alex Munyoki. Okay. Mimi yangu ni machache tu ya kuzungumzia kuhusu Katiba ya Kenya. Katiba ile itatuwezesha tuwe na usawa katika nchi hii yetu. Kitu cha kwanza, ndio tuwe sawa, na tusije tukanyanyaswa na wale wako na pesa nyingi, ni kuwa na independence. One: Judiciary must be independent. If there is anybody who has done or has committed corruption, he should be taken to the court. Because, majority in our country, they behave as if they are above the law. So you take them to the courts, the following day, there is no action. Kwa sababu ya hiyo, ndio sasa uchumi wetu unaendelea kuzoroteka. Na mimi ningetaka kuuliza kama ingewezekana, Judiciary iwe independent. Ndio mtu, hata kama ni Waziri akishikwa akipelekwa kortini, (Inaudible) aachwe ashikwe kama mahabusu yule mwingine.

Kitu kile kingine ni independence in the Electoral Commission. Hiyo itatuwezesha kuchagua watu wale tunataka bila kuwa na remote control. Kwa sababu mtu anaweza kusimama kwa sababu yuko na power in a certain post in the Government, he can



do remote control, anapita bila kuchaguliwa na wananchi. Kwa sababu ya hiyo, hizo sehemu mbili ningependa ziwe independent. Ndio tuchague watu wale ambao wataenda kutuwakilisha Bungeni, na watusikize sisi. Na waangalie kwa action. Kwa sababu bila kuangalia kwa action, hakuna, -hata sisi vijana hatutaona muelekeo katika maisha mema, maishani mwema. Kwa hivyo mimi hii Tume, ningependelea kwa hayo maswala mawili iangalie sana. Ahsante.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Alex. Mukimaliza kutoa maoni mutupigie signature hapo. Anybody, - wa mwisho wewe utakuwa. That's the last one. Ikipigwa (Inaudible) ya Mohamed, tunafunga hii kikao.

**Interjection. (Not clear) ...** Naitwa Francis Kiriga.

**Francis Kiriga:** Maoni yangu, nitazungumza kuhusu utangulizi wa Katiba yetu ya Kenya. Ningependekeza, Katiba yetu ianze na kumtambua mwananchi mwenyewe katika zile haki zake za kimsingi. Kwa mfano, Katiba yetu inaanza na 'Republic of Kenya.' Kwa hivyo ningependekeza ianze na haki zetu, na ieleze, na ifafanue kwamba mwananchi ndio mwenye haki ya kuwa na mali na imulinde mwananchi, ambapo ni rights zake zote impatie. Kwa hivyo isianze na Serikali, ianze na sisi. Mapendekezo yangu ya pili ni kwamba, Wabunge wetu, tuwe na fursa ya kuwaita waje hapa. Ikiwa ni mwaka mmoja tusingojee miaka mitano. Kwa hivyo tuwe tunaweza kuwaita, na isipite miaka mitano. Kwa hivyo tuwe tunaweza kuwaita, na tupige ile kura. Pendekezo langu lingine ni kwamba kuwe na fidia, ikiwa mtu amepolekwa jela, ama ameshikwa amewekwa kizuizini, akitolewa, kwanza siku ile ameshikwa, asiwe guilty, awe not guilty, mpaka awe proved guilty. Kwa hivyo akitoka pale akiwa hana hatia, alipwe fidia.

Pendekezo langu lingine, ni Constitution yetu. Wabunge wakiketi pale na waweze, wawe wanaweza kuifanyia amendments. Kwa hivyo ningependekeza waje kwetu hapa tuketi na wao, kisha, baada ya kukaa na wao, tupige kura, ndipo waende kule wapigie kile kipengele kura pia na wao, ili waweze kukirekebisha. Kwa hivyo wasiwe na uhuru kabisa wakubadilisha Katiba kama ni kipengele chochote.

Tume za Kikatiba. Tuwe pia na Tume za mikasa, hasa majanga ya kitaifa. Kwa mfano leo, tungekuwa na Tume hapa ingetusaidia. Kwa hivyo Tume hizi ziwe kila Tarafa, kila mahali Kenya, na Tume hii itatusaidia. Pia ningependekeza tuwe na Bunge mbili, ambapo tutakuwa na Prime Minister na Rais. Rais aangalie mambo yake ya kisiasa, na Prime Minister aangalie vile mambo ya Administration vile yataendelea. Kwa hivyo kuwe na Prime Minister na Rais, ndio zile nguvu zaidi ambazo amepewa zitapungua kidogo. Halafu ningetoa maoni yangu kwamba kuna zile agreement, saa hii tunalalamika kwamba hatuna title deeds, lakini kwa vile kuna ule ukoloni mambo leo, tuliachiwa na wale ambao walikuwa wanaishi. Kwa hivyo kila mmoja awe na title deed yake, na zile agreements ziwe scrapped kabisa. Kusiwe na agreement yoyote iendelee.

**Com. Mosonik:** Which type of agreement is that?

**Kiriga:** Kama zile za, - agreement ambazo zilikuwa kwamba ni Uganda, Kenya and Somali protectorate, zile zisiwe, kama zitakuwa revived. Kwa hivyo kusiwe na agreement kama hizo ambazo zitaleta – kama zile za Mazrui zile zimeshikana na hiyo.

Kuna kule ku-appoint, kama vile permanent secretaries wanakuwa appointed na Rais. Tungependekeza wawe na qualifications hawa watu. Na hawa watu wawe wakiangalia wawe independent kwa kazi yao. Mwisho nitaangalia, kuwe na sehemu fulani, katika kila mahali, kila korti, ambapo twaweza tukapeleka complaints zetu kama Ombudsman, ningependekeza hiyo. Ikiwa tumenyanyaswa tuende mahali tuandikishe ile, na tukisha andikisha ile, tutasema kwamba tumeonewa na ipelekwe. Hiyo kwa wakati huu tunaona kwamba, hatuwezi kupeleka malalamishi yetu kwa mtu yeyote, kwa vile tukisema tunaonewa, tunaenda kwa askari. Askari ndio Serikali. Kwa hivyo tunataka kuwe na chombo maalum.

Mwisho ningependa kutoa shukurani na kuomba, - muda huu tumepewa watu wa Lamu ni kidogo ya kutoa maoni yetu. Kwa hivyo tukependekeza tuongezewe muda na civic education, ningeomba kwa mapendekezo yangu pia, iendelee. Kuna zile kadi za kura pia. Muda ambao ulitolewa ni kidogo, na leo hii kuna wengi wamefikisha miaka kumi na minane. Kwa hayo machache, ahsanteni.

**Com. Hassan:** Ahsante sana Bwana Francis.

**Ali Abdala Shee:** Asalaam aleykum warakhmatulahi wabarakatu. Mimi jina langu ni Ali Abdala Shee. Ni Imam, na ni katibu wa msikiti wa Pwani. Mwanzo nikianza, naanza kwa ardhi. Ingawaje Bwana Commissioner wazungumza kwamba mambo ya ardhi, ama yasiregelewa mambo yaliyosemwa asubuhi, lakini asubuhi mimi sikuweko. Kwa hivyo mtanisamehe, lau nikizungumza, nikirudia mambo ambayo yamezungumzwa. Sisi wanadamu hatuishi kwenye mbingu wala kwenye anga. Sisi twaishi kwenye ardhi. Ardhi hii hapa kwamba twaishi, ni lazima sisi tuwe na nafasi, na tuwe na maeneo yetu sisi ya kuketi na kujenga, na kuweza kufanya kila kitu. Lakini la kusikitisha, kwamba katika Kenya, kuna mikoa minane, mikoa kama hii, yote mikoa minane utaona kwamba watu ambao wamerithi ardhi ni watu wale wa asili, ambao kwamba ni wenyewe. Lakini kwa maonevu, tukisema wazi kwamba maonevu ambayo tunafanyiwa sisi Waislamu, ambao kwamba katika Coast, au katika Pwani, wengi Waislamu ndio wao, pamoja na North Eastern. Huku kwetu utaona ardhi katika (Inaudible) yote au iliyobakia ni chache kabisa. Yote imechukuliwa na watu ambao kwamba si wa asili, watu ambao kwamba ni wageni. Kwa hivyo twasema sisi, au twatoa mapendekezo kwamba, ardhi yetu ya Coast Province ipewe watu wa asili. Na ikiwa itachukuliwa na watu, ikiwa ni wa bara, ni Wazungu na wengine wowote, kuwe na kifungu kupewa ridhaa, zile pesa walizitoa waregeshewe wenyewe, turegeshewe ardhi zetu sisi huku. Lau, ikiwa itaendelea namna hii, hatutakubali wala hatutakubali, kwamba ardhi zetu zaweza kuchukuliwa kinyang'anyiro. Yaani kila atayekuja apewa, pasi na sharti zozote, pasi na vipengee zozote. Bali sisi twaipa kheri kwamba ardhi ya Kenya, ikiwa ni Pwani, tunatakriban miaka elfu nne, kuanzia wazazi wetu, mababu zetu. Ambapo makabila makubwa yako ndani ya Kenya, ikiwa tukisema ni Wakikuyu, hawazidishi miaka mia tano, ikiwa ni Wajaluo, hawazidishi miaka mia tatu. Sisi tuko hapa ndani ya Kenya katika mkoa wa Pwani, takriban Waswahili, tuseme Waswahili, takriban miaka elfu nne na ushuhuda uko, mtu akitaka kuenda kumwambia kinaga ubaga.

Kitu cha pili ni Kazi. Kuhusu kazi twadhulumiwa, twanyanyaswa. Utaona katika maeneo yote ya Serikali, ikiwa ni makampuni, ikiwa ni kwamba ya watu binafsi, sisi Waswahili au sisi Waislamu, twanyanyaswa, na twaenezwa na twagandamizwa, hatupati nafasi za kazi. Vijana wetu wafaulu vizuri katika masomo, utaona wakienda kupeleka application ya kazi, nafasi kama zile, ikionekana majina ni ya Kiislamu, nafasi kama zile hamupatiwi. Na mkipatiwa, twapatiwa kama nzi mweupe. Sijui kama Commissioners mnajua nzi mweupe. Nzi mweupe. Nzi ni yule ambaye kama huyu ambaye ako hapa. Kwa hivyo Nzi mweupe ni yule ambaye kwamba si rahisi kumwona. Ni kama takriban alfu moja umuone moja. Ndio tunapatiwa nafasi kama hizo. Lakini ikiwa ni kupewa, twataka tupewe sawa sawa na wengine. Kwa sababu sisi hapa ni kwetu na tujifadhili, sisi ndio wazelando katika Kenya hii. Kwa hivyo ni lazima nafasi za kazi, kusiwe na ubaguzi. Mfano, sisi tunao ufadhili mkubwa, au utajiri mkubwa ndani ya Mombasa, ikiwa ni Port. Lau utakwenda kutembelea port, utaona kwamba sisi Waislamu, au sisi Wapwani asili, ni wachache sana kuliko Wabara, na wengine. Kwa nini iwe namna hii? Utaona hayo ni maonevu, na nafasi za kazi, ilikuwa mwanzo tupate sisi, kisha ndio wapewe wengine. Mfano ni kama ardhi. Ardhi ilivyo ni kwamba tisini asilimia – 90% tupewe sisi wenyewe, kisha kumi ndio waangaliwe wengine. Na kazi pia hivyo hivyo, kwa sababu huku kwanza tuangaliwe sisi. Kama tukienda sehemu nyingine, sisi hata hatutambulikani. Kwa hivyo ikiwa huku kwetu twanyanyaswa je? tukinda mahali kwingine tutafanya nini? Kwa hivyo Bwana Commissioner, hiyo ni mambo ambayo kwamba kuanzia wazazi wetu, mpaka sasa, na kila siku huzidi.

Ya tatu ni kuhusu Kadhi. Kadhi ni lazima awe atapata majukumu, au atapata cheo, kiasi ya Makadhi wote wa Kenya, wawe ni kama mahakimu yaani majaji, na Chief Kadhi awe kama jaji mkuu. Ikiwa hawi Chief Kadhi, ni Mkuu wa Sheria, lakini awe ni jaji mkuu. Ama kwamba Kadhi, ikiwa kesi kama ile imesikizwa, isiwe kuwe kutakuwa na ku- appeal, ama kuenda kwenye high court. Leo katika Katiba ya Kenya, yatupa kwa mkono wa kivuli, inatupokonya kwa mkono wa kushoto. Mfano, katika Katiba ya Kenya, si lazima Kadhi iongee katika kesi za baina ya talaka na ndoa, na miradi, kwamba mashahidi wawe Waislamu. Waweza shahidi ukamchukua Muislamu, na abaki Muislamu. Kisha ikiwa kesi, - wewe hukuridhika na uamuzi wa Kadhi, basi wewe una uwezo wa ku-appeal. Utaona huku mwatupa, huku mwatupokonya. Kwa hivyo ikiwa Kadhi anahukumu, mtu hakuridhika aende kwa Chief Kadhi, ndio ku-appeal kwetu. Hatutaki kwamba mumetupa kisha mwatupokonya upande mwingine, mwatupea mkono wa kuvuli mkitoa mkono wa kushoto. Huku mwatupa huku mwapokonya. Ikiwa mambo yetu ya Kiislamu, na sio, nataka mapendekezo yetu katika Uislamu iwe mambo matatu. Kuoana na kuachana, na miradi iwe ni mambo yatengezwa kama kifungu cha katika Katiba, kuna maegezo ambazo ni sheria, huno ni upungufu ambao Kadhi wetu hawakuegeza. Lakini umefanya marekebisho, umeegeza mambo kadhaa. Kwa hivyo katika Katiba hii yetu, ni lazima mambo kama hayo, yafikiriwe na uamuzi wa Kadhi na Chief Kadhi ukipitishwa, kwa aya za Qurani, na hadithi ya mtume ambayo Mwenyezi Mungu asema, (*He quoted a verse in Arabic from the Quran*). Hakuna katika muumini mwanamume wala mwanamke, Mwenyezi Mungu akisha kupitisha jambo na mtume, hakuna uwezo wewe wa kupinga. Kwa hivyo ikiwa wewe ni Muislamu, una imani kamili, Kadhi akisha kutolea aya na hadithi au Chief Kadhi, uwe ni lazima utaridhika.

Hatutaki tena mambo ya kuenda kwa high court, wala Makadhi wengine. Na Kadhi, ni lazima awe mwanzo ni Muislamu,

Muislamu mwenyewe aliye barabara. Sio Muislamu wa kanzu na kofia. Awe ni Muislamu, hana shari yoyote ya Kiislamu. Kadhi kama huyo, ajue nyumba ya Kiarabu, Kadhi kama huyo ajue Quran. Mwanzo kuna Makadhi ambao kwamba waandikwa, Quran yenyewe hawaifuati. Kwa hivyo twataka Makadhi ambao kwamba wajua kusoma Qurani mwanzo. Kisha wawe wamehifadhi nusu kadhaa. Kwa uchache wawe wamehifadhi nusu tano. Kumi, - uzuri awe amehifadhi msafu mzima Kadhi. Lakini lau haipatikani, basi nusu au robo ya Quran hawaipati. Kuna wengine, sijui swaakhma hawaipati na hao ni Makadhi. Na haya mambo tumefanya utafiti, na tumepata kwamba kuna Makadhi wengine, Quran yenyewe mayata hawaipati, kisha tumewekewa kwamba wao ni Makadhi. Kwa hivyo ni lazima Makadhi wawe waipata Quran vizuri. Kisha katika hao Makadhi, wawe wamaliza kulia, yaani kulia kamishena ikiwa hivi ni Kiarabu, kusema college. Wamemaliza college ya sheria. Ambapo sheria ukienda kusoma, wasoma sheria zote za ulimwengu, mwanzo ukisoma sheria ya Kiislamu. leo Makadhi wahukumu, mtu asikiza kesi ya mwanamume na mwanamke, akimaliza atoa hukumu yake, pasi na kifungu chochote cha sheria. Kadhi ajue Quran tafsiri vizuri, tena ajue na hadithi za Bwana mtume Mohamed swala salaam. Kwa uchache ajue swakher bukhari, swakher Muslim, ikiwa ni (Inaudible) na zingine zile sita. Au (Inaudible) kubwa awe akipata vizuri. Kadhi mwenyewe lau utampa hadithi kuisoma, hahisi kumeandikwa nini. Leo kumechukuliwa Makadhi wamemaliza form four, kisha baada ya miezi mitano, miezi sita, huyu apewa kazi. Hatuwezi kukubaliana na hayo namna hii. Kwa hivyo Makadhi ni mahakimu, na ni wenye kusimamia matatizo ya Kiislamu, lazima mambo kama haya yaangaliwe vizuri.

Jambo lingine ni upande wa masomo. Ni upande wa Rais. Rais ana madaraka makubwa, madaraka yenyewe yamempita mwenyewe. Rais ni mkubwa wa nchi. Rais huyu ni mkubwa wa Serikali. Rais huyu ni mkubwa wa majeshi. Lini Rais alikuwa mwanajeshi? Mfano mmoja tu. Rais aliwahi kuwa hata siku moja? Pengine lau utampa bunduki, aekeze kitu ambao kwamba kina upana mkubwa, atairusha juu ama ataiweka chini, kisha awe ni mkubwa wa majeshi. Mfano mdogo. Kwa hivyo Rais awe kiti chake ni cha urais. Masaada ya kuwa majeshi, masaada ya ukuu wa nchi, hivi ni vyeo vingi, na ni vyeo vikubwa, ambayo kwamba yataka mtu, ambayo kwamba vyeo kama hizi atazitengesha. Wataka kumvisha mtu kofia tatu, au zaidi ya tatu, atazivaa vipi? Na kichwa ni kimoja? Lazima kofia uvae kwenye kichwa kimoja. Huwezi kuvaa kofia zaidi ya moja. Au sio? Kwa hivyo Rais ana uwezo mkubwa, ambao uwezo wake, -juzi tu amezungumza kwamba uwezo huu lazima upunguzwe. Kwa nini kuzungumza namna hii? Ni kwamba yeye afunga virago aenda zake, mwingine asipande. Kwa hivyo sisi twasema wazi kwamba Rais, asipewe uwezo kama alivyokuwa nao, Rais wetu huyu wa sasa. Kwa hivyo ni lazima apunguziwe Rais vyeo vyake, ambao kwamba kwa uchache ni hivi. Na zingine Rais amchagua mkuu wa sheria, Rais awapa Mawaziri awatakao, haangalii watu ambao kwamba wanastahili, wanapeana kikabila, au kwa kujuana. Kwa hivyo ni lazima vyeo kama hivi vipunguzwe kwa marais wetu. Iwe Rais ni mkubwa wa nchi, na iwe kama England.

England ukija fahamu, malikia Elizabeth, yeye ni mfalme, hata si Rais. Sindio Bwana Commissioner? Lakini, lau malikia amekugonga wewe utakwenda kumshtaki. Waweza kumwambia malikia, kwamba wewe umefanya makosa kadhaa, kwa hivyo mimi nimekufungulia mashtaka. Haya njoo hapa awe Rais, Bwana Mtukufu Rais Daniel Toroitich Arap Moi, mimi bwana umenikosea, uangalie, hutodara kiapo, utachukuliwa juu kwa juu. Kwa hivyo Rais ni lazima apunguze madaraka yake.

Kisha upande mwingine ni upande, - na haya mambo lau ni kwa haraka haraka, kwa sababu mafundisho yote tumepata katika Uislamu, Mtume Swala Asalaam alipo, - mwanamke mmoja alipojenga (Inaudible) na mwingine, wakawa wanafanya uihairia, akiwekwa pale, akifanya makosa mtu ambaye kwamba ni Shariff Mtukufu, enda mlango wa nyuma. Ambayo kwamba ni karibu ndio kupatiwa adabu. Mtume Wasalaam ikikutokezea kisa cha mwanamke uwadhan mahsumia kuihepa, ataendewa na kijana cha zege aitwa Usama, akasema kwamba Swalalahu katika mambo kama haya uyaondosha katika mlango wa nyuma. Mtume akasema maneno yake Mtukufu, lau la... (*Quotes in Arabic*). Akamwambia Usama kwa ukali, Laha ni mtoto wangu mwenyewe Fatima, (Inaudible) ningemkata mkono. Haya tuangalie mambo yalivyo. Mimi na wewe tukifanya twafungwa twateswa, lakini wengine wakifanya na wakihepa, wanahepa huku na wanaenda kuwekwa kwingine. Na huku wamemaliza na huku wasibakishe kabisa. Kwa hivyo ni lazima madaraka ya Rais yapunguzwe.

Upande wa bahari. Bahari bwana Commissioner, ndio masomo yetu, ndio mavuno yetu katika mkoa wa Pwani.

**Com. Hassan:** Nakuomba tafadhali u-summarize ile point imebaki.

**Ali Abdala Shee:** Nifanye haraka haraka?

**Com. Hassan:** Summarize, eeh, fupisha.

**Ali Abdala Shee:** Kwa hivyo mimi naenda kwa urefu, sio?

**Interjection. A lady in the audience:** Fanya mukhtasari.

**Ali Abdala Shee:** Haya, bahari jamani ndio mavuno yetu, na ndio yaani mapato yetu. Kwa hivyo Bwana Commissioner, twaomba sisi watu, tukizungunza mara, hutupanda waelewa kwa hamasa. Kwa hivyo ikiwa tumekosea mara ingine mwaweza kuchukulia ni ubinadamu. Kwa hivyo bahari, ndio machumo yetu, ndio mavuno yetu. Ni lazima bahari iangaliwe vizuri. Sisi ni watu ambao kwamba ni masikini huku kwetu, na Serikali ni lazima iangalie vizuri kuhusu swala la bahari. Bahari, - juzi tu kulitokwa mambo ya wa Amerika kuja hapa kutembelea bahari, watu takriban wiki mbili hawana chakula, hawana chochote. Na waliosababisha ni watu kama hawa. Kisha tumeekeza vikwazo vikubwa Bwana Commissioner, kuhusu bahari. Watu watoa makodi makubwa makubwa, mara kumeekwa game park sio? Reserve park, marine park. Yaani mahali kumetengwa masamaki makubwa makubwa, wale ambapo (Inaudible) ma-tourist wakija hapa watalii, wanapata pesa nyingi ndugu zetu mabaharia, lakini mahali kama zile zimewekwa, Serikali pesa zile zaingia upande wao, sisi huku masikini twaumia.

Kingine ni kwamba zaja meli kutoka China na Japan, zakuwa mpaka hizi dagaa, mwajua zile dagaa Commissioner? Zile visamaki vidogo kiasi kama vidole. Zote zinachukuliwa na mameli kama haya. Kwa hivyo ni lazima mameli kama haya, yaangaliwe vizuri kwa sababu baadhi ya ndugu zetu waenda baharini hata kitoweo, mnajua kitoweo? Nisije nikazungumza ikawa hayaandikwi. Ni vizuri kama...

### **Interjection. Laughter.**

Kitoweo ni kile chakula cha kula mwenyewe, pia hawapati. Waenda karibu wiki nzima. Kwa hivyo ni lazima watu kama hawa wawekewe roadblock kwamba bwana hamuna ruhusa wa kutia jambo kama hili katika bahari, au sio jamaa? Kwa hivyo huno ni upande wa bahari. Kwa hivyo bahari yetu ndio... -na upande wa mikoko, pia mikoko...

**Com. Hassan:** Ngoja kidogo, unajua tunachukua hii tape, it is live inachukuliwa. Kwa hivyo usiwe na wasiwasi. Hata kama hatujui Kiswahili, huko Nairobi –recorders- kuna wale Waswahili ambao watajua hiyo.

**Ali Abdala Shee:** Sawasawa. (Inaudible) kuchapa upepo tu.

**Com. Hassan:** Hapana. Sio kwamba (Inaudible).

**Ali Abdala Shee:** Kisha mengine ni kuhusu mikoko. Mikoko Bwana Commissioner, umesikia mara nyingi watu wa Pwani, ama haswa wa Lamu, wanapiga makelele kuhusu mikoko. Mikoko ndio mavuno yetu, sisi tukiinukia, -mimi haswa babangu alikuwa ni mkataji mikoko. Kwa hivyo mikoko ni lazima kwamba kila siku tukiinukia sisi, ilikuwa ikija meli na mabomu kutoka Arabuni na India na Iran. Meli kama hizi haziji tena, kwa sababu kila siku imekuwa ni vikwazo, hufunguliwa ikifungwa. Hapa twapiga mayowe kila siku, mangungi yasije tena yaingiie katika ukingo huu. Lakini, uchumi wetu wa mikoko, utaona kila siku lina matatizo mpaka watu wenyewe wameanza ku-affect, yaani wameanza kuvunjika moyo, hawataki tena kufanya kazi ya mikoko, kwa sababu Serikali haina imani nayo kuhusu kazi kama hii. Kwa hivyo tunaomba kwamba katika Katiba, lizungumzwe swali kama hili, iwe mikoko ni (Inaudible), iwe mikoko itakuwa wazi watu waikate, isipokuwa tu kukatwe kwa mipango. Kumekatwa kopo hili, kuendelea na kopo lingine.

Nikimalizia ni kuhusu masomo. Masomo, -sisi twanyanyaswa, na (Inaudible), na twagandamizwa. Sisi watoto wetu mashala, kwa vile kwamba tunapata protini, yaani samaki, tunakula sana, akili zetu sisi ni kali sana kutoka huku. Lakini la kusikitisha ni kwamba, watoto wetu wakifanya vizuri, zile zikitoka results, vijana wakipeleka maombi katika upande wa maskuli –National schools- ikiwa ni mambo ya college, ikiwa ni mambo ya kuenda university, utaona nafasi kama zile zetu zinalaliwa, kisha zinapewa zingine ambao kwamba si sisi. Ambao mtu pengine amepiga A, ama amepiga B+ , anachukuliwa mtu ambaye amepata B plain. Haya ni mambo ambayo kwamba yako dhahiri shahir, na ushuhuda uko, ambao kwamba kwa upande wa masomo, na kwa upande pia wa makazi, utaona sisi twanyanyaswa, na twaenezwa. Na sisi twajigamba kwamba

katika Kenya si kidogo, watu wasema ni kidogo. Ikiwa Kenya kuna watu milioni thelathini, sisi Waislamu ni miliono nane. Ni kama sisi ni robo ya Kenya. Kila watu wakiwa wanne, sisi huwa ni mmoja katika wanne. Kwa hivyo sisi si wachache. Ni lazima jambo kama hili liangaliwe.

Nikimalizia la mwisho ni kuhusu kitambulisho. Sisi kuhusu mambo ya kitambulisho Bwana Commissioner, na pia nimesikia kidogo imetajwa, kwamba ukienda kule waambiwa ulete birth certificate ya babako, ya mamako, ya nyanyako, ya nyanyake nyanyako, ambao kwamba nyanyake nyanyangu pengine alikufa kabla uhuru haujapatikana. Kisha mtu ananiambia mimi nataka birth yake. Ambao kwamba birth imeanza kwa miaka,- ikiwa sikusahau ni sabini na kitu. Sasa utaona kwamba yote hayo ni katika unyanyasaji na kutufanya sisi wapwani, ambao kwamba ni waasili, kwamba sisi si wanakenya. Sisi kwamba ni Waarabu. Twakubali kwamba sisi, asili yetu ni ya Waarabu, lakini twasema kwamba sisi ni Waswahili, ambao Waswahili wamekusanya makabila mengi, ambao kwamba katika Kabila lililotajwa katika Katiba, namba ya arobaini na mbili ni Wabajuni, Wabajuni si Waswahili, Wabajuni ni sehemu katika Waswahili. Waswahili wako makabila mengi. Lakini twaonekana Wabajuni, ni watu ambao kwamba vichwa vyao ni vigumu, lau hawatoandikwa kupasha habari. (Inaudible) kabila laitwa

hivi. Hili ndilo lengo lilifanywa na Serikali likawekwa kwa... mimi mwenyewe naitwa hivi ni Mbajuni. Ni Mswahili. Lakini utaona Waswahili wako Wajomvu ni Waswahili, Wa Kilindini ni Waswahili, na wengine na wengine. Wengine siwakumbuki vizuri. Lakini ni makabila mengi, makabila. Lakini halikuzungumzwa Waswahili, wazungumza kwamba lugha ya Kiswahili iko, lakini Waswahili hakuna. Mambo gani hayo? Afaa ya (Inaudible). Vipi kuweko Waswahili, kuweko lugha waswahili wasiweko? Kwa hivyo hii yote yalikuwa ni kufanya kwamba sisi tusijigambe wala tusinene, kwamba sisi ni Waswahili. Ukienda kwenye kitambulisho ukisema mimi ni Mswahili, waambiwa 'hakuna kabila hiyo!' hebu sema kabila yako vizuri. Kwa nini? Mimi ni Mswahili, hata ukanipeleka wapi, mimi nitakuambia ni Mswahili. Lakini, mambo kama haya yakifundishwa kwa skuli, watu wameinukia mpaka mtu ukimwambia kwamba mimi ni Mswahihili, mtu akucheka. Lakini ukisoma geziti vizuri, ukisoma hizi, utaona kwamba Waswahili miaka kabla elfu nne, walikuwa wakiteka ngamia upande wa China na Japan kwa mfalme, na tukaweka punda milia, na majumba ndio yasije yakakuta, -tunayo Lamu Zanzibari (Inaudible) na kadhalika Zanzibar. Hii yote ni kuonyesha kwamba Waswahili ndio sisi. Kwa hivyo Bwana Commissioner, upande wa vitambulisho twanyanyaswa, upande wa passport ni juu zaidi. Wapekwa miaka na ziaka, nenda rudi, na pengine mpaka uchoke usi...

**Com. Hassan:** Umechukua karibu dakika arobaini sasa, tafadhali jaribu kumaliza.

**Ali Abdala Shee:** Eeh! Kwa hivyo ndio namaliza. Kwa hivyo Bwana Commissioner, zaidi zaidi, ya kwamba haya tulioyazungumza, hatutaki Katiba iwe ni Katiba imeandikwa ni kama kitu kimeekwa michicha. Twataka Katiba ambayo kwamba itatumiwa katika maisha yetu. Na Katiba ilindwe, iwe ni kanuni. Kama sisi lau tutaambiwa twataka Katiba, sisi twataka Quran na hadithi, ndio Katiba yetu Waislamu. Lakini tuko nchi ambayo wewe ni Muislamu mwenzangu, tuko nchi ambayo kwamba haifuati sheria za Kiislamu, ni lazima tufuate mfumo ambao kwamba uko. Lakini twatetea kwamba Waislamu ni lazima na wao wapewe haki zao, na hii Katiba ambayo yatungwa, isiwe ni kama Kiswa, - ama ni kama ile Katiba



iliyokwenda kuzungumzwa na kupangwa Lancaster House. Ilipangwa na huku kwetu kulifanywa mambo mengi, lakini hata moja hatukupatiwa.

Nikimaliza kwamba napongeza na kuisitiza, twataka majimbo. Sisi twataka majimbo. Iwe sisi tujitawale wenyewe, mambo yetu yote tutafanya wenyewe, hatutaki kuingiliwa. Kila mtu aende kwao. Wasalaam aleykum, ninapotoa shukurani kubwa kwa kunipa nafasi kama hii.

**Com. Hassan:** Ahsante sana (Inaudible). Tafadhali tupigie signature hapo. Hiyo itakuwa sasa mwisho wa ... (Inaudible) kwa hivyo utatusamehe, twataka kufungunga hii... this program of the day. Kesho tutakuwa tukienda Mpeketoni Catholic Church Hall. Sijui iko wapi? Lakini kama iko karibu, kuna wale hatujasikiza bado, mnaweza kuja huko pia mtoe maoni. Ningependa kumwita chairman wa Constituency Committee, Bwana Abubakar Almudi, aje hapa mbele ndio tuweze kufunga hiki kikao cha Katiba. ... (Inaudible). I am looking for the Chairman of the C.Cs.

**Abubakar Mohamed:** I am the Chairman but ... (Inaudible).

**Com. Hassan:** I am sorry, he is going to represent the chairman.

**Abubakar Mohamed:** ... (Inaudible) nimechukua fursa hii kuwashukuru ma-Commissioner kwamba wameweza kutekeleza ile ahadi, ya kuweza kufika hapa leo kupambana na program. Jina –Abubakar Mohamed. Kwa hivyo, kwanza ningependa kushukuru Commissioners, kwamba wameza kutimiza ule wajibu na wameweza kufika hapa, kama kulingana na program walioiweka. Pili ningependa kuwashukuru coordinator, na Bwana Kassim, kwa kutayarisha mambo haya kikamilifu. Kama mulikuja hapa hamungekuta pengine watu. Kwa hivyo wameweza kufanya haya matayarisho, mpaka mkaona watu wamejaa hapa kwa matangazo, kwa views. Ilikuwa nzuri na arrangements. Kadhalika, sitawasahau wananchi kwa kujitokeza wote kufika hapa, group mbali mbali, na kuweza kutoa maoni yao, bila hofu, bila wasiwasi, na wamejieleza vizuri, wametoa mapendekezo mazuri, na hakuna hata mmoja ambaye aliyekatazwa. Ikiwa mtu mwenyewe ametoka, na hakurudi tena, hiyo ni makosa yake. Isispokuwa tu mulichelewa, na watu wengine walipoona kwamba muchelewa, walianza kuwatazama. Lakini twashukuru kwamba mumefika na mambo yote yamekwenda sambamba kabisa. Kwa hivyo twawaombea safari njema Mpeketoni, na haya yote ni matumaini yetu ya kwamba yatatiliwa maanani, na tutaona matunda yake siku za usoni. Kwa hayo, twamuomba Sheikh Ali, atoe maombi, tufunge mkutano huu. Ahsante.

**Sheikh Ali:** Prays in Arabic.

Meeting ended at 5.30 p.m.

